

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

## BUNGE LA TANZANIA

### MAJADILIANO YA BUNGE

#### MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 20 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

#### MASWALI NA MAJIBU

Na. 170

#### Ujenzi wa Dampo la Kisasa - Dar es Salaam

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika haraka za kujenga dampo la kisasa Jijini Dar es Salaam zinahitajika shilingi bilioni 12 katika kuboresha huduma za uwekaji taka kitaalam:-

- (a) Je, Serikali inajizatiti vipi na hali hiyo?
- (b) Je, Manispaa zote tatu zilizopo Jijini Dar es Salaam zina bajeti ya kutosha?
- (c) Je, ni sehemu gani katika Manispaa hizo ambako dampo hilo litajengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuliweka Jiji la Dar es Salaam katika hali ya usafi kwa kubuni mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga/kuendeleza eneo maalum la kutupia taka ngumu kitaalam (*Sanitary Landfill*). Jumla ya shilingi bilioni 12 zinahitajika kwa ajili hiyo. Fedha hizi zitatumika pia kununulia mitambo, magari na vifaa vingine maalum vya kuendeshea eneo hili. Kuanzia Machi, 2004, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia Wataalam Washauri (*Consultants*) itafanya utafiti wa kina wa athari za kimazingira (*Environmental Impact Assessment - EIA*) katika eneo la Pugu Kinyamwezi. Utafiti huu unatarajiwa kukamilika katika muda wa miezi miwili. Baada ya utafiti kukamilika, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Serikali, itakaribisha wawekezaji.

Tayari nchi za Canada, Denmark na Japan zimeonyesha nia ya kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika kujenga eneo la kisasa la kutupia taka ngumu kitaalam (*Sanitary Landfill*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Bajeti ya Mpito cha Januari hadi Juni, 2004, Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke na Halmashauri ya Jiji la Da es Salaam, zimetenga jumla ya shilingi milioni 36 kwa ajili ya utafiti wa kina wa athari za kimazingira kwa maeneo ya Chamazi na

Pugu Kinyamwezi. Baada ya kukamilika kwa utafiti, Halmashauri zote kwa pamoja na kwa kushirikiana na Serikali, zitatafuta mwekezaji katika Mradi huu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika tathmini ya awali (*Feasibility Study*), maeneo mawili ya Chamazi katika Manispaa ya Temeke na Pugu Kinyamwezi katika Manispaa ya Ilala, yalikubaliwa kufanyiwa tathmini ya kina ya athari za kimazingira. Eneo la Chamazi limeshafanyiwa utafiti mwaka 2003 na eneo la Pugu Kinyamwezi litafanyiwa utafiti Machi, 2004. Baada ya utafiti wa eneo la Pugu Kinyamwezi kukamilika, Halmashauri zote kwa pamoja zitakuwa katika nafasi nzuri ya kuchagua ni eneo gani linafaa kuendelezwa.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali lifuatalo: Kwa kuwa Miji mingi Tanzania inaonyesha kwamba itakua kadri *population* inavyoongezeka na hakuna dalili angalau za maandalizi za kutengeneza madampo kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Je, kwa hili Serikali inasemaje? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hilo linatambulika na Serikali na kama mnavyofahamu, karibu Waheshimiwa Wabunge wote, tumekuwa na mpango wa uendelezaji wa miji yetu na katika mpango huo (*USRP*), kulikuwa vilevile na *component* ya utengenezaji wa madampo ya kisasa katika Miji ambayo ni Manispaa nane. Juzi kama mtakuwa mlipata bahati ya kuona, nilikuwa Dar es Salaam kukabidhi vifaa kwa ajili ya madampo hayo manane ambayo yamegharimu Serikali kiasi cha shilingi bilioni moja. Kwa hiyo, juhudi hizi zitaendelea vilevile kulingana na hali halisi itakavyokuwa inaendelea.

Na. 171

#### **Huduma katika Hospitali ya Mwananyamala**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA (k.n.y. MHE. ROSEMARY H. K. NYERERE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mwananyamala iliyopo kwenye Wilaya ya Kinondoni ni moja kati ya hospitali zinazolalamikiwa sana juu ya huduma zisizoridhisha au uzembe:-

- (a) Je, katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 hadi 2002 ni malalamiko mangapi yamepokelewa kuhusiana na huduma zisizoridhisha au uzembe?
- (b) Je, ni vifo vingapi vilivyotokana na huduma zisizoridhisha au na uzembe wa watumishi wa hospitali hiyo kwa kipindi hicho?
- (c) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wahusika na Serikali imeweka utaratibu gani kama hatua muhimu na za makusudi za kukomesha mwenendo huo mbaya kwenye hospitali hiyo na nyinginezo kote nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 hadi mwaka 2002 jumla ya malalamiko 21 yamepokelewa na uongozi wa Manispaa ya Kinondoni kuhusiana na huduma zisizoridhisha au uzembe wa watumishi wa Hospitali ya Mwananyamala.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1999 na 2002 vifo sita vilitokea kutokana na aidha, huduma zisizoridhisha au uzembe wa watumishi wa Hospitali ya Mwananyamala.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji kazi wa Madaktari unatawaliwa na Sheria ya Madaktari wa Binadamu na Meno Sura 409 ya mwaka 1959 kama ilivyorekebisha na Sheria Namba 24 ya mwaka 1968 (*Medical Practitioners and Dentists Ordinance of 1959 Cap.409*). Utendaji wa Wakunga na Wauguzi nao unatawaliwa na kifungu cha (V) na kifungu kidogo cha (1)(L) cha Sheria ya Usajili wa Wakunga na Wauguzi Namba 12 ya mwaka 1977 (*The Nurses and Midwives Registration Act, No.12 of 1997*). Hatua mbalimbali za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya wahusika kutokana na msingi huo ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha kazi, baadhi yao kupewa onyo na wengine walifukuzwa kazi. Jumla ya watumishi 17 wa kada mbalimbali walihusika na hatua hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyowekwa na uongozi wa hospitali hii kama hatua muhimu ya kukabiliana na mwenendo huo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- (i) Kubaini watumishi ambao utendaji wao wa kazi ni mbovu na wamekaa katika hospitali hii kwa muda mrefu;
- (ii) Kubaini watumishi wa ngazi za chini walioajiriwa ambao hawana sifa zinazotakiwa na wala hawana wito ili wapunguzwe kazini na kuajiriwa wengine wenye sifa na ari kwenye hospitali hiyo;
- (iii) Kuhakikisha kwamba vifaa vya matibabu vinapatikana wakati wote;
- (iv) Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imehakikisha kwamba watumishi wote wanakuwa na vitambulisho; na
- (v) Vikao vya *Clinical Meetings* na *Mortality Meetings* vimeanzishwa ambapo masuala mbalimbali ya magonjwa na tiba ambazo hutolewa kwa wagonjwa pamoja na vifo vilivyotokea vinajadiliwa na Madaktari na Wauguzi mara moja kwa mwezi.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali lifuatalo: Kwa kuwa vifo vilivyotokea ni vingi; na kwa kuwa kwa maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ni watumishi kama 14 tu ndiyo wamechukuliwa hatua; je, Serikali haioni kwamba bado hatujadhibiti kikamilifu uzembe unaofanyika hasa kwenye sehemu inayowahusu akinamama wajawazito ambao wanateseka sana katika hospitali hizi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hakuna jambo ambalo linafanywa dhidi ya mtumishi yeyote bila kuzingatia sheria. Kwa hiyo, haya niliyoyaeleza ndiyo taratibu zilizowekwa na hao waliobainika, ndiyo hao tuliweza kuwachukulia hatua. Kwa hiyo, kwa kadri taratibu hizi zitakavyozidi kuimarika, tuna hakika tutaendelea kudhibiti hali hiyo kwa kiasi kikubwa zaidi.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali ya uzembe na huduma mbaya imeshamiri katika hospitali nyingi, Vituo vya Afya na hata kwenye Zahanati. Je, ni hatua gani za makusudi ambazo zinachukuliwa na Serikali ili kuhakikisha hali hii inatoweka tukizingatia kwamba Wizara ya Afya ni mojawapo ya Wizara ambayo imetia sainsi Mkataba wa huduma bora kwa wateja? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Serikali inaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa kisheria. Kwa hiyo, wazembe wote katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati pote nchini, nao wanashughulikiwa kwa utaratibu huu. Lakini labda nihimiza tu kwamba, kwa kweli *salvation* yetu katika jambo hili ni ile ya kuimarisha Bodi za Afya katika Wilaya zetu ili waweze kukabiliana kwa karibu zaidi na matatizo haya ambayo tunayazungumzia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo kwenye *Gallery* ya Spika leo tuna mgeni Mheshimiwa Severine Mzingumungongo, Waziri wa Uchukuzi kutoka Burundi amefuatana na Balozi wake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Na. 172

### **Msamaha wa Madeni**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

Tangu Tanzania ianze kusamehewa madeni:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha madeni kimesamehewa hadi sasa na kwa mchanganuo gani?
- (b) Je, kuna uhusiano gani kati ya msamaha wa madeni na gawio la bajeti za Wizara ya Elimu na Utamaduni, Afya, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Chakula na Miundombinu ya barabara?
- (c) Je, utaratibu wa kusamehewa madeni unaweza kuendelea mpaka lini na je Serikali ina mpango gani wa kujitegemea pindi misaada itokanayo na misamaha ya madeni itakapokwisha?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango wa *HIPC*, Tanzania imeahidiwa msamaha wa madeni ya jumla ya dola za Kimarekani bilioni tatu, sawa na shilingi trilioni 3,190.77 Msamaha huo wa madeni utatolewa katika kipindi cha miaka 20. Sehemu kubwa ya msamaha huo itatokana na Benki ya Dunia na Nchi Wanachama wa Kundi la Paris (*Paris Club*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi 31 Januari, 2003, Tanzania imepata msamaha wa madeni (*Debt Cancellation*) ya jumla ya shilingi bilioni 5,459,125.89 ambayo ni sawa na dola za Kimarekani milioni 5,132.69 yenye mchanganuo ufuatao:-

- Kwa nchi, *bilateral debt cancellation* ni shilingi bilioni 5,145,363.89 ambayo ni sawasawa na dola za Kimarekani milioni 4,837.69. Kati ya hizo shilingi bilioni 3, 979, 232.85 ambayo ni sawasawa na dola za Kimarekani milioni 3,741.29 zilitoka kundi la nchi za Paris.

- Msamaha toka Taasisi za Fedha za Kimataifa ni shilingi milioni 313, 762.00 ambayo ni sawa na Dola za Kimarekani milioni 295 ambayo inajumuisha:-

(i)	<i>IDA</i>	Sh.	172,156 milioni
(ii)	<i>IMF</i>	Sh.	102, 233.23 milioni
(iii)	<i>ADB/ADF</i>	Sh.	33,729.95 milioni
(iv)	<i>IFAD</i>	Sh.	2,607.95 milioni
(v)	<i>EIB</i>	Sh.	258.45 milioni
(vi)	<i>NORDIC Fund</i>	Sh.	2,776.00 milioni

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, unafuu wa madeni hautuongezei mapato kwa kuwa hakuna mapato ya ziada yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kinachotokea ni kwamba, kutokana na

mapato yanayokusanywa, mgao kwa ajili ya kulipia madeni ya nje unapungua na kiasi kinachookolewa kutoka fungu la kulipa madeni kinaongeza uwezo wa Serikali wa kuongeza gawio la bajeti la Elimu, Afya, Maji, Kilimo na Miundombinu. Huu ndiyo uhusiano kati ya msamaha wa madeni na gawio kwa sekta za kipaumbele.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeshafikia hatua ya mwisho (*Completion Point*) katika mpango wa *HIPC* wa kusamehewa madeni. Kama nilivyosema awali, msamaha wa madeni wa dola za Kimarekani bilioni tatu utatolewa katika kipindi cha miaka 20 kwa kuwa msamaha unatolewa kila deni husika linavyoiva, hasa madeni ya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Aidha, bado tunaendelea kujadiliana na nchi zisizo katika kundi la Paris ili nazo zitupatie msamaha wa mdeni ambayo yanafikia takribani dola za Kimarekani milioni 800. Kwa hiyo, ni vigumu kusema utaratibu huu utaendelea mpaka lini. Serikali inajitahidi kujenga uwezo wake wa kukusanya mapato ya ndani ili kupunguza hatua kwa hatua utegemezi wa misaada ya nje. Sambamba na hili, Serikali inaendelea kuimarisha udhibiti na matumizi bora ya mapato yake na fedha za misaada ili kuleta uwiano wa mapato na matumizi ya Serikali ili tuwe tunatumia tulichonacho.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Nina swali moja la nyongeza. Je, ni kweli limbikizo la madeni ya nje linaongezeka na Serikali inafanya nini kudhibiti kasi hii ya ukuaji wa limbikizo la deni la nje?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kitu tunachoangalia katika deni la Taifa ama nchi kukopa kutoka nje kinatiwa *Debt Sustainability Ratio (DSR)*. Uwezo wetu wa kulipa madeni ndiyo unasababisha ama tunaangalia tukope kiasi gani. Uwezo wetu wa kulipa madeni ya nje sasa hivi unaongezeka kadri ya uchumi wetu unavyoongezeka na tutaendelea kukopa kadri ambavyo uchumi wetu unatuwezesha kutulipa hayo madeni. Kutokana na msamaha wa madeni kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, unatupa nguvu zaidi ya kupata mapato mengi zaidi kutoka katika misamaha hiyo ya madeni, lakini pia kutokana na kuongezeka kwa kukusanya kodi ama mapato ya ndani. Kwa hiyo, tutaendelea kukopa na tutaendelea kuongeza bidii katika kukusanya mapato ya ndani na hatimaye mipango yetu mingi ya maendeleo itafanikiwa kama tunavyopanga.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa *budget deficit* ya Tanzania bado ni takribani asilimia 45, ina maana hatujafikia asilimia 55 ya kujitegemea katika bajeti yetu ya nchi na kwa kuwa asilimia 80 ya uchumi wa nchi bado inategemea kilimo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, mabwawa katika vijiji ambavyo yangeweza kukiinua kilimo yanapata fedha za ziada ili tuweze kukidhi mahitaji ya kuinua uwezo wetu wa kujitegemea kibajeti katika miaka 20 ambayo tuna *relief* ya hizi bilioni tatu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wetu umefaidika sana na uwekezaji uliofanyika hivi karibuni katika sekta ya madini na sekta ya utalii. Kwa hiyo, sekta hizi mbili, madini, pamoja na utalii, zinatupa fedha ama mchango mkubwa zaidi kwenye Pato la Taifa kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Ni kweli kwamba, kilimo kinachangia kiasi kikubwa katika uchumi wetu na ndiyo uti wa mgongo. Lakini *overtime* inabidi tutegemee sekta zingine kama viwanda na biashara na kama ilivyo hivi sasa madini na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ipo ya kilimo cha umwagiliaji na kama mnavyojua kuna *Irrigation Master Plan*, ambayo Wizara ya Kilimo na Chakula tayari imeshaikamilisha na tunaamini kwamba katika bajeti zijazo Wizara ya Kilimo na Chakula, itaendelea kupata fedha nyingi zaidi katika kutekeleza ama kuendeleza kilimo nchini.

Na. 173

#### Ugawaji wa Fedha

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa katika utoaji wa fedha za maendeleo za kila Mkoa hapa nchini kuna ukomo wake ambao hutumika kugawa sawa kulingana na vigezo vilivyowekwa:-

- (a) Je, vigezo vinavyotumika viko vingapi?
- (b) Je, vigezo hivyo hutumiwa na Wizara ya Fedha au Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika ugawaji huo kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali haina vigezo maalum vya kugawa fedha za maendeleo kwenda Serikali za Mitaa. Utaratibu wa sasa wakati wa kugawa fedha za maendeleo kwenda Serikali za Mitaa mambo yafuatayo huzingatiwa:-

- (i) Miradi inayoendelea hupewa kipaumbele katika ugawaji wa fedha za maendeleo ili iweze kukamilishwa;
- (ii) Kuhusu miradi mipya ya maendeleo inayoanzishwa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wafadhili ambayo pia ina masharti ya kuchangia fedha za ndani (*Counterpart Funds*), Serikali huchangia fedha hizo kulingana na makubaliano ya mikataba ya kuanzisha miradi hiyo; na
- (iii) Itakumbukwa kuwa jukumu la kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Serikali za Mitaa ni la Serikali nzima yaani Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Aidha, Serikali Kuu hujaribu kuziba pengo la fedha linapojitokeza Serikali za Mitaa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na vigezo vya kitaalam vya uwazi na vinavyokubalika katika kugawa fedha za bajeti na hivyo kuwa na uwiano utakaokubalika wa maendeleo nchini, Serikali katika mwaka 2003/2004, inaendelea kufanya utafiti wa mfumo utakaotumika kugawa fedha nchini kwa kuwatumia wataalam kutoka ndani na nje ya nchi. Matokeo ya utafiti huu yataiwezesha Serikali kuwa na utaratibu bora wa kugawa fedha za maendeleo na pia fedha za kawaida. Kuhusu mfumo mpya wa kugawa fedha za kawaida kwenda Serikali za mitaa, wataalam wamewasilisha Serikalini ripoti ya awali na mapendekezo yake kuhusu vigezo vitakavyotumika kugawa bajeti ya kawaida ya sekta zinazolenga kupunguza umaskini kama elimu na afya kwenda Serikali za Mitaa. Aidha, zoezi la kuchambua ripoti hiyo, pamoja na vigezo vitakavyotumika, linaendelea kufanywa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Idara ya Menejimenti ya Umma na sekta nyingine za uchumi nchini. Uchambuzi unaoendelea utatoa majukumu ya wadau mbalimbali.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hatukuwa na ratiba au utaratibu maalum huko nyuma na ndiyo maana ukanisababisha mimi niulize swali hilo, kwa kuona kwamba kuna baadhi Mikoa ina idadi ya Wilaya nyingi na ina idadi ya watu wengi. Lakini unakuta wanapewa fedha kidogo sana za maendeleo na baadhi ya Mikoa mingine ambayo ina Wilaya chache na watu wachache inapewa fedha nyingi zaidi. Kwa hiyo, Serikali itakubali kwamba imefanya makosa makubwa sana huko nyuma mpaka mwisho wake sasa hivi tunazidiana maendeleo kwa sababu ya Mikoa mingine kupewa fedha nyingi zaidi wakati wakiwa na Wilaya chache na watu wachache na Mikoa mingine ambayo ina idadi ya Wilaya nyingi na watu wengi wanapewa fedha kidogo kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu maalum? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utaratibu wa sasa unaoendelea na uzoefu wa miaka ya nyuma katika kugawa rasulimali nchini,

Serikali inakiri kuwepo kwa mapungufu ya uwiano wa ugawaji wa fedha za maendeleo nchini. Ni kweli kwamba, kuna baadhi ya Mikoa inapata fedha nyingi za wafadhili ikilinganishwa na Mikoa mingine. Hali hii inaleta uwiano mbaya wa kimaendeleo. Serikali ya Awamu ya Tatu, imedhamiria kuchukua hatua madhubuti kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka ujao wa fedha, inatarajiwa kwamba, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti nilioutaja katika jibu langu la msingi kuhusu mfumo wa ugawaji wa fedha, fedha zitagawiwa kufuatana na vigezo vifuatavyo: Kwanza, tutaangalia idadi ya watu katika Mkoa na Wilaya. Pili, tutaangalia umaskini uliopo katika eneo lile yaani *Poverty Count* kwa kila Mkoa ama Wilaya. Mwisho, kati ya vigezo vingine vitakavyotumika, tutaangalia pia watoto wenye umri wa kwenda shule ni wangapi katika Wilaya hiyo. Kwa hiyo, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu na nimhakikishie pia Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte kwamba, Serikali inaliangalia suala hili na kuanzia mwaka ujao wa fedha, matatizozaliyokuwepo huko nyuma yatarekebishwa na kadri tunavyokwenda, basi tutaweza kuwa na utaratibu mzuri zaidi na wenye uwazi na ambao ni wa haki na usawa zaidi. (*Makofi*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, inawezekana Serikali ikatuletea vigezo hivyo katika Bunge la Aprili, 2004 ambavyo amevisema vitaleta uwiano katika fedha, je, inawezekana kwenye maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, kuna utafiti ambao ulikuwa unaendelea kwa kushirikiana na wataalam kutoka Chuo cha *Andrew Young* huko Marekani na tayari utafiti huo umekamilika. Kinachofanyika sasa ni kufanya matayarisho na hatua za mwisho ili kuanzia bajeti ijayo vigezo hivyo ndiyo vitatumika. Kwa hiyo, kusema kwamba tutavileta hivyo vigezo katika Bunge lijalo la Aprili, 2004, itakuwa ni kupakua chakula kabla hakijaiva. Naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira bajeti ijayo vigezo hivyo vitatumika.

Na. 174

### Wasichana Wanaopata Mimba Shuleni

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inathamini na kutoa kipaumbele katika kuboresha elimu yetu nchini kwa kuangalia wanafunzi wa jinsia zote kwamba wanapatiwa elimu ipasavyo:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya watoto wa kike ambao hupata mimba wakiwa shuleni?
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaruhusu wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni, waendeleo na masomo yao baada ya kujifungua?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali inathamini na inalenga katika kutoa elimu iliyo bora kwa wanafunzi wa jinsia zote. Lakini katika kufanya hivyo, Serikali hutakiwa pia izingatie na iendeshe shule kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 iliyotungwa na Bunge hili, ambayo katika kifungu 60(0) inamtaka Waziri anayesimamia mambo ya elimu, atunge Kanuni ya Elimu inayotamka makosa ambayo mwanafunzi bila kujali kama ni msichana au mvulana, akiyafanya kosa atafukuzwa shule. Katika kutekeleza kifungu hicho, Waziri ametunga kanuni iitwayo "*The Education (Expulsion and Exclusion of pupils from schools) Regulations, 2002*", ambayo imeyatamka makosa hayo yakiwemo makosa ya umalaya, utumiaji madawa ya kulevya na makosa yanayopingana na maadili mema (*Ofence Against Morality*), hata kama mwanafunzi husika hakushtakiwa

Mahakamani. Aidha, mwanafunzi atafukuzwa shule kama atajiingiza katika ndoa bila kujali kama ni mvulana au msichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mtoto wa kike anayekuwa na mimba shuleni huwa ni ushahidi wa wazi wa mojawapo ya makosa ya kufukuzwa shule ya ama umalaya (*prostitution*), maadili yasiyo mema (*Imoral Behavior*) au kuolewa akiwa mwanafunzi (*a pupil has entered into wedlock*). Kwa hiyo, mwanafunzi huyo anafukuzwa shule bila kuchelewa.

(b) Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2003, jumla ya wanafunzi 41,554 sawa na asilimia 0.64 ya wanafunzi wote wa Shule za Msingi wakiwemo wasichana 19,394 sawa na asilimia 0.30 ya wanafunzi wote walikatisha masomo kwa sababu mbalimbali. Kati yao waliokatisha shule kwa sababu ya kuwa na mimba walikuwa 2,227 sawa na asilimia 0.07 ya wanafunzi wote wasichana wa mwaka huo.

Kwa hiyo, hao wote 2,227 waliofukuzwa shule kwa ajili ya kuwa na mimba ni asilimia 5.4 ya wote 41,554 waliokatisha shule kwa sababu mbalimbali. Kutokana na takwimu hizi Serikali haioni umuhimu wa kuwaruhusu wasichana waliopata mimba waendelea na masomo yao baada ya kujifungua, hasa kwa kuzingatia pia wajibu wao mpya wa kuwalea watoto waliojifungua.

Lakini Serikali hivi karibuni kwa kutekeleza kifungu 35.3 cha Sheria ya Elimu, imetunga kanuni mpya iitwayo "*The Education (Imposition of Penalties to persons who marry or impregnate a school girl) Rules 2003*" yaani kanuni ya kuwapa adhabu wale wanaowapa mimba watoto wa shule inayotoa adhabu ya kifungu cha miaka mitatu bila faini kwa mwanamume yeyote anayempa mimba mtoto wa shule. (*Makofi*)

Kanuni hii imetungwa na imeanza kutumika tarehe 1 Agosti, 2003. Wizara yangu imetoa maelekezo kwa Maaifisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kwa njia ya Waraka wa Elimu, waanze kuwachukulia hatua wote waliowapa mimba watoto wa shule kuanzia tarehe 1 Agosti, 2003 nilipotunga kanuni hii ili wafunguliwe mashtaka na ni matumaini yangu kuwa Mahakimu hawatasita kuwatupa gerezani kwa miaka mitatu.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, haoni kama hii Sheria ya mwaka 1978 inambana tu mwanafunzi na walimu wengi ambao wanawapa mimba wanafunzi wao hawachukuliwi hatua na bado wanaendelea sana kuhamishwa kutoka shule moja kwenda nyingine?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani naye kwamba, sheria inambana mwanafunzi tu peke yake na haimbani mwalimu aliyehusika. Kwa mwalimu kumpa mimba mwanafunzi ni kosa pia la kimaadili. Kwa hiyo, akipatwa na hatia sasa atakutwa na mambo yote mawili. Kwa hii kanuni mpya maana yake anaweza akafungwa miaka mitatu, lakini pia anafukuzwa kazi pamoja na ualimu. Yaani anafukuzwa kazi na hataruhusiwa kufanya tena kazi ya ualimu.

Kwa hiyo, naamini bado pana adhabu kali kwa walimu. (*Makofi*)

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kazi wanayoifanya ya kutunga sheria kuwasaidia hawa vijana wanaopata mimba shuleni. Je, Waziri anajua kwamba, kuna Sheria za Elimu ambazo zimetungwa mpaka sasa hivi hazifanyi kazi, Sheria Na. 20 ya Mitihani, mtu akifanya kosa afungwe, hawafungwi na mitihani inaibwa na watoto shuleni wanabakwa, anajua kwamba walimu wake wanawabaka watoto shuleni katika maofisi yao? (*Makofi*)



**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba, zipo kanuni ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Elimu pamoja na hiyo aliyoitaja, ambazo zipo katika maandishi lakini hazijatumika ipasavyo. Panaonekana katika taratibu zetu za kusimamia elimu, bado tumekuwa na pengo kubwa kati ya sheria na kanuni zinavyosema na utekelezaji (*enforcement*) ya kanuni hizo. Ndiyo maana katika kujibu swali hili katika jibu langu la msingi nimetoa wito kwa Mahakimu kwamba, wasisite kuwachukulia hatua na kuwapa adhabu hizi hizi za kifungo. Mimi mwenyewe katika Wizara tunachukua hatua baada ya kutunga kanuni tunafuatilia kwa kutoa Waraka wa Elimu kutoka kwa Afisa Elimu Kiongozi kwenda kwa Maafisa Elimu wa Wilaya ili tuweze kuwabana kwa sababu wao pia ni sehemu ya wale wanaotakiwa kuchukua hatua ili wale wanaofanya makosa kwa kuvunja kanuni hizi waweze kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane katika *enforcement* ya kanuni hizi. Katika mikutano yetu tuwaeleweshe watendaji pamoja na wananchi juu ya umuhimu wa kufuata kanuni hizi ambazo zimetungwa chini ya Sheria ya Elimu.

Na. 175

### **Ujenzi wa Shule za Sekondari**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI (k.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni imekamilisha majengo mengi ya Shule za Msingi kupitia mpango wake wa MEM na kwa kuunganisha nguvu za wananchi; na kwa kuwa madarasa mengi yamejengwa na kwa sasa wananchi wamejenga madarasa ya Sekondari; je, ni lini Serikali itaunga mkono nguvu za wananchi wanaojenga Shule za Sekondari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuwapongeza wananchi wa Wilaya ya Nzega, kwa kukusanya nguvu zao kujenga majengo ya Shule za Msingi na pia kuanza kujenga jumla ya Shule za Sekondari za kutwa tano, ambazo kwa taarifa tulizonazo, nne zimekwishafunguliwa na moja iko katika hatua ya kukamilishwa. Pamoja na mafanikio hayo iko haja ya kukamilisha ujenzi wa majengo ya Shule za Msingi sio katika Wilaya ya Nzega tu bali katika Wilaya zote nchini, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu. Mpaka hapo lengo la MEM la kuwa na mkao sahihi wa ulishaji elimu madarasani wa wanafunzi wasiozidi 40 darasani wenye mwalimu mwenye nyumba pale shuleni litakapofikishwa kwa uhakika katika kila shule na katika kila Wilaya.

Serikali kupitia Wizara yangu imekamilisha Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 - 2009 ambao hivi sasa unafanyiwa tathmini (*appraisal*) na Benki ya Dunia na pia unafanyiwa majadiliano (*negotiation*) kwa ajili ya mkopo wa Benki ya Dunia wa *USD150* milioni. Aidha, huko mbele *Basic Education Development Committee (BEDC)*, ambayo ni Kamati ya ushirikiano wa Serikali, wadau, wahisani na wabia wetu wa maendeleo ya elimu kwa ajili ya kupitishwa na kupangiwa vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni pamoja na Serikali kuweza kutoa ruzuku ya maendeleo ya Sh. 7,000,000 kwa kila darasa na Sh. 9,000,000 kwa kila nyumba ya mwalimu kwa wananchi wanaojenga Sekondari kwa lengo la kufikia kutoa Elimu ya Sekondari kwa asilimia 50 ya watoto wote wa rika la Elimu ya Sekondari ya kawaida ambalo ni la umri wa miaka 14 hadi 17 na asilimia 25 kwa rika la Elimu ya Sekondari ya Juu ambalo ni la umri wa miaka 18 hadi 19. Inatarajiwa mpango huu (MMES), utakuwa sehemu muhimu ya Bajeti ya Serikali kuanzia bajeti ya mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza, kwa niaba ya watu wa Nzega, napokea pongezi nilizopewa. Lakini naomba niulize maswali mawili madogo

sana. Pamoja na Wilaya ya Nzega kuwa na shule chache sana za Sekondari, lakini zilizopo hazina walimu au ikama ya walimu haijatosha. Je, ni lini Wizara ya Elimu na Utamaduni itakamilisha ikama ya walimu katika shule hizo hasa ya Nzega Mjini na Itobo?

Pili, Shule ya Sekondari ya Itobo mpaka sasa haina hata *Headmaster*, Waziri anaweza kutuahidi atatupelekea lini *Headmaster*? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa walimu katika Sekondari zilizoko katika Wilaya ya Nzega kwamba ikama haitoshelezi, napenda nikiri kwamba, hali hiyo ni kweli iko hivyo na iko hivyo pia katika shule nyingi za Sekondari hususan zilizojengwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kumkumbusha Mheshimiwa Stephen Kahumbi na Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika *Supplementary Estimate* yaani haya makisio ya ziada yaliyopitishwa na Bunge hili siku chache zilizopita, Wizara yangu imepewa Sh. .2.424 bilioni, lengo la fedha hizo ni kutuwezesha kuajiri walimu. Tunatarajia kuajiri walimu wa namna tatu. Namna ya kwanza ni walimu ambao tayari wana vyeti vya *Diploma* na ambao wenye Shahada za Chuo Kikuu. Lakini tunafahamu kwamba, hawa wanaweza wasitosheleze kujaza mapengo yote kwa sababu wengine bado wako katika maandalizi. Kwa hiyo, namna ya pili, tutawachukua vijana waliohitimu na kufaulu vizuri Kidato cha Sita na hawa watapewa mafunzo ya Pedagogia (*Pedagogy*) yaani mbinu za kufundisha, wakafundishe yale masomo ambayo wao wenyewe wamefaulu ya muda mfupi. Kundi la tatu watakuwa ni wale ambao wana Shahada za Chuo Kikuu zisizo za elimu.

Tunafahamu hivi sasa hapa nchini kuna wengine wamemaliza digrii za *Engineering*, wengine za masomo mengine mbalimbali sio walimu, lakini hawajapata kazi. Tutatangaza magazetini waombe kazi za ualimu na watapewa mafunzo ya pedagogia pamoja na wale wa Kidato cha Sita na baada ya hapo watapewa leseni za kuwa walimu na huku tukiwa na programu ya kuwapa mafunzo ya ualimu wakiwa kazini. Kwa hiyo, napenda kulishukuru sana Bunge hili kwa kutupa hizo fedha katika *Supplementary Estimates* na tunategemea kujaza mapengo yaliyopo.

Kuhusu swali la pili la Sekondari ya Itobo, nafahamu kwamba, pale hatujateua *Headmaster* kutokana na katika matatizo hayo hayo yaliyokuwepo. Katika siku za hivi karibuni tutafanya kila juhudi na fedha tulizopewa na Bunge hili kujaza mapengo yaliyopo ya walimu pamoja na Wakuu wa Shule. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika *millennium development goals* imesisitiza kabisa kwamba kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa watoto wa kike na hasa ukizingatia pia tumekuwa tukiridhia Itifaki mbalimbali za haki sawa kwa wanaume na wanawake; na kwa kuwa mpango wa MMES umezingatia tu suala la madarasa na nyumba za walimu na kusahau kipengele muhimu sana cha mabweni ya watoto wa kike kuwaepusha na upatikanaji wa mimba bila ya kuwa na utaratibu rasmi; Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani la kuingiza suala zima la mpango wa mabweni katika Shule za Sekondari ili kuwaokoa watoto wao wa kike? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika *millennium development goals*, suala la kutoa elimu kwa usawa kwa wavulana na wasichana ni mojawapo ya malengo yaliyomo humo. Lakini kama Mheshimiwa Rais alivyotutaarifu katika Hotuba yake kwa Bunge hili tarehe 12 Februari, 2004, Tanzania tayari tumekwifafikia lengo hilo la kutoa elimu kwa usawa kwa wavulana na wasichana katika ngazi ya Elimu ya Msingi. (*Makofi*)

Msichana katika jumla ya wanafunzi wa Elimu ya Msingi sasa hivi wako asilimia 49 na *point* juu. Lakini katika wanafunzi wanaofanya mtihani wa darasa la saba kwa miaka miwili mfululizo sasa wasichana ni wengi kuliko wavulana. Kwa hiyo, kwa kweli tumekwishatimiza lengo hilo. (*Makofi*)

Kuhusu ngazi ya Elimu ya Sekondari, jitihada kubwa inafanywa tunapofanya *selection* ya wanafunzi katika ngazi ya Sekondari tunawachukua kwa usawa wavulana na wasichana kuingia Kidato cha

Kwanza. Kasoro kubwa inakuja kutokea kwenye Kidato cha Tano. Kwa sababu pale kwenda Kidato cha Tano ni suala la kufaulu mtihani wa Kidato cha Nne vizuri na hapo inatokea tofauti kubwa kwa sababu bado tuna matatizo wasichana hawafaulu kama wavulana. Inawezekana pia inatokana na alichokieleza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba, wasichana katika shule za kutwa wanapambana na matatizo mengi. Napenda kumhakikishia kwamba katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari, moja ya vitu vitakavyopewa fedha ni ujenzi wa hosteli kwa ajili ya wasichana. (*Makofi*)

Na. 176

### **Uandikishaji wa Vijana Kwenye Jeshi la Polisi Zanzibar**

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika zoezi la uandikishaji wa vijana kujiunga na Jeshi la Polisi mwishoni mwa mwaka 2002 huko Zanzibar walitakiwa vijana wenye sifa maalum na wale tu waliomaliza shule kuanzia mwaka 1999 na kuendelea; na kwa kuwa vijana waliokuwa na sifa zilizotakiwa lakini waliomaliza shule mwaka 1998 na kurudi nyuma waliokuwapo hawakuchaguliwa:-

- (a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu za hali hiyo?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba vijana hao walioachwa licha ya kuwa na sifa zilizotakiwa wamekoseshwa haki zao za ajira kama Watanzania?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mbunge wa Mikunguni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa katika zoezi la kuandikisha vijana wa kujiunga na Jeshi la Polisi Tanzania Zanzibar na Bara mwishoni mwa 2002, walitakiwa vijana wenye sifa maalum ambazo zilitangazwa kwenye vyombo vya habari na walitakiwa ni wale tu waliomaliza shule kuanzia mwaka 1999 mpaka 2002 na kuwaacha wale waliomaliza kabla ya mwaka 1999. Kufanya hivyo kulitokana na sababu zifuatazo:-

(i) Kwa kuchukua vijana waliomaliza masomo kati ya mwaka 1999 na 2002 kulitoa nafasi kubwa ya kuwapata vijana wenye umri kati ya miaka 18 na 25, umri uliotakiwa katika ajira hiyo; na

(ii) Kwa kuwa vijana wanaomaliza shule na kukosa ajira kila mwaka ni wengi sana, kama tusingeweka muda huo maalum wa kumaliza masomo, idadi ya waombaji ingekuwa kubwa sana na ingefanya zoezi la usaili kuwa gumu na lingechukua muda mrefu zaidi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kuwaacha vijana waliomaliza masomo ya Sekondari kabla ya 1999, yaani walio na umri wa zaidi ya miaka 25, haikuwanyima vijana hao haki ya kuajiriwa katika Idara zingine za Serikali au katika sekta binafsi. Pengine ingefaa Mheshimiwa Mbunge, akaelewa vile vile kwamba, kwa sababu ya uchache wa nafasi, hata miongoni mwa vijana waliomaliza masomo mwaka 1999 na baadaye wapo wengi walioachwa.

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali la nyongeza.

Hizi nafasi za uajiri za Polisi zinagawiwa baina ya Zanzibar na Bara ambazo ziko nafasi chache na kuna kero kubwa au tuhuma nyingi kule Zanzibar kwamba watoto wanaochukuliwa kule dakika za mwisho baadhi yao huenguliwa na baadhi kya wakubwa wa Polisi wanaleta jamaa zao kutoka huku kwenda kule wanajiingiza katika nafasi zile za Zanzibar; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kusema nini juu ya tuhuma hiyo au kero hiyo kwa wananchi wa Zanzibar?

Pili, je, kutokana na tuhuma hizi anaweza kukubaliana nami kwamba aunde chombo kidogo tu cha muda ambacho kikijumuisha baadhi ya wananchi, Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi na watawala kule ili kuratibu hawa wanaochukuliwa kutoka Zanzibar ni hakika wale ambao wanaotakiwa? Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli nafasi zinapopatikana hugawiwa kimkoa kote Tanzania Bara na Zanzibar ambapo kila mkoa unatengewa nafasi zake.

Sina taarifa kama kuna nafasi za Mikoa baadaye zinachukuliwa na Maofisa wa Polisi kinyume cha utaratibu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama anao ushahidi huo anipatie. Lakini pia nitoe wito kwa Wabunge na viongozi wenzangu popote walipo na wananchi kama wakigundua kitu kama hicho watuarifu kwa wakati muafaka ili tuweze kusahihisha kabla mambo hayajaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile utaratibu uliopo ni mzuri tu wa kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama za ngazi mbalimbali toka Vijijini, Wilaya mpaka Mkoani, ambamo wanashiriki viongozi wa aina mbalimbali, nadhani vyombo hivyo vinatosha na hatuna haja ya kuunda chombo kingine. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa hivi sasa elimu imepanuka na kuna mambo mengi wanafunzi wanahitajika kusoma. Mfano mtu anapomaliza Kidato cha Sita inatakiwa asome kompyuta na mambo mengine. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hivi sasa umri wa miaka 18 mpaka 24 ni mdogo ili wananchi au watoto wa askari waweze kupata elimu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umri uliowekwa wa sasa hivi wa miaka 18 hadi 25 unazingatia zaidi *nature* ya kazi yenyewe ya Polisi ambapo hasa katika ngazi za chini nadhani huwa tunaeleza mara nyingi tunahitaji vijana ambao wana nguvu katika utendaji wa kazi.

Si busara katika ngazi hizi kuanza kuchukua vijana ambao wameshaanza kuingia utu uzima kiasi ambacho itaathiri na utendaji wa kazi za Polisi. Hata kwa kuzingatia hayo bado wale ambao wanajifunza zaidi wanaofikia Kidato cha Sita, Chuo Kikuu, wanaajiriwa katika umri wowote wanaokuwepo kwa matarajio kwamba, wanapoajiriwa hawachukui muda mrefu wanakuwa maofisa na maofisa wanaruhusiwa kuwa katika umri mkubwa zaidi.

Na. 177

### **Matukio Yanayohatarisha Usalama wa Raia na Mali Zao**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na mwenendo wa muda mrefu sasa wa matukio mengi ya uporaji wa mali za raia, unyang'anyi na mauaji kwa silaha; na kwa kuwa hali hiyo inakwenda sambamba na matukio ya baadhi ya majengo ya umma kuungua moto likiwemo jengo la Wizara ya Nishati na Madini, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Bima na nyumba kadhaa za raia:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahakikishia raia wake usalama wao na mali zao dhidi ya ujambazi unaotokea mara kwa mara usiku na mchana?

(b) Kutokana na ukosefu wa mitambo mahsusi ya kisasa ya kupambana na ajali za moto ambazo huteketeza majengo ya umma na ya raia, je, kwa sasa Serikali inaweka mikakati gani ya kukabiliana na ajali za moto zinapotokea?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti matumizi mabaya ya silaha zinazotumika katika uvamizi na ujambazi dhidi ya raia wema wa nchi yetu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, yapo matukio mengi katika baadhi ya Mikoa ya uporaji wa mali za raia pamoja na unyang'anyi na mauaji ya kutumia silaha. Katika kuwahakikishia raia usalama wao na mali zao dhidi ya ujambazi, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, inapambana na tatizo hili kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuimarisha doria mijini na vijijini, hasa katika maeneo yenye matukio ya uhalifu wa mara kwa mara, ushiriki wa vikundi vya Sungusungu katika doria zinazohusu maeneo yao ni muhimu sana;

(ii) Kuimarisha doria katika maeneo yenye harakati nyingi za Kibiashara na mzunguko mkubwa wa fedha. Hapa huwa tunaomba ushirikiano wa karibu kutoka kwa raia wema na waajiri, hasa umuhimu wa kuomba *escort* ya Polisi wanapopeleka au kutoa fedha Benki;

(iii) Kukusanya taarifa za kiintelijensia zinazohusu majambazi na kuzifanyia kazi kwa ukamilifu;

(iv) Kufanya misako dhidi ya wahalifu kufuatana na taarifa za kiitelejenzia zinavyokusanywa vituoni pamoja na zile zinazotolewa na raia wema.

(v) Kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari au kwa Viongozi wa Serikali/Vyama vya Siasa katika ngazi za mitaa, Vijiji, Wilaya na kadhalika ili waunde vikundi imara vya ulinzi wa jadi na kutoa taarifa za kuwafichua wahalifu kwa nia ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao; na

(vi) Wizara inaandaa utaratibu utakaowawezesha wananchi kushirikiana na vyombo vya ulinzi kwa karibu zaidi katika kulinda maeneo yao, yaani utaratibu wa "Polisi Jamii".

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na ajali za moto, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya ukaguzi na kuhakikisha kuwa vifaa vya kuzimia moto vinakuwepo kwenye maeneo na majengo mbalimbali;

(ii) Kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuwa na vifaa vya kuzima moto na namna ya kutumia vifaa hivyo;

(iii) Kuhimiza kuwa kila eneo la Wizara za Serikali, viwanda, majengo marefu, mashule na vyuo, pamoja na maeneo yote hatari kwa moto, kunakuwa na visima virefu vya maji ya akiba ili kutumiwa na wazima moto endapo janga litatokea;

(iv) Kuhimiza kuwa kila sehemu yenye hatari ya kutokea moto kunakuwa na ving'amuzi moto (*Alarm and Fire Detection Systems*) na njia za dharura kwenye maghorofa marefu au nyumba yenye mikusanyiko ya watu; na

(v) Kuimarisha vikosi vya zimamoto vya Halmashauri za Manispaa, Jiji na Miji, kwa kuongeza zana za kuzimia moto na mafunzo kwa Askari wa Zimamoto.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti matumizi mabaya ya silaha zinzotumika katika uvamizi na ujambazi dhidi ya raia wema wa nchi yetu, Serikali inayo mipango ifuatavyo:-

(i) Kufanya misako ya mara kwa mara na kuwakamata watu wanaotengengeza silaha kienyeji, kuzimiliki au kuziua kinyume cha sheria na kuwachukulia hatua za Kisheria;

- (ii) Kufanya ukaguzi wa kushtukiza kadri taarifa za kiitelijensia zinavyopatikana dhidi ya watu wanaomiliki silaha kihalali lakini wanaziazimisha kwa wahalifu;
- (iii) Kuwataka wanaomiliki silaha kinyume cha sheria wazisalimisha kwenye Vituo vya Polisi; na
- (iv) Kuwaomba wananchi/raia wema kuwafichua watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria au wanaoazimisha silaha hizo kwa wahalifu ili Serikali ichukue hatua za kisheria dhidi yao kabla silaha hizo hazijaleta madhara kwa wananchi na mali zao. (*Makofi*)

**MHE. JOHN E. SINGO:** Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya katika kupambana na majambazi pamoja na ajali za moto.

Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kumlinda raia na mali yake. Je, Serikali imewahi kufidia raia wangapi walioporwa mali zao na majambazi?

La pili, kwa kuwa Halmashauri zetu hazina uwezo wa kuweza kununua vifaa vya kupambana na ajali za moto. Je, Serikali kwa makusudi ina mpango gani kuziwezesha Halmashauri kuwa na uwezo wa kununua vifaa vya kupambana na ajali za moto?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba Mheshimiwa John Singo, akubaliane nami kwamba, hiyo takwimu aliyoitaka si rahisi kuipata kwa mara moja, itahitaji utafiti. Kwa hiyo, ningemshauri atuletee hilo swali kwa njia za kawaida ili tupate muda wa kulitafiti.

Pili, kuhusu suala la Halmashauri kusaidiwa vifaa vya moto, utaratibu huu upo, pale ambapo Serikali inakuwa na uwezo kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam na hata Jiji la Mwanza, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kununulia magari ya moto kwa kuzingatia wingi wa matukio ya moto katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unaongezeka, tutaweza pia kufikiria na Halmashauri nyingine. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Kikosi cha Zimamoto kiko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na ilifanyika hivyo kusudi ili kuimarisha vikosi hivi. Je, Askari wa Zimamoto maslahi yao yanalingana kiasi gani na Askari wengine wa Polisi ili kuona kwamba na wao wanatoa huduma muhimu katika nchi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimfahamishe Mheshimiwa Missanga na Bunge lako Tukufu kwa ujumla kwamba, Kikosi cha Zimamoto kilichopo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni cha kuratibu shughuli za Vikosi vya Zimamoto ambavyo viko kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la Zimamoto sasa hivi ni *decentralized*, Halmashauri zina vikosi vyao na Viwanja vya Ndege vina vikosi vyao ambavyo havina mahusiano ya kiutawala na kikosi kilichopo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na tumegundua kasoro katika jambo hili. Kwa hiyo, hivi sasa tupo katika kuitazama upya Sera nzima ya Zimamoto na Uokoaji ili kuwa na utaratibu ambao utaweza kukidhi hayo maombi aliyoyaelezea Mheshimiwa Mohamed Missanga, kwa njia ya swali, ambayo hivi sasa ni kweli hayapo.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba, Jeshi la Polisi lililokuwepo miaka 60 iliyopita Askari walikuwa wakienda kwa miguu, chini wanafunga pasisi na wakienda kukamata wahalifu walikuwa wanapanda punda. Je, haoni kwamba sasa ni wakati muafaka wa

kufunga vyombo maalum ndani ya Miji, mahali ambapo uhalifu unapatikana sana ili Makachero kwenye vyumba vya siri waweze kuwaona wahalifu hao au angalau baada ya kufanya uhalifu huo wakaweza kuwatambua? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, upo umuhimu wa kuwa na vifaa vya upelelezi katika maeneo maalum, kwenye sehemu ambazo zinajulikana kwamba zina uhalifu mkubwa. Wazo hilo tunalo na tunalifanyia kazi na upo mpango madhubuti wa kuanza kuweka vifaa hivyo hivi karibuni tu, lakini hatutataja maeneo ambayo vitakuwepo. *(Makofi)*

Na. 178

### **Simu Wilaya ya Bukombe**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza: -

Kwa kuwa mawasiliano ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya nchi na kwa kuwa wakulima wanahitaji kuwasiliana ili kuwa na uhakika wa kupata soko la mazao yao na kwa kuwa Serikali ilikuwa imeahidi kupeleka huduma ya simu katika Wilaya ya Bukombe mwaka 2003:-

- (a) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia kiwango gani?
- (b) Je, nini maelezo ya Serikali kuhusu kupeleka simu Makao Makuu ya Wilaya zote ambazo hazina huduma hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ilishafanyika katika Mpango wa Maendeleo wa *TTCL* wa mwaka 2003 na kuonekana umuhimu wa kupeleka simu za kisasa aina ya *digital* katika Wilaya ya Bukombe ili kukidhi matakwa ya wakulima kuwa na mawasiliano ya uhakika na ili kufanikisha shughuli zao za kibiashara kama vile wachimbaji wadogo wadogo wa madini, biashara ya mahindi na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania inatambua kuwa kukosekana kwa mawasiliano ya simu ya uhakika katika baadhi ya Wilaya nchini, kunaathiri juhudi za Serikali za kupeleka maendeleo karibu na Wananchi kupitia Halmashauri zao. Hii ndiyo sababu ya kubuni mpango wa kuboresha huduma za mawasiliano ya simu katika Makao Makuu ya Wilaya nchini kote pamoja na kuondoa simu zote za kukoroga.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kampuni ya *TTCL* sasa imekalia mgogoro badala ya kufanya kazi na mgogoro huu ukiachwa uendeleo unakwamisha utekelezaji wa azma ya Serikali ya kupeleka simu Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini. Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha mgogoro huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, mgogoro huu sasa umekwisha kwa sababu tayari limeshatolewa agizo rasmi kwamba, walipwe Shilingi milioni tano kwa mujibu wa mahesabu yalivyofanywa. Ninaamini sasa tutaendelea kufanya kazi ya kuendeleza simu vijijini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mashala kwamba, wakati tukiendelea na mgogoro shughuli za mawasiliano na simu hazikusita. Huduma za *CelTel*, *Mobitel* na *Vodacom*, zilikuwa zinaendelea kama walivyokuwa wamepanga. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa simu hizi za kisasa za *Wireless Local Loop* zinatumia zaidi umeme kama hakuna umeme kwa kweli mawasiliano hakuna kabisa, hata kama ni wiki nzima na Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kutuambia hapa Bungeni kwamba, atazungumza na watu wa *TTCL* ili waweke betri ya akiba na mawasiliano yaendele. Je, mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mitambo ya *Wireless Local Loop* inahitaji umeme na zile simu zetu ni lazima ziwe na betri ya ziada. Kote tulikoweka shughuli hizi za *Wireless Local Loop*, tumetoa betri kwa ajili ya shughuli hii, lakini ufumbuzi wa tatizo hili ni kupata umeme katika maeneo husika. Nina hakika wanaohusika na suala hili la umeme wanalitilia maanani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa maelezo ya nyongeza kwa yale majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu swali la msingi la Mheshimiwa Mashala kama ifuatavyo: Napenda kutoa taarifa kwamba, Bukombe itapata huduma za *Celstel* mwisho wa mwezi Machi. Kwa maana hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Robert Mashala, kwa kusukuma sana jambo hili la mawasiliano Bukombe. Pia, napenda kutoa taarifa kwamba, uzinduzi wa huduma za *Celstel* Kondo utafanyika tarehe 1 Machi, 2004. Uzinduzi wa huduma za *Celstel* Mbulu utafanyika tarehe 4 Machi, 2004, vile vile tutafanya uzinduzi Qatesh na Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa *Captain* Theodos Kasapira kwamba, Mahenge nayo itapata huduma za mawasiliano ya *Celstel*. Ingawa tumechelewa kidogo, lakini si baada ya Septemba, yaani ni kabla ya mwezi Septemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaatifu Bunge lako Tukufu kwamba, *Celstel* ina mpango wa kufikisha huduma za simu Wilaya zote Tanzania ifikapo 2005. *(Makofi)*

Na. 179

### **Huduma ya Simu Mji wa Mhunze**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza: -

Kwa kuwa Mji wa Mhunze ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu lakini hauna mawasiliano ya simu, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya simu katika Mji huo ili kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya hiyo na sehemu nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ng'wala Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu Tanzania, ilifanya utafiti wa soko la biashara ya simu katika baadhi ya maeneo mbalimbali nchini na inapanga kufanya utafiti katika Mji wa Mhunze. Matokeo ya utafiti huo ndiyo yatakayodhihirisha uwezekano wa Mji huo kuingizwa kwenye mpango wao wa maendeleo ya Kampuni. Kwa upande wa simu za mkononi, napenda nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Kampuni ya simu ya *Celstel* imeshafanya tathmini ya awali ya soko katika Wilaya ya Kishapu mwaka 2003. Tathmini ya kiufundi itafanyika Februari, 2004 matokeo yake ndiyo yatakayotumika katika kufikia uamuzi wa kujenga mnara katika Kijiji cha Mhunze. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Kishapu, waendeleo kuvuta subira.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Serikali imevuna ilichopanda katika *TTCL* na kwa kuwa ili katika Shule za Sekondari kuweza kuwa na *computer* na *internet* ni lazima kuwe na simu za *landline*, siyo *Celstel*. Je, kwa kuwa sasa *TTCL* haina tena hela za kupeleka *landline* kwenye maeneo kama Kyerwa na kwingine, kuna Kampuni nyingine ambayo Serikali inafikiria itairuhusu ili iweze kupeleka simu hizo? *(Makofi)*



**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwamba, muda wa *selectivity* wa miaka minne ukimalizika, *TTCL* haiongezewi tena muda. Kwa maana hiyo, simu nyingine za kutoa *basics* zitaanza kupewa nafasi hiyo na nina hakika huduma hiyo itafika kwa Mheshimiwa Mbunge.

Na. 180

#### **Kilimo cha Umwagiliaji kwa Maji ya Ziwa Victoria**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, alikwishazungumzia swala hili, kwa heshima naomba kuliondoa.

**NAIBU SPIKA:** Unasemaje?

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naliondoa swali langu.

**NAIBU SPIKA:** Sawa.

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali)*

Na. 181

#### **Uzalishaji wa Sukari Nchini**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA (k.n.y. MHE. JOHN L. MWAKIPESILE)** aliuliza: -

Kwa kuwa sukari inayozalishwa na viwanda vyetu vya Kilombero, Mtibwa, *TPC* na Kagera ni haba na adimu kwa baadhi ya maeneo hapa nchini kama vile Mikoa ya Kusini na Kusini Magharibi na kutokana na ukweli huo kwamba katika Mkoa wa Mbeya sukari inayozalishwa na viwanda hivyo haijaonekana katika soko kwa zaidi ya miaka kumi (10) sasa.

Je, baada ya kurekebisha na kubinafsisha viwanda vyetu, uzalishaji wa sukari umefikia kiwango gani kabla na baada ya ubinafsishaji kiasi cha kufanya baadhi ya maeneo ya nchi kukosa bidhaa hiyo kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo: -

- (i) Kampuni ya Sukari ya Kilombero ilibinafsishwa mwaka wa 1998/99 na mwaka huo ilizalisha tani 42,063 za sukari. Msimu huu wa 2003/2004, kampuni hiyo imezalisha tani 126,743, hivyo uzalishaji umeongezeka kwa asilimia 68.8 ikilinganishwa na uzalishaji kabla ya kubinafsishwa.
- (ii) Kampuni ya Sukari ya *Tanganyika Planting Company (TPC)* ya Moshi ilibinafsishwa mwaka wa 1999/2000. Mwaka huo Kampuni hiyo ilizalisha tani 34,584 za sukari. Msimu huu wa 2003/2004, Kampuni hiyo itazalisha tani 62,000, hivyo uzalishaji utakuwa umeongezeka kwa asilimia 44.2 ikilinganishwa na uzalishaji kabla ya kubinafsishwa. Hadi kufikia mwanzoni mwa Januari, 2004, Kampuni hiyo ilikuwa imezalisha tani 50,177 za sukari.
- (iii) Kampuni ya Sukari ya Mtibwa Morogoro, ilibinafsishwa mwaka wa 1999/2000 na uzalishaji wa sukari mwaka huo ulikuwa tani 32,110. Katika msimu wa 2003/2004,

uzalishaji wa sukari utafikia tani 40,000. Uzalishaji utaongezeka kwa asilimia 19.7 ikilinganishwa na uzalishaji kabla ya ubinafsishaji.

- (iv) Kiwanda cha Sukari cha Kagera kilichobinafsishwa mwaka 2001/2002, kinatarajiwa kuanza uzalishaji msimu wa 2004/2005 kwa kuzalisha tani 30,000.

Uwekezaji katika viwanda vya sukari baada ya ubinafsishaji umewezesha uzalishaji wa sukari nchini kuongezeka kutoka tani 108,753 mwaka wa 1998 hadi kufikia tani 228,743 katika msimu wa 2003/2004. Hili ni ongezeko la asilimia 52.5. Napenda kuchukua nafasi hii kuyapongeza Makampuni yanayohusika kwa utendaji mzuri na wa kuridhisha sana.

Matumizi ya sukari nchini ni tani 310,000 kwa mwaka. Kati ya tani hizo, wastani wa tani 65,000 hutumika viwandani na tani 245,000 hutumika kwa matumizi ya kawaida ya majumbani. Hivyo, upatikanaji wa sukari nchini wa tani 228,743 utatosheleza mahitaji ya sukari inayotumika kwa matumizi ya kawaida kwa asilimia 93.4. Upungufu wa sukari ya matumizi ya kawaida ni tani 17,000 sawa na asilimia saba. Kiasi hicho kinahitajika kuagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa sukari katika Mikoa ya Mbeya na Rukwa, Kampuni ya Sukari ya Kilombero imefungua ghala la kuhifadhi sukari Mjini Mbeya na kila wakati inahakikisha kuwepo kwa tani 300 hadi 500 za sukari katika ghala hilo. (Makofi)

Kutokana na matatizo ya upatikanaji wa sukari katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya na Ruvuma, Serikali imeruhusu uingizaji halali wa sukari kutoka Malawi na Zambia hadi viwanda vyetu vitakapoweka utaratibu mzuri wa kusambaza sukari katika Mikoa hiyo na Mikoa mingine ya mipakani. Uingizaji huo utazingatia viwango vitakavyowekwa na Bodi ya Sukari Tanzania. Aidha, Bodi ya Sukari imeagizwa kuimarisha usimamizi ili wafanyabiashara wasitumie mwanya huo kuendelea kuingiza sukari nchini isivyo halali.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba kuna *godown* ya sukari imewekwa kule, sisi kule Mkoani Mbeya hatujaona sukari yenyewe hata kidogo. Je, anatuambia nini katika suala hilo?
- (b) Kama wameruhusu Zambia na Malawi kuleta sukari kwetu, mbona wafanyabiashara wale wadogo wadogo wanasumbuliwa kiasi ambacho inabidi wapite njia za panya; pia, Waziri anasemaje katika hili, maana tunakosa sukari katika utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la msingi linasema kutokana na matatizo ya upatikanaji wa sukari katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya na Ruvuma, Serikali imeruhusu uingizaji halali wa sukari kutoka Malawi na Zambia. Itakuwa ni *provision* ya kuweka ghala kwa lengo hili, yaani tuko katika *process* checheto, chachatu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba kwa Mheshimiwa Mbunge, awe na subira tu, ghala litakapokuwepo na wanunuzi tupo sukari itapatikana kwa bei ya wazi wazi na ni nyingi tu. Inavyoonekana hao wafanyabiashara wadogo wadogo wanaleta isivyo halali. Kwa hiyo, tunapenda kutoa mwito kwa wote wanaopenda kuingiza sukari katika maeneo hayo, wawasiliane na Bodi ya Sukari Tanzania kusudi mambo yawe poa. (Kicheko/Makofi)

Na. 182

### Miundombinu ya Maji

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza: -

Kwa kuwa hali halisi ya miundombinu ya maji ya mabwawa, visima, matanki ya kuhifadhia maji vijijini, mabomba na pampu za kupeleka/kusukuma maji vijijini kwa Wananchi na kadhalika imeharibika vibaya na mahali pengi miundombinu hiyo imekufa na haiwezi kutoa huduma kabisa:-

- (a) Je, ni mabwawa, visima, pamoja na matanki mangapi nchi nzima ambayo imekufa au haitumiki kabisa?
- (b) Je, kuifufua miundombinu hiyo inaweza kugharimu kiasi gani cha fedha?
- (c) Je, Serikali itaanza lini kuifufua au kuikarabati miundombinu hiyo na itachukua muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu: -**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard M. Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, ipo miundombinu ya maji kama vile mabwawa, visima, matanki, malambo ya kuhifadhia maji vijijini, mabomba na pampu za maji vijijini, ambayo ama imeharibika kabisa au haifanyi kazi ipasavyo. Matatizo ya miundombinu hii yanatokana na sababu tatu zifuatazo: -

- (i) Kuzeeka kwa mitambo au mabomba;
- (ii) Mabadiliko ya hali ya hewa, kwa mfano, mabwawa kubomoka kwa sababu ya mvua nyingi au kukauka kwa mito, visima au chemchemi za asili kutokana na ukame; na
- (iii) Kuharibika na kuibiwa kwa mitambo na mabomba kutokana na matengenezo na matunzo duni ya miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuendelea kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufukia Desemba, 2003, idadi ya visima vifupi humu nchini vilivyo na pampu za mikono zinazofanya kazi zilikuwa ni 16,089 na visima vilivyo na pampu za mikono ni 2,089. Pia, yapo mabwawa 705 na kati ya hayo 546 yanahitaji kufanyiwa ukarabati. Aidha, idadi ya matanki inakadiriwa kufikia 3,020 na kati ya hayo yanayohitaji ukarabati matanki ni 464.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kufufua, kukarabati mabwawa, visima na pampu za mikono pamoja na matanki ya maji, kiasi cha fedha zinazohitajika ni kama ifuatavyo: -

- (i) Mabwawa yanahitaji kiasi cha Shilingi milioni 18,855;
- (ii) Visima na pampu vinahitaji Shilingi milioni 2,089; na
- (iii) Matanki ya kuhifadhia maji yanahitaji Shilingi milioni 4,364.

(c) Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika, pamoja na Wananchi, inaendelea kukarabati miundombinu ya maji kulingana na fedha inayopatikana kutokana na Bajeti ya Serikali au kwa msaada wa wafadhili mbalimbali humu nchini. Aidha, siyo rahisi kubaini muda wa kumalizika kwa ukarabati wa miradi ya maji kwani hali hii itategemea sana jinsi Serikali itakavyopata fedha za kutekeleza kazi hii pamoja na shughuli zake nyingi ambazo zinaeleweka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kadhalika, hali hiyo itategemea kasi ya Wananchi ya kuunda vyombo vyao kisheria waweze kuendesha na kulinda miradi yao ya maji. Hata hivyo, Wizara yangu inaendelea kutathmini miradi yote ili kujua ukubwa wa kazi iliyobaki.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nimetumwa na Wananchi wa Vijiji vinavyokaa karibu na miundombinu ambayo ameitaja Mheshimiwa Waziri. Je, Serikali au Waziri anaahidi nini kuhusu kukarabati haraka iwezekanavyo ili kuwaondolea adha Wananchi wanaoishi karibu na Vijiji ambavyo miundombinu yake imeharibika? Vijiji hivyo ni Songambe, Kinambeu, Kaselya, Mtoa, *Old Kiomboi*, Ndago, Kinampanda, Kisiriri, Maluga, Urugu, Kidaro, Usunsu na Wembere?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoieleza, miundombinu na maeneo mengi ya miradi hii ya maji iliwekwa miaka mingi iliyopita na miundombinu hiyo imeharibika kwa sababu nyingi kama nilivyoieleza. Sasa, kwa hamasa hiyo hiyo ya Mheshimiwa Mbunge kutaka kuona Serikali inasaidia katika kukarabati miundombinu hiyo, ningepomba aelewe usemi mmoja kwamba: “Nikikupa mkono kukusalimia ni vizuri pia na wewe ukaniletea mkono, lakini niki-*extend* mkono wangu wewe ukakaa kimya na mimi sioni sababu ya kukusalimia.”

Kwa maana hiyo, ningependa sana Mheshimiwa Mbunge, aje ofisini kwetu atueleze kwa kiasi gani wao wamejitayarisha katika kukarabati miradi ambayo imechakaa ili Serikali tuweze kuona kuwa kweli sasa hivi kuna nia na matatizo yaliyokuwepo hapo nyuma hayapo tena, kwamba wataisimamia na kuulinda na kuifanya kuwa miradi endelevu. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, aje ofisini kwetu ili tuje tuone jinsi gani tutasaidiana kwa nia hiyo hiyo ya kuweza kuwasaidia Wananchi wa Jimbo lake.

Na. 183

### **Maji Kijiji cha Kinyasi**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza: -

Kwa kuwa Kijiji cha Kinyasi katika Jimbo la Kondo Kaskazini kina shida kubwa ya maji kwa matumizi ya nyumbani na mifugo kwa sababu maji yanayotokana na chemchemi iliyopo katika mlima wa Kinyasi hayatoshelezi kwa wananchi na mifugo yao kijijini hapo na kwa kuwa tanki lililopo ni dogo na kwamba linashindwa kusambaza maji kwenye maeneo ya vitongoji vilivyopo na kusababisha Wananchi kufuata maji masafa marefu kwenye Vijiji vingine, kitu ambacho kinawapotezea muda wa kazi zingine za kujenga Taifa Wananchi hao:-

(a) Kwa kuwa tatizo hilo limedumu kwa muda mrefu takribani mika zaidi ya mitano bado kutafutiwa ufumbuzi; je, ni tatizo gani hasa la kiufundi lililogundulika katika mtandao huo wa maji na kama limegundulika, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo hilo?

(b) Je, ni kwa nini tanki la maji lisingejengwa kwenye kilima ili kutiririsha maji kwa wingi na haraka kinyume na lilipo sasa na maeneo yanayohitajika kusambazwa maji?

(c) Je, ziko chemchemi ngapi katika mlima huo ambazo zingeunganishwa na kutoa maji mengi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mbunge wa Kondo Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kinyasi kipo katika Kata ya Pahi na kinakisiwa kuwa na wakazi 6,200 ambao mahitaji yao ya maji ni mita za ujazo 220 kwa siku. Mradi wa Maji unaohudumia kijiji cha Kinyasi ulijengwa na Serikali mwaka 1974 na kufanyiwa ukarabati mwaka 1999. Mradi huu ulikuwa unahudumia pia Kijiji cha Ikengwa. Vyanzo vya mradi huu ni chemchemi mbili ambazo kwa pamoja zilikuwa na uwezo wa kutoa kiasi cha maji cha mita za ujazo 334 kwa siku. Kutokana na uharibifu wa mazingira, chemchemi moja ambayo ilikuwa inatoa kiasi cha maji cha mita za ujazo 104 kwa siku

imekauka na hivyo haitumiki kwa sasa. Hali hii imesababisha upungufu mkuwa wa maji katika Kijiji cha Kinyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza tatizo la maji katika Vijiji hivi, Serikali imechimba kisima kirefu na kufunga pampu kwa ajili ya kuhudumia Kijiji cha Ikengwa. Kazi hizi zimetetelezwa katika kipindi cha mwaka 2002 kwa msaada wa *Belgium Survival Fund/International Fund for Agriculture Development (BSF/IFAD)*. Mradi wa zamani utabaki kuhudumia Kijiji cha Kinyasi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupanua huduma ya maji katika Kijiji cha Kinyasi itazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kujenga tanki kwenye kilima ili liweze kuhudumia pia Wananchi ambao sasa wanaishi katika maeneo ya juu.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanyika umeonyesha kuwa, hakuna chemchemi zaidi ya zile zinazotumika na kutoa maji katika eneo husika.

Na 184

### **Uvuvi Haramu**

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD (k.n.y. MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 1988 kabla ya Azimio la Rio de Janeiro kuhusu mazingira Vifungu vya 6(1) - 13(1), 15 - 16 - 17 na 18 vinapiga marufuku uchaguzi wa maji ya bahari na uvuvi haramu wa utumiaji wa juyo, Baruti, Sumu na Bunduki ya Pwani (mishale). Aidha, utumiaji wa nyavu zenye matundu chini ya inchi moja na nusu katika sehemu za pembezoni mwa fukwe na mafungu na kwa kuwa kanuni kuu za uvuvi za mwaka 1993 vifungu vya 30(1), 31(1), 32, 33, 35, 48 na 50 vinalenga suala la uhifadhi wa mazingira ya baharini na kwamba Serikali inakataza uvuvi haramu: -

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba pamoja na amri za Serikali zote mbili, bado kuna wavuvi kutoka Tanzania Bara wanaendelea kupuuzwa na kuvunja amri, kwa kuendesha uvuvi huo uliokatizwa kwenye Bahari ya Kizimkazi?

(b) Je, Serikali imewahi kupokea malalamiko yoyote toka Idara ya Uvuvi, Maliasili na Mazingira Zanzibar kuhusu madai hayo na kama jibu ni ndiyo, je, ni matukio mangapi yamewahi kutolewa taarifa na Serikali imechukua hatua gani?

(c) Ili kuhakikisha kwamba uvuvi haramu hauendelei kufanyika katika eneo lote la bahari, je, Serikali itachukua hatua zipasazo ili kukomesha tatizo hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Awali ya yote, naomba nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, hatuna Bahari ya Kizimkazi isipokuwa tuna eneo la Kizimkazi katika Zanzibar. Baada ya kusema hilo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali haina taarifa zozote kuhusu wavuvi kutoka Tanzania Bara kwenda kufanya uvuvi haramu mwenye eneo la Kizimkazi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu (a), Serikali haijawahi kupokea malalamiko yoyote toka Idara ya Uvuvi, Maliasili na Mazingira, Zanzibar, kuhusu madai hayo na kwa msingi huo hakuna hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa na Serikali hadi sasa.

(c) Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kusimamia rasilimali za uvuvi kwenye maji yake, mikakati hiyo ni pamoja na:-

- Kuendesha doria za mara kwa mara za majini kwenye eneo lake la maji;
- Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Idara wanaohusika na kuendesha doria za baharini;
- Kuweka wasimamizi kwenye meli za uvuvi wa kamba;
- Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Uvuvi Na. 6 ya mwaka 1970 ili kutoa viwango vya adhabu vinavyoendana na uzito wa kosa; na
- Kutoa Elimu ya uvuvi endelevu kwa wananchi.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, awahamasishe wananchi wanaoishi karibu na eneo la Kizimkazi, ili waweze kutoa ushirikiano katika kusimamia matumizi ya raslimali ya uvuvi kwa lengo la kuwa na raslimali endelevu. Iwapo Mheshimiwa Mbunge, anayo taarifa yoyote ya uvuvi haramu katika eneo la Kizimkazi, ninamwomba aiwasilishe katika Wizara yangu ili iweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja kama ifuatavyo: Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, limeongezeka wimbi kubwa la uvuvi haramu hasa hawa wanaotumia baruti. Je, endapo watu hao watakatwa Serikali itawachukulia hatua gani?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kama nilivyosema kwamba, sheria ipo na kwamba wakikamatwa hawa wanafungwa na mali zao zinataifishwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumemaliza maswali. Kama mnavyojua leo ndiyo siku ya mwisho ya Mkutano huu. Ningependa kutoa taarifa tu, kuanzia sasa kutakuwa na michango ya Waheshimiwa Wabunge, mpaka saa 6.00 mchana, kuanzia saa 6.00 mchana mtoa hoja, Waziri Mkuu, atajibu zile hoja. Baada ya yeye kumaliza tutasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni wakati ambao itatolewa hoja rasmi ya kuahirisha Mkutano huu mpaka mkutano ujao. Kwa hiyo, kutakuwa na wachangiaji ambao ninao kwenye orodha mpaka hiyo saa 6.00 mchana. Ninao wachangiaji wengi lakini wale watakapata nafasi na imezingatiwa wale ambao hawajachangia kabisa, kuna misingi imetumika katika kuwapata.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ambaye anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo Ijumaa, saa 7.00 mchana kuna kikao cha dharura Chumba Namba 227 ghorofa ya pili. Pia Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, anawatangazia wale ambao aliwapatia madododo ya kujaza kuhusu kuondoa umaskini, anaomba wale ambao hawajamrudishia warudishe kwake ili waweze kuyafanyia kazi. Hayo ndiyo matangazo yaliyokuwepo. Tunaendelea Katibu.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

### **Muswada wa Kodi ya Mapato wa Mwaka 2004 (The Income Tax Bill, 2004)**

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

### HOJA YA KUJADILI HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA BENJAMIN WILLIAM MKAPA

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, ninayo orodha ndefu hapa. Lakini asubuhi hii anayeanza kuchangia ni Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, atafuatiwa na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga na Mheshimiwa Stephen Kahumbi pia ajiandae.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nilikuwa nimetoa jina langu nilikuwa sijajiandaa kwa hiyo, naomba mwingine labda afuate. Ahsante.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais asubuhi hii ya leo. Kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa Hotuba yake nzuri. Ninampa pole kwa maradhi yanayomsibu na namwomba Mwenyezi Mungu ampe nafuu apone mapema. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa kwenda kwenye Bunge la Afrika, *SADC PF* na kwenye *Commission* ya Bunge. Bila kumsahau Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, aliyeteuliwa na Rais kujiunga nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila tukio lina zama zake. Zama za Mheshimiwa Benjamin Mkapa, ni zama za mapinduzi ya uchumi hapa Tanzania. Tulipita zama za kufufua uchumi, sasa tuna zama za mapinduzi ya uchumi. Mafanikio tuliyoyapata kama alivyoyabainisha Mheshimiwa Rais, yametokana na vitu vikubwa vitatu. Kitu cha kwanza ni Utawala Bora. Tangu Rais Benjamin Mkapa, ameingia katika utawala, utawala wake ulikuwa bora kwa sababu unafuata sheria, kanuni na taratibu tulizojiwekea japo watendaji wachache hupotosha taratibu au kanuni. Haya ni mambo ya kibinadamu. Lakini pili kuna uwazi na ukweli ambao unasaidia sana kusukuma maendeleo haraka. Mwisho, kuna kuwajibika. Watendaji na viongozi mbalimbali, Waheshimiwa Mawaziri wake aliwapa nishani ya kuwa wanaanga na kwa kweli wote wanatekeleza wajibu wao vizuri na wanafuatilia mambo yanavyotakiwa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kufanikiwa sana kwa sababu ya ushirikishwaji wa umma katika shughuli zetu. Shughuli za ujenzi wa madarasa, uimarishaji wa elimu ya msingi umefanikiwa sana kwa sababu tumewashirikisha wananchi katika utendaji. Ukiwashirikisha watu wanaona kitu hicho kuwa ni sehemu ya kazi zao. Lakini unapowashirikisha unatimiza ile sera ya mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. Kwa kweli nchi yetu ni maskini kama tungetegemea vitu vingine zaidi ya nguvu ingekuwa vigumu sana. Hata hivyo, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ametuambia na nakubaliana naye kwamba, sasa umefika wakati ambapo kitu kingine zaidi ya nguvu za wananchi kinahijitaka. Ametuambia kwamba, sasa tunahitaji kuwa na mtaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi tuliyoipitisha juzi juzi hapa ni moja ya kuwapatia wananchi mitaji ya fedha kwa sababu tunawaruhusu wananchi kumiliki ardhi. Kwanza, tumeiwekea ardhi kuwa na thamani, tunawaruhusu kuimiliki, kuiweka rehani wakapata fedha kutoka vyombo vya fedha. Hii ni kuwawezesha wananchi kupata mtaji wa fedha. Lakini hata hivyo pamoja na hotuba hii nzuri, nilipenda kukumbusha mwaka 1999 tulipokuwa tunaingia Karne ya 21 niliwahi kusema hapa Bungeni kwamba, wengine tutaingia kwenye Karne ya 21 tutawasindikiza tuwapeleke mpaka kwenye mlango wa kuingilia kwenye Karne ya 21 tuchukue kalenda turudi Karne ya 19. Hii imejidhihirisha hata leo Wabunge wamesema kwa sababu sidhani Mikoa kama ya Tabora, Kagera, Kigoma ambayo haiunganishwi hata na Mikoa ya jirani kwa barabara ya kudumu, ungeluweza kuipeleka *airport* kupanda ndege anayoondoka nayo Rais Mkapa. Wengine mtatuacha hata kiwanjani hatujafika, kwa sababu miundo mbinu ndiyo inarahisisha maendeleo.

Sisi hatuna barabara, hatuna umeme, hata lilipokuwa linajibiwa swali hapa nilitaka nimwulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa nini fedha nyingine zinazokwenda kwenye Mikoa, Mikoa mingine inapata fedha nyingi, Mikoa mingine inapata fedha kidogo za maendeleo? Ni kwa sababu

ni wazi kabisa wawekezaji wako kwenye Mikoa yenye umeme, wawekezaji wako kwenye barabara nzuri. Sasa Mkoa kama wa Tabora au rafiki zangu wa Kigoma au wa Kagera, labda Kagera sijui sijafika mimi tangu nizaliwe, lakini Kigoma nimefika hawana umeme, hawana barabara. Tabora hatuna barabara, hatuna umeme. Hata barabara hii inayojengwa sasa hivi inapita nchani kwenye Kata ya mwisho ya Wilaya ya Nzega. Inaingia Igunga, afadhali ya Igunga imekatwa katikati. Umeme katika Wilaya ya Nzega uko, Nzega Mjini na katika vijiji viwili. Jambo la kusikitisha ndiyo niliyosema kwamba, tunafuata kanuni, taratibu lakini wakati mwingine taratibu watendaji wanazifanya kiajabu tu. *(Makofi)*

Pale Nzega wameteremsha umeme kuna *sub-station* ambayo imechukua umeme kwenda Igunga. Lakini kwenye kijiji chenye ulipoteremshwa umeme kujiji kile hakikupewa umeme. Unashangaa pale kuna Kituo cha Afya, kuna mgodi mdogo, wachimbaji wadogo wadogo wako pale, wameteremsha umeme wakauvurumisha mpaka Igunga, huko Igunga ndiyo wakasambaza kwenye vijiji. Sasa hizi taratibu, sera unaibadili makusudi tu, mambo haya yanaleta migogoro ya maendeleo. Hatuwezi kudai kwamba watu wa Wilaya hiyo wanapewa fursa sawa ya kuleta maendeleo, kwa sababu mwanadamu haendelezwi kama alivyosema Mheshimiwa Benjamin Mkapa, hatuwezi kugawa hela kama wanavyodai wengine, lakini tuwape fursa. Sasa fursa kama hii unateremsha umeme kwenye kijiji unapeleka maili 80 pale unawanyima, umewapa fursa kweli?

Kwa hiyo, hii miezi 20 ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, iliyobaki anasema *ai-take off*, sisi atatuacha *airport* pengine tutakuwa hata *airport* hatujafika. Mimi siamini kabisa kwamba, Mikoa hiyo ya Kigoma, Tabora, Kagera na mingine ambayo haina hata umeme itakwenda pamoja na wenzao maana tumenyimwa fursa. Sasa sijui katika miaka 20 itakuwaje? Mimi nimeingia hapa Bungeni mwaka 1985, tangu nimeingia hapa nadai umeme Nzega, nilipoingia mwaka 1985 hata Nzega yenyewe ilikuwa haina umeme. Nimedai umekuwa toka Shinyanga ukawekwa Nzega, ukapita vijiji njiani wananchi wakanisaidia wakawa wanakata nyaya, wanafungua *bolts* wanatengeneza oksikatis wakawakamata, nikasema msiwakamate hawana faida nao umeme. Wakateremsha kijiji kimoja cha Nata mpaka leo basi. Sasa na mimi nitamsindikiza Mheshimiwa Mkapa maana sitagombea tena Ubunge. Sasa nitaondoka katika Bunge hili umeme Nzega haujafika. Mimi nimepiga kelele tangu mwaka 1985. Sasa sijui ndugu yangu Waziri wa Nishati na Madini na sasa ameingia Naibu Waziri, mtani wangu, nikisema anasema utani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hotuba hii ilikuwa nzuri mno, ningekuwa sina maneno mengi sana ya kusema lakini napenda nizungumzie habari ya udhaifu wa Wapinzani. Nafikiri Mheshimiwa Mkapa asingetia wasiwasi kuhusu udhaifu wa Vyama vya Upinzani. Hiki kitu siyo cha kumfanya asilale, alale tu, wao waliambiwa mapema na Baba wa Taifa kwamba, anzisheni vyama vichache, utitiri wa vyama hauwafikishi mahali. Sasa tuwaacha wafe polepole, watakufa kama *Congress*, sisi kwenye TANU tuliacha *Congress* ilikufa tu, *AMUNIT* ilikufa tu na hawa watakufa tu. Sasa hiki siyo kitu cha kumkosesha usingizi Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alale mpaka saa 4.00 waache wafe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niseme kidogo tu ni njaa. Mheshimiwa Rais, alinifurahisha sana kwa kutukumbusha msemu wa Wachina kwamba, huwezi kufunika moto kwa karatasi, itaungua karatasi. Tumekuwa tukisema kwamba, jamani kuna njaa Waswahili tumejifunze lugha nyingi tu, watu wanasema hakuna njaa ila kuna upungufu wa chakula, sijui maana yake ni nini? Sasa hivi tuna njaa, Mheshimiwa Rostam Aziz, nilimsikia juzi alikwenda kununua chakula kwa ajili ya watu wake wa Igunga, namshukuru sana. Lakini Serikali imetusaidia imetuletea mahindi tangu mwezi Desemba huko Nzega, nashukuru sana kwa niaba ya watu wa Nzega kwa msaada tulioupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kuwapotezea muda mwingi sana, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya ya Mheshimiwa Rais. Kabla ya kufanya hivyo, napenda pia niwapongeze Wabunge waliopata nafasi katika Bunge la Afrika, *SADC* na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kujiunga na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wote nawapongeza. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia. Naunga mkono hotuba hiyo kwa sababu ina miongozo tosha kwa Taifa na pia ni ushuhuda kwa Mataifa wa hali halisi Watanzania tulivyo miongoni mwa Mataifa. Nitatumia kauli nukuu aliyoitumia Mheshimiwa Rais katika hotuba yake, chini ya kifungu cha kubadili Fikra na Usimamizi wa Uchumi wa Soko alitoa majibu kwa mwananchi mmoja aliyekuwa amelalamika. Nanukuu malalamiko ya huyo mwananchi, alisema: "Unajua ninyi wenye saa mnatuchanganya kweli, siku nzima ya leo nimekuwa nauliza watu wakati na mara zote nimepewa majibu tofauti". Mheshimiwa Rais akajibu akasema, nanukuu: "Na mimi nawaambia watumishi wa umma kuwa wasiwalaumu wenye saa wala wasichanganyikiwe. Ukweli ni kuwa nyakati zinabadilika haraka na majibu lazima yabadilike".

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo haya yana hekima kubwa na nzito. Yanatuhimiza viongozi kwamba lazima tutafute majibu tofauti kwa matatizo yetu na Baba wa Taifa alitoa kielelezo kizuri sana pale alipotaka kutekeleza Mradi wa *TAZARA*. Watu wa nchi za Magharibi walimwambia kwamba huo mradi hauna faida kiuchumi, ni ghali mno na nchi ni maskini. Angekuwa hakutafuta majibu mbadala basi mradi ule usingetokelezwa. Lakini alikwenda nchi za Mashariki ya Mbali na ndugu zetu Wachina wakasema tutautekeleza kwa ufanisi mkubwa na kwa muda mfupi na hayo yalifanyika. Leo faida ni dhahiri kwa mradi huo ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge, wanaulizia ni kwa nini hatujatumia makaa ya mawe yaliyoko kule au chuma kilichoko kule? Hayo ni matokeo ya kutafuta majibu tofauti kwa tatizo lililokuwepo. Mbinu kama hiyo zimetumiwa vizuri na Serikali ya Awamu ya Tatu. Kwa hiyo, nampongeza Rais na Serikali yake katika kipindi hicho.

Mawaziri wengi ambao wamekuwa wakichachalika kwenda huko na huko kutafuta majibu tofauti, wamethibitisha kwamba, mambo mengi yanawezekana. Ni dhahiri wote tunakumbuka Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa mfano, ilivyobadili lengo toka mwaka 2015 hadi mwaka 2006 kwa Mpango wa MEM. Wizara hiyo chini ya Waziri, Mheshimiwa Joseph Mungai, wameweza kurekebisha malengo hayo ya mwaka 2015 na kuyafanya yawezekane mwaka 2006, hayo ni mafanikio makubwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali. (*Makofi*)

Eneo la pili ambalo Rais, katika hotuba yake amelijengea hoja na mimi nakubaliana naye ni katika eneo la utandawazi. Chini ya kifungu cha utandawazi aliposema nanukuu: "Dunia iliyopo nje ya nchi yetu inaweza kuendelea bila sisi. Lakini siamini kwamba sisi tunaweza kuendelea bila dunia hiyo". Mimi nakubaliana naye na napenda kumpongeza na Serikali yake kwa sababu wamechukua hatua nyingi za kuridhia Mikataba ya Kimataifa.

Moja ya Mikataba muhimu ambayo nakumbuka ni ule Mkataba wa Ardhiyeu ya Bonde la Mto Malagarasi na Mto Myovosi. Hili ni eneo kubwa sana lenye hekta zipatazo milioni 3,250,000. Ni bonde lenye ardhi ya ajabu. Hili bonde kwa raslimali zilizoko mle limechukuliwa kama urithi wa dunia (*The Global Heritage*) na Tanzania ilianguka Mkataba wa Hifadhi ya bonde hilo mwaka 2000. Tangu mwaka 2001 imeanza kuliendelea. Lakini ninachoomba katika hili, kama mipango yetu ikiwa ni ile ya kutafuta majibu tofauti kama alivyotuelekeza Rais, basi bonde hili linaweza kuchangia katika kuondoa njaa katika Taifa letu. Wakati fulani Mheshimiwa Ndaboina alisema upeni Mkoa wa Kigoma ulishe Taifa, lakini baadhi ya Wabunge, walionyesha kama siyo kitu kinachowezekeka. Kwa kuwa fursa zilizopo na raslimali zilizoko kule hazijatumika na ningetarajia bonde kama hili ambalo lina aina 56 ya samaki ambao hawapatikani mahali pengine duniani, bonde ambalo katika Mto Malagarasi una mamba ambao hawapatikani mahali pengine duniani. Bonde ambalo lina aina ya ndege wa kiasili ni sehemu yenye mvuto kiutalii.

Tunaposema Mkoa wa Kigoma tunahitaji umeme siyo kwamba tunafanya hivyo kama kitu cha anasa. Tunasema eneo kama hili ambalo Mkoa umepewa dhamana ya kusimamia kwa niaba ya Jumuiya ya Kimataifa, lithafadhiwa namna gani kama wananchi wake wataendelea kutumia kuni katika maeneo hayo, kama wananchi wake hawatakuwa wameunganishwa na majirani zao wa Tabora maendeleo yatapatikana vipi? Mheshimiwa Lucas Seleli, jirani yetu toka Nzega alisema watu wa Tabora ni wachapa kazi, nakubaliana naye na hivyo ndivyo ilivyo pia kwa watu wa Kigoma. Hakuna asiyejua kwamba watu ambao wanaweza kuchapa kazi. Kama fursa zilizopo, raslimali zilizopo, mipango ikitekelezwa tunaweza kufikia mahali pa kulisha Taifa hili kwa kiasi kikubwa sana. Viongozi waliotangulia Rais Mtaafu Ali Hassan Mwinyi, aliwahi kusema alipotembelea Kigoma kwamba: "Panda chuma kitaota". Alikuwa na maana ya

namna kushawishi matumizi mazuri kuzalisha chakula kingi sana kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, si hilo tu, mto Malagarasi kwa taarifa za *TANESCO* waliwahi kutueleza kabisa kwamba, unauwezo wa kutoa *megawatt* 80 za umeme katika maporomoko ya Igamba ikaonyesha kwamba ni *megawatt* 45. Utafiti uliofanyika na makampuni ya nchi za Magharibi ulionyesha kwamba, utekelezaji wa mradi huo utagharimu dola milioni 43, lakini utafiti wa *Sivaguru Engineers* kutoka India wao wanasema unaweza kuendelezwa mradi ule kwa awamu tatu na ukatoa *megawatt* 28 ambayo ni mahitaji zaidi ya Mkoa wa Kigoma. Ukiacha huo umeme unaweza kutumia pia chanzo kingine ambacho siyo maji. Kasulu kuna makaa ya mawe na kama Waheshimiwa Wabunge, ambavyo wamekuwa wakisisitiza, makaa ya mawe ni chanzo mbadala cha umeme. Kamishna wa Madini analijua hilo kwamba kuna makaa ya mawe Kasulu. Kwa hiyo, eneo kama hili, lazima tuwe na sababu ya kuliendeleza na tuwe na sababu ya kutumia maelekezo aliyotoa Rais hapa kwamba, lazima majibu yawe tofauti kwa sababu bila kuwa na majibu tofauti tukiendelea na majibu yale yale kwamba hatuna fedha, hatuwezi kuleta maendeleo katika uwiano tunaoutaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mawaziri waliotembelea Kigoma akiwemo Waziri wa Elimu na Utamaduni, Waziri wa Kilimo na Chakula, Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Waziri wa Nishati na Madini. Hawa tunashukuru sana. Wapokuja wana nafasi nzuri majibu tofauti na yale yaliyozoeleka. Kwa hiyo, ni wito wangu kwa Mawaziri wengine kama Waziri wa Afya, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sisi tuna matatizo. Ni vema atembelee aone mwambao wa Ziwa tunavyohangaika. Aone watu wanavyonyang'anywa nyavu zao, wanavyonyang'anywa *engine* zao na hapa ataweza kupata majibu tofauti ya kutatua tatizo hilo. Nitoe wito pia kwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo naye atembelee Bonde hilo la Mto Malagarasi katika vijiji vya Nguruka, Mtegwanoti ambako nimesikia leo kumetokea upepo mkali ambao umeezua nyumba, *dispensary*. Kwa hiyo, natoa wito kwa Waziri wa Afya, atembelee eneo hilo pia ili aone hali halisi ilivyo na aweze kutoa majibu tofauti na yale yaliyozoeleka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujalia asubuhi hii kufika hapa na kuweza kushiriki katika shughuli hizi tukiwa katika hali ya afya njema. Pili, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa ni mdogo tu na nitaanza na pale Mheshimiwa Rais alipogusia matatizo ya kisiasa Zanzibar kufuatia Uchaguzi Mkuu uliopita wa mwaka 2000 na akasema kwamba, matatizo haya yametatuliwa na kwa sasa yamemalizika na akagusia matukio ya tarehe 26 na 27 Januari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi kubwa aliyochukua katika kusimamia kupatikana kwa Muafaka huu mwaka 1999. Nataka nikiri kwamba, kama sio juhudi kubwa na kutumia muda wake wa ziada, Muafaka huu kwa kweli usingepatikana na sijui kama leo hii tungekuwa wapi. Lakini Mheshimiwa Rais, aliweza kutumia muda wake wa ziada kushughulikia suala hili hadi tukafikia hapa ambapo tumefikia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa Muafaka umetekelezwa lakini pamoja na hayo, bado kuna mambo ya msingi kwa kweli hayajatekelezwa. Kwa bahati mbaya sana, kwa mujibu wa makubaliano ya Muafaka, basi Muafaka wote uliotarajiwa ungekuwa umetekelezwa kabla ya kufanya Uchaguzi Mdogo wa Mei, 2004. Kwa mfano, baada ya Mheshimiwa Rais kuona Tume ya Kuchunguza Matukio ya tarehe 26 na 27 ya Mheshimiwa Mbita na kufuatilia matukio yale na hatimaye kutoa ripoti kwa Mheshimiwa Rais, ilikubalika kwamba hadi itakapofika tarehe 31 Desemba, 2002 hicho kifuta machozi kilichotajwa na Serikali, kingetakiwa kiwe kimelipwa kwa waathirika wa matukio ya tarehe 26 na 27.

La kusikitisha zaidi ni kwamba, hadi hii leo tunazungumza hapa bado kifuta machozi hicho hakijatolewa. Binafsi niliuliza suala hili tarehe 4 Novemba, 2003 juu ya hatma ya suala hili, nikajibiwa kwamba, mipango iko mbioni kutayarishwa na baada ya muda mfupi tu mambo haya yatakuwa yamekamilika na kifuta machozi hiki kitakuwa kimelipwa. Tumekaa mpaka juzi mwenzangu mmoja naye akaulizia tena suala hili, majibu yalikuwa ni hayo hayo. Sasa hili kwa kweli linanitia mushkeli kwa sababu yapo matukio kadhaa ya maafa yaliyotokea baada ya matukio haya ya Januari na fidia hiyo imetolewa kwa wananchi hao, lakini haya matukio ambayo yamepita muda mrefu zaidi bado kila siku yanapangiwa tarehe.

Wakati ule nakumbuka suala hili nilipoliuliza nilipata majibu kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera), akijibu kwa niaba ya Waziri Mkuu. Mwenzangu mmoja alipouliza swali lile lile, kajibiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Utawala Bora). Sasa mimi hapa nachanganyikiwa, hivi *who is responsible* kwa suala hili? Kutokana na kujibiwa na watu wawili tofauti suala lile lile napata wasiwasi kwamba hili suala linapigwa chenga na inawezekana tukamaliza mpaka 2005 suala hili lisipate jibu.

Sasa maombi, Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi kutekeleza yale yanayomhusu mbebe ya Watanzania na mbebe ya dunia kwamba atayatekeleza. Mimi nina wasiwasi kwamba, suala hili Mheshimiwa Rais haelezi ukweli. Lakini kama ninavyomjua na alivyosimamia, asingekuwa tayari kuona suala hili linapigwa chenga kila siku. Kwa hiyo basi, namwomba Mheshimiwa Rais na watu wake wa katibu wanaonisikiliza, namwomba kabisa hili alivalie njuga, watu hawa ambao wameathirika kwa kiasi kikubwa, hicho kifuta machozi basi kiweze kupatikana katika muda mfupi ujao. Sio heshima kwao tu na faida kwao, lakini pia itakujengea heshima kwa hili na kuondoka katika madaraka ukiwa kwa kweli ni mtu uliyejenga matumaini kwa Watanzania bila kubagua Uanzibari au Utanganyika. Hilo ni moja.

La pili katika suala hilo hilo, sehemu ya pili nimesema kwamba, kwa kiasi kikubwa Muafaka umetekelezwa lakini bado kuna mambo ya msingi ambayo hayajatekelezwa. Moja katika hayo ni marekebisho ya Mahakama. Tulikubaliana katika Muafaka kwamba, Mahakama zitarekebisha kufuata mfumo wa nchi za Jumuiya ya Madola. Wataalam walikuja Zanzibar wakatoa mapendekezo yao kwamba, kwa utaratibu wa Mahakama za Jumuiya ya Madola, utaratibu ni moja, mbili, tatu, wakapeleka. Lakini bado hadi leo mambo hayo yamekaliwa na hakuna chochote kilichotokea katika mabadiliko haya ya Mahakama. Moja katika jambo la msingi katika kuendesha uchaguzi ulio huru na wa haki, basi ni kuwa na Mahakama huru halikadhalika. Sasa endapo mpaka tunaingia katika Uchaguzi wa 2005 na bado Mahakama hazijarekebisha kwa mujibu wa Muafaka, napata wasiwasi kwamba, haki inaweza ikakosekana na uchaguzi wa haki ikawa ni ndoto na yakatokea maafa zaidi ya yale ambayo yameshatokea na makusudio yetu ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Rais, yaliyopita si ndwele.

Kwa hiyo, naomba sana suala hili wahusika walichukue kwa uzito wake ili marekebisho haya ya Mahakama yaweze kufanywa ili tuweze kuingia katika uchaguzi wa mwaka 2005 tukiwa na uhakika kwamba, uchaguzi wetu utakuwa ni huru na salama na haki kutendeka na mshindi kwa mujibu wa matakwa ya wananchi akaweza kutangazwa na kumsheherehekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amesema kwamba, katika Uchaguzi wa 2005 tunatarajia kwamba, Daftari la Wapiga Kura litakuwepo. Kwa hili nampongeza Mheshimiwa Rais kutokana na nia yake nzuri kabisa, kuendelea kusimamia uchaguzi wa huru na haki, sio Zanzibar tu lakini Tanzania kwa ujumla. Hivi karibuni tunatarajia kuanza shughuli ya uandikishaji wa Daftari kwa upande wa Zanzibar na tayari kuna baadhi ya maneno tunaanza kuyasikia. Mara panaletwa watu laki moja, mara hivi, sasa kila ikikaribia shughuli ya uchaguzi mambo kama haya hujitokeza. Sasa wito wangu kwa Serikali ya Muungano, ambayo ndiyo ina dhamana ya kuhakikisha usalama wa wananchi wote wa Tanzania, naiomba sana Serikali ya Muungano ichukulie suala hasa la uandikishaji wa wapiga kura kwamba ni suala nyeti sana, linahitaji usimamizi kama mlivyoweza kuchukua juhudi kusimamia Uchaguzi Mdogo kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa juhudi kubwa aliyoichukua katika kuhakikisha kwamba, uchaguzi umekwenda salama na kwa kweli kwa kuwa aliamua hivyo na kweli uchaguzi ulikwenda salama, hakuna mtu aliyeguswa hata

pele. Namwomba tena Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, asimamie uandikishaji uende kwa mujibu wa sheria inavyotaka na hata pele mtu asiweze kukunwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Rais alitaja kwamba, mwaka 2005 tunatarajia kuingia kwenye Chaguzi za Serikali za Mitaa. Mimi napata wasiwasi kidogo hapa kwamba, sisi tunatumia Tume yetu ya Taifa Uchaguzi, sasa ndio inasimamia mambo ya uchaguzi. Sasa lipi hasa la msingi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. Napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, muda ni dakika kumi.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu, inayohusu Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuungana na wenzangu kuwapongeza Wabunge wenzetu, ambao tumewachagua kwenda kutuwakilisha katika Mabunge mbalimbali na katika Tume ya Huduma za Bunge. Vile vile nampongeza mdogo wangu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge katika Bunge hili la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwapongeze wenzetu walioweza kwenda Hija ya mwaka huu ikiwa ni katika harakati za kutimiza moja ya nguzo tano za imani ya Kiislam. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Nilisikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais na kama ilivyo desturi yangu, nazisikiliza Hotuba zote za Mheshimiwa Rais na kila ninapomsikiliza akizungumza, siachi kumkumbuka kiongozi mmoja ambaye mpambe wake alimwambia kwamba: "Mkuu nimesikiliza hotuba zako katika miaka ya hivi karibuni na *every speech you make is worse than the previous one*". Sasa huyo mpambe alikuwa jasiri. Lakini kwa Hotuba za Mheshimiwa Rais wetu naweza nikasema *every speech I listen to is better than the previous one*. Ningependa kumpongeza sana. Tulipata msamiati mpya, wengi tulikuwa hatujui maana ya unyumbulifu, leo tunajua na vile vile hotuba yake ilikuwa imejaa takwimu. Takwimu kama tunavyojua ni nyenzo ya kupima maendeleo na utekelezaji wa mipango yetu. Taarifa na hotuba ambazo hazina takwimu ni porojo tu hizo. Kwa hiyo, ningependa nimpongeze kwa hotuba hii ya kisayansi, nampa hongera nyingi. Vile vile nawapa hongera Watanzania, wanastahili pongezi kwa sababu walichekecha na kuchuja mpaka wakampata mtu mwenye kipaji kama Rais wetu, mtu mchapakazi na tunawashukuru sana Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyoona katika hotuba yake, takwimu zimetumika katika kila sekta aliyoiugusia, ndiyo hiyo inatuonesha hapo tulipotoka, tuko wapi sasa hivi na tunaelekea wapi. Upande wa elimu wenzangu wengi wamechangia na tunatambua kwamba, wananchi sasa hivi wanatambua umuhimu wa elimu. Wanatumia nguvu zao, wanaongeza vyumba vya madarasa vyenye madirisha mapana, wanakarabati shule na nyumba za walimu. Sasa hivi madarasani mwanga ni mwingi, usikivu wa watoto umekuwa mzuri na upatikanaji wa vitabu umeongezeka. Ningependa niishukuru Serikali na kuipongeza Wizara ya Elimu kwa kusimamia vizuri mradi wa MEM na vile vile kwa Serikali nzima kwa juhudi ambazo *TASAF* inatusaidia.

Lakini katika kuboresha hivi vyumba vya madarasa na usikivu wa wanafunzi wetu, nia yetu ni moja. Ni kwamba, tunataka tuboreshe taaluma kwa sababu miaka ya hapo katikati kulikuwa na malalamiko makubwa kwamba watoto wetu walikuwa hawafaulu. Sasa takwimu tunazo ambazo ni kipimo. Tunataka kuona kama kweli watoto wetu wanafaulu na takwimu zinajionyesha zenyewe kwamba watoto mwaka hadi mwaka toka awamu hii imeingia wanafaulu vizuri. Ningependa kuipongeza Serikali kwa hilo.

Katika Wilaya yangu ya Rungwe, katika matokeo ya mtihani wa mwaka 2003 wa Darasa la Saba wengine labda mtakuwa hamjui kwamba Rungwe imeshika namba ya kwanza. Yaani katika Wilaya zote takribani 120 wao ndio wamebebwa. Kwa hiyo, ningependa niwape pongezi nyingi sana walimu katika

Wilaya nzima, wanafunzi, wazazi, viongozi, wakiwemo Wabunge wao, ambao ni Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. Wakati tunashangilia matokeo haya, kumezuka *crisis* kwa maana ya kwamba, hatuna Sekondari za kutosha ili tuweze kuendeleza vipaji vya hawa watoto waliofaulu vizuri. Miaka mitatu iliyopita Halmashauri yetu ilipitisha azimio kwamba, kila Kata ijenge Sekondari yake. Ni kazi ngumu lakini tumeweza kuwaelimisha watu wetu kwamba mwanzo ndio mgumu na hivi ninavyozungumza mbele ya Bunge hili, tuna Sekondari karibu 12 ambazo zinajengwa. Kwa hiyo, ningependa niwapongeze sana wananchi kwa kuitikia wito huu. (*Makofi*)

Nimefarijika kusikia habari za MMES ambao ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari na tuna imani kwamba, itatusaidia ili ndoto yetu iweze kutimizwa. Tumepata wahisani wengi, lakini vile vile tumekuwa na harambee ambazo tumealika watu kuja kuchangia ili kusaidia nguvu za wananchi. Kati ya Wabunge wenzangu, tumewakaribisha wengine wawe wageni wa heshima na ningependa niwatambue. Tuliwahi kumkaribisha Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, namtambua pia Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wetu wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye. Wote hawa walikuja kutusaidia kuendesha harambee kama wageni wa heshima, nawashukuru sana. Vile vile kuna Wabunge wenzetu ambao walifunga safari mpaka Rungwe kuja kuongeza nguvu katika shughuli zetu za harambee nao nawataja. Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Ernest Mabina na Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga. Wote hawa walifika na kuungana na sisi na ningependa kusema kwamba, kushiriki kwao kulitutia nguvu na walitoa mchango mkubwa sana katika kufanikisha harambee zetu. (*Makofi*)

Natambua kwamba, kanuni zetu hazituruhusu kurudia yale yaliyozungumzwa na wenzetu waliotangulia, lakini naona nitakuwa sijafanya yaliyo sahihi kama sitagusia suala la Ukimwi, ambalo halijazungumzwa na wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msanii mmoja anayeitwa Komba, ameuita Ukimwi ni mgeni, ambaye ameingia ndani, ameingia mpaka chumbani na hataki kutoka na ndio ukweli wenyewe kwamba, Ukimwi ukitoka, unatoka na mtu. Kama unavyojua *back-ground* yangu hutashangaa nikisema kwamba, nimehudhuria na kushiriki mara nyingi sana katika Semina, Warsha, Kongamano na kuweza kutoa mihadhara inayohusu Ukimwi. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu Ukimwi ambazo nimehusika na yote hayo yametumia mamilioni ya Shilingi. Tulikuwa na msemu nilipokuwa Muhimbili kwamba, wanaofaidika na kuwepo kwa Ukimwi ni wengi kuliko wale wanaokufa kwa sababu ya Ukimwi. Wanaofaidika ni pamoja na watu kwenye miradi, watataka magari, Ofisi zao zina viyoyozi na makompyuta, kuna posho nene nene. Wengi ambao wamewahi kuhudhuria Semina, swali ambalo linajitokeza mara kwa mara hata hapa Bungeni ni kwamba, mbona Bajeti ya Ukimwi ni kubwa sana lakini hizo fedha haziwafikii walengwa? Tuna wagonjwa, tuna mayatima, tuna wajane na watu wengi ambao wameguswa na madhara haya ya Ukimwi lakini hizo pesa wanazisikia tu kwa mbali. (*Makofi*)

Lakini jibu tunaloambiwa ni kwamba, lengo letu kuu ni kuzuia ugonjwa usienee. Serikali inajaribu kuwakinga wale ambao hawajaathirika wasiupate. Kwa hiyo, nyenzo tunayotumia ni elimu, wajue namna ya kutopata huo Ukimwi. Vile vile msisitizo uliopo sasa hivi ni kuwaambia watu waende wakapime kwa hiari na tumeona Vituo vingi vimeanzishwa kama ANGAZA na katika mazungumzo hapa Bungeni tumeiomba Serikali isambaze hiyo huduma hata kwenye *Dispensaries* zetu. Sasa watu wanauliza je, nikipima...

**NAIBU SPIKA:** Dakika kumi zimeshatimia.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Ooh, samahani, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika Hotuba nzuri na ya kupendeza ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Kwanza, kabla sijakwenda mbali sana, niwapongeze wale wote ambao wamepata ushindi mnono wa kutuwakilisha katika Bunge la Afrika, bila kumsahau mdogo wangu Mheshimiwa Charles Makongoro

Nyerere, ambaye ameteuliwa kama kitindamimba. Juzi nilimwambia wewe kwa umri wale wote kumi huwazidi. Kwa hiyo, busara ya Rais ilizingatia kuanzia akina Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira kuja wewe ambaye kiumri inakwenda namna hiyo. Nafikiri mtu wa kwanza kumwona hapa alikuwa Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, aliteuliwa mapema. Sasa kitindamimba ni Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere. Ni wakati muafaka na yeye alikubali kwamba salamu hizo niweze kuzisema hapa ili aweze kusoma hiyo *Hansard* baadaye akiona hilo kwamba ni sehemu yake. (*Kicheko/Makofi*)

Naipongeza Hotuba hii ilikuwa ni nzuri na yale ambayo tumeongea au yametanguliwa kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengine ni ya muhimu, ningeomba tu kwamba, Serikali baadaye mtakapokuwa mnatoa majibu, mjaribu kuangalia ni mambo gani ambayo Wabunge wameongea kwa wingi zaidi, hayo ndiyo yapewe kipaumbele.

Naungana na Waheshimiwa Wabunge ambao wameongea katika suala zima la kilimo na Mheshimiwa Rais ameligusia suala la kilimo kwa sababu njaa ipo na suala la njaa ni kwa sababu aidha yale maeneo ambayo yanaweza kuzalisha chakula hayajitiliwa mkazo wa kutosha au kuna bajeti isiyotosha au wataalam wanajua kwamba pale panaweza pakazalisha kwa wingi, lakini panahitajika msukumo. Sasa suala la kilimo, naomba Mkoa wa Kigoma uingizwe katika Mikoa bora ya uzalishaji wa chakula. Ile *Big Four*, sasa badala ya kuwa na *Big Four* iwe *Big Five*. (*Makofi*)

Kwa sababu hatuelewi dhana ya kupeleka mbolea iliyopunguzwa bei Rukwa, Ruvuma, Iringa na Mbeya, lakini sisi Kigoma, ambao mvua ipo tukashindwa kupunguziwa bei na tunaweza tukazalisha kwa kiwango kikubwa. Sababu ya msingi ni ipi? Hili linaleta lawama kwamba, mbolea sasa hivi kama Serikali inakubali kutoa ruzuku, ipige mahesabu kwa Mikoa yote ile inayozalisha kiwango cha chakula/vyakula vyote.

Nichukue nafasi hii kwanza, kuipongeza Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa sababu Mawaziri wote hawa wamefika Kigoma. Mheshimiwa Charles Keenja amefika, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala ameshatembelea Mkoa wa Kigoma na matatizo au bei ya vyakula aliyoiona baada ya kufika haisumbui, uzalishaji unatosha lakini tuwape nguvu ile ambayo inahitajika sasa. Maana haya hatuongei kinadharia, Waziri yeyote anaweza akifika Mkoani Kigoma akakubaliana kwamba, hawa wanahitaji msukumo. Sasa huu msukumo wa mbolea, hivi sisi tunatengeneza mbolea kutoka wapi? Si mtupunguzie bei tu hiyo mbolea, badala ya huo mfuko wa Sh.25,000/= na sisi tununue kama Rukwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunajiandaa kwenda kununua mbolea Rukwa, hiyo hiyo mnayoipunguza bei, tukubaliane na wale watu basi watuengezee kule, sasa hiyo safari tunapita wapi? Hata hiyo barabara hakuna ya kutoka Kigoma kwenda Rukwa. Maana msipotupunguzia sisi huko Kigoma tutafanya safari zetu, iwe manamba tutatembea tu, tutabeba vichwani mpaka nywele zetu zinyonyoke hapa ziishe. Ndicho mnachotaka sasa! Ndiyo, muipeleke huko huko Iringa, tutatembea kwa miguu maana hata barabara kutoka Kigoma hakuna. Reli sasa hivi mizigo imelundikana hata ya kwenda Burundi imeshindikana kwenda, Mwanza imeshindikana, sasa tutabeba mbolea vichwani ili tuzalishe mje mnunue. Sasa hivi Mkoa wa Kigoma ndio unaolisha Mwanza na Shinyanga. Tuliwaruhusu, hiki kilimo tukitazame!

La pili, mafanikio kuhusu elimu, niipongeze Wizara ya Elimu kwa kufanikisha suala hili, lakini tatizo la ada kwa watoto wetu wengi wanaokwenda Sekondari limerudi kuwa ni kikwazo kikubwa na kigumu kweli kweli. Miongoni mwa idadi kubwa ya watoto wanaokwenda Sekondari, hili limeshaongelewa na Wabunge wengi na mimi nasisitiza, sio kwamba nalirudia, hapana. Tunasisitiza kwamba, tufanye tathmini upya kwamba watoto wengi wanaposhindwa kwenda sasa hivi Sekondari na wazazi wao wamekaa wanasema mtoto wangu alishinda kwenda Sekondari, lakini hawezi, ada imekosekana. *Head Master* anamrudisha. Mmefanya tathmini ya huyo mtoto? Maana kigezo kikubwa cha mtoto kukaa hakwenda Sekondari, ina maana baba yake na mama yake hawakupenda. Ina maana huyo mtoto hawezi kusoma, mtoto wa kitanzania? Yaani tuna watoto wengine wanaoweza kumaliza Elimu ya Sekondari na wengine walishinda tu, akili wanazo lakini kwa sababu ya ukosefu wa Sh.80,000/= ankaa. Wasaidiwe hawa, watoto, tufanye tathmini upya. Kama ni Elimu ya Sekondari, *Form One to Form Four* iwe *free*. Kwa hiyo, angalau tuwa-charge kwenda *Form Five*, *Form Six* kwa sababu wanakuwa wameshakuwa wamepata mwanga, lakini hii iwe kama Shule ya Msingi.

Kuna mambo mengi ya kuweza kuelezea na dakika tano karibu zinakwisha, sasa niende lingine. Nampongeza Waziri wa Elimu na MMES mjaribu kuisukuma angalau iweze kupata Sekondari nyingi za Kata na nampongeza kwa sababu mpango huo Waziri wa Elimu ameshaulezea.

La tatu, ni suala la barabara. Mimi nimpongeze Waziri wa Ujenzi, nilikuwa na kipande cha kilometa 50 tangu mwaka 1990 hakijatengenezwa.

Nimekwenda Ofisini kwa Naibu Waziri wa Ujenzi mara 25 kuomba Mwandiga-Manyovu, mpaka yeye mwenyewe kila nikiingia pale, anasema umekuja kwa ajili ya Mwandiga-Manyovu? Sasa bwana nikija Dar es Salaam naomba chai ya maziwa sasa. Ahsante, nitakunywa.

Baada ya juhudi hizo kufanyika wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini sasa hivi wanapongeza hatua hiyo ya mwanzo na mimi nakupongeza kwa sababu kwa kufanya hivyo shughuli ya uzalishaji inaleta matumaini sasa. Lakini kipande hicho hicho naomba sasa mpango wa kukitengeneza kwa lami uanze hivi karibuni yaani ukishatengeneza hiyo ukishamwagia hiyo changarawe anza mpango wa lami sasa ndiyo *target* yetu kwa sababu inaenda mpaka Burundi. (*Makofi*)

Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Burundi alikuwepo hapa jana, alikuja kutembelea Bunge. Moja ya msisitizo ni kwamba hii mizigo ipitie pale kwenye hiyo barabara kwenda Burundi, Rwanda mpaka Kongo. Kwa sababu inapata shida inaposhushwa kwenye *train* halafu iingie ndani ya maji kwenye *store*, itoke kwenye *store* irudishwe tena ipandishwe halafu kule tena itakuwaje. Hiyo barabara itakuwa imeshawaletea wepesi.

Sasa naomba Wizara ya Ujenzi, salaam hizi naomba kwa kweli pamoja na kwamba hizi juhudi mmefanya lakini *agenda* ni kwamba barabara ile itiwe lami na mnajua kwenye Bajeti hii hilo halikupi shida Mheshimiwa Waziri Wa Ujenzi. Naomba ianze kwa sababu na wenyewe wameomba na hata Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya alishafika kule, ameliona. Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, ameliona.

Kwa hiyo, wote nawapongeza kwa kuwa juhudi hizi za mawasiliano ni muhimu. Hakuna maendeleo duniani pasipo mawasiliano, haiwezikani. Wewe unaenda namna gani, unataka tubebe mizigo tena kama watumwa wa miaka ile, unatembea kutoka hapa mpaka huko kwenye soko la biashara ya utumwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa la mwisho, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba hii sura ya uraia na wasio raia, Ndugu Omar Ramadhani Mapuri hebu litazame upya. Hivi ukija pale mpakani Kigoma unakuta huyu ni raia huyu si raia? Jana mimi nilikuwa naongea *A to Z*, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Naibu Waziri pale alikuwa anasema, ahsante ninaunga. Lakini ninaomba sisi ni raia. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa katika Bunge letu kwa kipindi hiki cha Mkutano wetu wa Bunge wa 14. Lakini nimefurahi kwamba nguvu za Mungu ni kubwa ameweza kujaliwa tena afya yake na kurudi katika hali yake njema na tunaamini kabisa kwamba tutaendelea kushirikiana naye, ataendelea kutusaidia vizuri katika mapambano haya ya kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunamwomba Mungu aendelee kumpa afya njema. Mimi nianze kwa kuwashangaa wale wote ambao wanaona hotuba hii haina maana na wamekuwa wakiikosoa kwa namna moja ama nyingine. Mtu atakayesema leo hii katika nchi yetu ya Tanzania kwamba hakuna kitu kilichofanyika kwa kweli hatukosei kabisa tukimfananisha na mfano ule wa Mheshimiwa Rais kwamba yuko katika kiti cha nyuma cha gari na haelewi huko mbele kuna kitu gani. Kwa hiyo, anasema tu kama vile ni mtu asiyelewa wala kutambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tukiwauliza hawa wenzetu katika mazingira ya kawaida tu wao kama akina baba katika familia zao wameshaweza kutimiza mambo yote wanayodaiwa na wake zao kule ndani? Lakini majibu yatakuwa kwamba wanawake wale watasema hawajanunuliwa bado vitenge na vitu vingine chungu mzima. Lakini bado wanavumilia na kuendelea kuwa wake zao na wakiamini kwamba hayo yote yatafanyika katika siku moja ama nyingine na baadaye. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kweli tunawashangaa sana na tunaomba ni bora waanze kujishangaa wao na maendeleo yao ndani ya familia zao kabla hawajaanza kusema vitu vya ajabu katika maendeleo haya yanayojidhihirisha katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wala sioni kwamba ni kitu kigeni kwa sababu kila kitu kinaonekana. Ukiangalia sekta zote Elimu, Sekta ya Afya, Viwanda, masuala ya Wanawake na masuala mengine chungu mzima ni mambo ambayo yako wazi na yana tofauti kubwa kabisa toka Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais wetu Benjamin Mkapa, Waziri Mkuu na viongozi wengine wote na Waheshimiwa Wabunge kazi kubwa imefanyika na maendeleo yanaonekana wazi na bila kificho kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema tuendelee mbele. Hii ndege itaruka tu na watu wapende wasipende itaruka na itaruka na itaruka kweli na itafika huko inakotaka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba tu nizingumzie kipengele kimoja ambacho kimekuwa kikiendelea kunipa hofu na wasiwasi kila siku. Tumekuwa na mabadiliko makubwa sana ya hali ya hewa katika ulimwengu mzima na mabadiliko haya ya hali ya hewa yanaenda sambamba kabisa na mpango mzima wa maendeleo na kupambana na umaskini katika nchi zote ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye kuathirika kwa nafasi kubwa na mabadiliko haya ya hali ya hewa ni nchi ambazo ni nchi maskini na Tanzania ikiwa ni mojawapo. Mabadiliko ya hali ya hewa yana athari nyingi katika kila sekta ya maendeleo kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kusababisha kutokuweza kufanikiwa katika suala zima la ukuzaji wa uchumi wetu. Kama mvua itaendelea kuwa ya matatizo ni wazi kwamba tatizo la uhaba wa chakula litaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hali ya hewa itaendelea kuwa mbaya hivyo ni wazi kabisa kwamba suala zima la kupambana na magonjwa kwa sababu ya ongezeko la joto hata nguvu zetu za kupambana na tatizo la malaria litakuwa ni la matata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya ya hali ya hewa kama itaendelea kuwa hivyo kama ilivyo masuala yote ya elimu yatakuwa ni matatizo. Sasa basi, mimi nilikuwa nafikiri kwamba pamoja na haya mambo mema na mazuri yote ambayo tumekuwa tunafanya katika Serikali yetu yanayoonekana ni budi sasa hivi tuwe na mpango yakinifu wa kuona namna gani tuna-adopt matatizo haya ya mabadiliko ya hali ya hewa tukilinganisha na nguvu zetu za kupambana na umaskini na hata tukichambua zile *millennium development goals* moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika sekta ya kilimo, tunafahamu kabisa kwamba sekta ya kilimo ndiyo ni sekta ya uti wa mgongo na ni sekta kiongozi. Na wakulima wetu wengi bado wamekuwa wakulima katika kilimo kile cha asili, kilimo cha kutumia majembe, kilimo cha kuhamahama na kilimo kisichokuwa na teknolojia sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi wa namna hiyo, tuseme asilimia kubwa ya wakulima hao ni wanawake. Mimi nilikuwa naomba sasa Taifa letu liwe na mkakati yakinifu wa kuwasaidia wakulima kulima eneo dogo kwa kilimo bora na cha kisasa kwa kutumia zana bora na za kisasa ili kupata mazao mengi na hivyo kuweza kunusulu maeneo makubwa ya ardhi yaweze kutunzwa na kusaidia kupambana na tatizo kubwa la mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutunza mazingira. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, mimi nilikuwa naomba hebu tuone katika Bajeti inayokuja tunaomba tuombe kazi kwa Mheshimiwa Rais. Sisi wanawake wa Mkoa wa Ruvuma tupewe mikoa angalau mitano tu yenye matatizo ya chakula na kila Wilaya moja iamuwe kuwa na mtoto Mkoa mmoja katika nchi yetu yenye tatizo la chakula. Tusaidiwe teknolojia ya majembe ya matrekta, mbolea na zana zote ambazo zitatusaidia kuzalisha chakula kwa wingi tukizingatia pia bila kusahau kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake wa Mkoa wa Ruvuma tunaweza kuwalisha hawa watoto wetu watano vizuri kabisa na kila mtu akawaonea wivu kwa sababu watanenepa na kunawili vizuri sana. Kwa hiyo, unaona kabisa kama tutaamua kweli kuongeza nguvu na kuweka msisitizo mkubwa katika suala la kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia za kisasa mimi nadhani pamoja na kujiletea maendeleo pia tutakuwa tumesaidia sana katika suala zima la kupambana na uharibifu wa mazingira na hivyo basi kusaidia nguvu za kidunia, nguvu katika nchi yetu ya kuzuia kasi ya ongezeko la mabadiliko ya hali ya hewa na hivyo tutakuwa tumeokoa mambo mengi kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba suala zima labda la ongezeko la tatizo la ugonjwa wa Malaria kutokana na joto kali litapungua pia tutakuwa tumesaidia kuwashirikisha wananchi katika kujiletea maendeleo kwa kuzalisha chakula cha kutosha na kukidhi hivyo basi kupunguza tatizo la njaa. Tutakuwa tumesaidia pia kuwasaidia wananchi wetu kutokana na wingi wa mazao yatakayolimwa kujisaidia kuyauza na hivyo basi kujipatia kipato na mapato ya wananchi yataongezeka na uchumi utaendelea kuwa mbele zaidi na basi kwa hali hiyo hiyo utakuta kwamba hata masuala mengine yataweza kufanyika vizuri na matatizo madogo madogo ya kifamilia ya ada na mambo mengine yanaweza yakatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi katika kuchangia hotuba hii nilikuwa naomba sana tuone kwa hakika kabisa tunawezaje tuchukulia tatizo hili la mabadiliko ya hali ya hewa tukaoanisha na mkakati wa Taifa wa kupambana na umaskini tukalinganisha na *millennium development goals* moja baada ya nyingine inajihusisha vipi katika kuleta maendeleo na kupambana na tatizo hili ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendeleo kuwashukuru Mawaziri wetu kwa kazi kubwa wanazozifanya. Wao kama binadamu wamekuwa na kazi kubwa na nyingi. Lakini kwa kweli tumekuwa tukienda nao sambamba. Tumekuwa tukishauriana na tumekuwa tukifanikiwa sana katika safari yetu hii ndefu ya kujiletea maendeleo. Nilikuwa naomba nitoe ombi maalum ambalo litatusaidia tena sana sisi wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tukisubiri ujenzi wa daraja katika kijiji cha Muhukuru likituunganisha na nchi ya Msumbiji. Kwa kuwa mipango ya Wizara ya Ujenzi imekuwa ikiangalia kwamba ujenzi huo wa daraja labda umekuwa na matatizo ya namna moja ama nyingine, sisi tulikuwa tunaomba tu hata kama kuna daraja la chuma limehamishwa mahali na likajengwa lingine tuletewe hilo kwa muda liweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa daraja hilo katika mto Ruvuma kijiji cha Muhukuru utatusaidia sana. Wakulima wetu wengi wameanza kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo. Wanazalisha mpunga kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, basi ujenzi wa daraja hilo ungeweza kusaidia licha ya kuwalisha wenzetu katika nchi yetu basi wangeweza kupata biashara na nchi jirani ya Msumbiji na kujipatia mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo mengine ambayo mimi leo niombe ni kuiomba sana Wizara ya Ujenzi iangalie uwezekano wa kujengwa kwa daraja hilo kusaidia maendeleo ya Mkoa wetu. Naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi angalau nichangie baadhi ya haya niliyokuwa nayo. Mengine nimekwishachangia kwa maandishi lakini nikaona yako mengine muhimu mawili ambayo itabidi niyazungumze kwa ufupi kabisa.

Kwanza na mimi nataka niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri. Lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu ya ufafanuzi alioutoa kabla ya kuzungumzia hoja yenyewe hii na pia niwapongeze Waheshimiwa Viongozi wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, hasa Mawaziri,

Makatibu Wakuu na watumishi wengine katika Mikoa na Wilaya, wanajitahidi sana kutekeleza hii Sera ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa anaizungumzia. (*Makofi*)

Nitaanza kuchangia hasa katika hotuba yake ya utangulizi ambapo Mheshimiwa Rais anaanza kusema hivi, iko katika ukurasa wa pili. Anasema kwa kuanzia ninanukuu: “Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kurejea kwenye muhtasari nilioutoa kuhusu sura kuu ya mwelekeo wa miezi 20 ijayo,” katika mwelekeo huo Mheshimiwa Rais ametoa sehemu kubwa tano. Ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne mpaka ya tano. Mimi nitazungumzia sehemu mbili kubwa.

Ya kwanza, anasema kwanza ni kuongeza kasi ya kubadili mtazamo wa watumishi wa umma kwenye Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ili wajue kuwa kazi yao ya msingi sasa ni kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiendeleza. Hilo la kwanza. Nalisema hilo kwa sababu tutake tusitake, Rais ametambua kwamba kasi ya kubadili mtazamo wa watumishi wetu bado iko nyuma sana na hii inaweza ikawa kuwa kweli inatokana na fikra za zamani ambazo tumekuwa nazo kwa kipindi kirefu.

Lakini pia ni kutokana na itikadi mbalimbali ambazo tumekuwa nazo miongoni mwa watumishi tuliokuwa nao. Rais anapozungumzia hiyo ametambua ya kwamba bado miezi 20 kasi bado hajaridhika nayo ya kwamba ili tuweze kupaa lazima tuongeze kasi kidogo na hili ni jukumu la kila mmoja pamoja na Waheshimiwa Wabunge tumepewa jukumu hilo ambalo lazima tumsaidie Mheshimiwa Rais kutekeleza hayo ambayo amekuwa akiyafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo liko wapi? Je, kweli tuna uhakika ya kwamba watumishi wote tuliokuwa nao wako pamoja nasi katika kutetea sera za CCM? Je, tuna uhakika viongozi wote mpaka kule katika Serikali za Mitaa wako pamoja nasi? Nalisema hilo kwa sababu chama chochote kinapoingia madarakani kazi yake ya kwanza kabisa kinaandaa watu watakaosimamia sera hizo. Je, kazi hiyo tuliifanya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana utakuta wakati mwingine baadhi ya viongozi ambao tuliwajua wakati wa kampeni walitupinga moja kwa moja, lakini Chama Cha Mapinduzi hakikuchukua hatua yoyote ya kuwaadhibu au kuwaondoa katika madaraka, bado inaendelea kuwa nao ndiyo maana nasema Chama Cha Mapinduzi ni mfano wa vyama vingi ambao kwa kweli lazima tuiige. Ingekuwa wenzetu wamechukua madaraka upande wa *Opposition* sijui kama wengine tungebaki hapa. Wangihakikisha wanang’oa watu wote hao ili waingize watu ambao wanajua wanasimama pamoja nao na wengine kama akina Kimiti sijui kama tungekuwa tunasimama ndani ya Bunge na akina Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, wangehakikisha hawa hawaonekani. Kwa sababu lazima uwe na uhakika ya kwamba watu wanaosimamia sera zako ni wale ambao mmekubaliana nao.

Lakini Chama Cha Mapinduzi kimekuwa kikijenga misingi ile ile ya heshima, uhuru, usawa, demokrasia. Ndiyo maana hata viongozi wa Upinzani wamepewa madaraka. Mimi nasema ni mfano mzuri wa kuigwa ili viongozi wajue chama hiki kiko pamoja nao. (*Makofi*)

La pili ni suala zima ambalo nadhani lazima tulielewe. Sura ya pili ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Rais ni kwamba katika kifungu cha tano, anasema lazima kuendelea kubainisha kero za wananchi na kuondoa vikwazo vilivyo katika njia ya Watanzania walio tayari kujiendeleza. Pia inazungumzia haki za wanyonge wakiwemo wananchi waliomo katika Sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Rais anapoizungumzia hiyo, anataka kasi iongezeke kuwasaidia wananchi katika maeneo yetu na nadhani wasaidizi wakuu ambao wako katika Mikoa na Wilaya. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya lazima wachukue *lead* ya kuhakikisha ya kwamba kero hizi za wananchi zinapunguka katika kipindi hiki. Ndiyo maana nataka nitumie nafasi hii mimi kwa kusema kwa wazi ya kwamba lazima niwapongeze badhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanafanya kazi zao nzuri sana katika kumsaidia Mheshimiwa Rais ili kuhakikisha anatekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Wakuu wa Mikoa ambao kwa kweli wanatakiwa kurekebisha tabia ni wale ambao kwa kweli wanaweza kuwa hawaendeshi shughuli zao kufuatana na misingi ambayo

tumekubaliana nayo. Kazi ya Mkuu wa Mkoa nataka nikubaliane pia na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ya kwamba wakati mwingine inaweza kuwa kwamba huoni umuhimu wa Mkuu wa Mkoa.

Mimi nimekuwa kiongozi kwa zaidi ya miaka 10 kama Mkuu wa Mkoa, najua umuhimu wa Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa mahali anapofanya kazi yake vizuri utakuta kuna amani, kuna utulivu na maendeleo ya wananchi katika eneo hilo yanakwenda vizuri sana. Hivyo kwa kweli anakuwa ni kiungo kizuri sana kati ya viongozi wakuu wa Serikali na pia wananchi katika maeneo hayo. Hivyo Mkuu wa Mkoa wakati mwingine anaweza kuwa ni kero kwa sababu labda hawaelewani au amejilingiza naye katika vikundi na amekuwa ni sehemu ya kukorofisha watu katika maeneo hayo, ama sivyo kazi yake akiifanya vizuri anaweza kuwa ni kiungo kikubwa sana cha kuleta maendeleo katika eneo hilo.

Mimi nadhani suala lisiwe ni jina. Suala liwe ni kwamba majukumu yake ni yapi ambayo tumeyaweka. Mimi nadhani ni vizuri tukaliangalia katika misingi ya kazi nzuri ambayo wanaifanya na mimi nina imani kabisa katika kipindi hiki sasa kasi ya kuendelea kuwatetea wananchi katika maeneo hayo ndiyo Mheshimiwa Rais anawaomba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya waendeleo kumsaidia ili tuweze kupaa wote pamoja si kwamba tunapopaa kwenye ndege wengine watabaki. Tunapopaa tunataka tupae wote pamoja na kazi hiyo itafanyika kwa kuhakikisha wote tunafanikiwa katika malengo hayo. *(Makofi)*

Lakini pia nataka niwaambie kitu kimoja, Wakuu wa Mikoa ni binadamu kama sisi, kama kuna matatizo katika sehemu fulani basi ni tatizo kati ya Mkuu wa Mkoa na mtu fulani na wakati mwingine huwa ni makundi ndiyo yanatufikisha hapo na makundi yanapokuwepo ndiyo maana inakuwa ni vigumu sana kuweza kutawala. Binadamu mahali popote ni rahisi kumtawala kama unajua namna ya kutawala. Binadamu anaweza kuwa mkorofi na mgumu kutawaliwa kama hujui namna ya kumtawala na wakati mwingine anapona anakosa haki zake, anakosa uhuru, anaona kuna upendeleo, binadamu anakuwa ni mgumu sana kuweza kumtawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba tunawatendea haki watu wetu na kipindi hiki cha kugawa chakula cha njaa lazima viongozi tuwe waangalifu sana. Tunaweza kukorofishana na wananchi wetu kwa sababu ya upendeleo. Lakini pia kwa ajili ya tabia ya baadhi ya viongozi kutaka kujilimbikizia chakula hicho wakitumie wao wenyewe badala watu walioathirika. *(Makofi)*

Hiyo ni kazi mojawapo Waheshimiwa Wabunge na sisi wote tulio hapa tusimamie ili kuhakikisha kero za wananchi na hasa kipindi hiki tuziangalia katika misingi ya kuona hakuna upendeleo wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani haya nimesema tu kwa ufupi kwa sababu mengine nimekwishayaweka kwa maandishi lakini naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais na nina imani kabisa itaungwa mkono na Wabunge wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KINGUNGE NGOMBALE-MWIRU:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nataka niungane na wenzangu kuunga mkono hoja hii ya hotuba ya Rais mia kwa mia. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ningependa nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache kulingana na muda ambao tunao. Ningependa vile vile kuwapongeza wenzetu Waheshimiwa Wabunge tuliowachagua kwenda kwenye Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba ambaye tumempeleka SADC na kumpongeza kijana wetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuwa Mbunge. Hotuba ya Rais imepewa sifa kemkem ndani ya Bunge na vile vile nje ya Bunge na mimi ningependa kusema kwamba Rais anastahili sifa hizo na pongezi hizo na pamoja wenzangu wametoa sifa aina mbalimbali ningependa na mimi niseme kwa ufupi tu.

Hotuba ya Rais inajitambulisha kwa mambo yafuatayo:-

Moja, hotuba hii ina uchambuzi wa hali ya juu. Pili, hotuba hii imejengeka kwa nguvu za hoja. Tatu, hotuba ina takwimu za uhakika, siyo takwimu nyingine tunazoletewa hapa na baadhi ya Wabunge

wachache. Yaliyoandikwa kwenye makala ni takwimu nyingine lakini sisi wanatutumia nyingine. Katika hotuba ya Rais takwimu pale ni za uhakika kabisa.

Nne, hotuba ni yenye ufasaha wa kuigwa mfano, ni fasaha kabisa na katika masuala haya ya mawasiliano suala la *clarity*, suala la ufasaha ni jambo la msingi. Tano, hotuba hii ni ya Kiswahili na Kiswahili safi. Wakati mwingine hata sisi viongozi wengi tunalichukulia suala la Kiswahili kijuu juu tu. Kwa sababu mkiwa na lugha yenu ya Taifa lazima muitumie kwa mujibu wa Kanuni zake za lugha hiyo na Mheshimiwa Rais Mkapu ametia fora katika hilo. (*Makofi*)

Lakini la mwisho sifa ya hotuba hii ni kwamba ni hotuba inayotia matumaini kwa Watanzania. Mafaniko yaliyopatikana chini ya uongozi wake kwa kushirikiana na timu yake ya Serikalini na timu yake akiwa Mwenyekiti wa Chama kwa upande wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ni mafanikio makubwa na yanaonyesha kwamba tukishikamana vizuri chini ya uongozi ulio safi tunaweza kufanya mambo makubwa zaidi. Kwa hiyo, ni hotuba inayotia matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuendelea kusifu na kusifu lakini nadhani lililo kubwa ni kwamba tujiulize tu hivi baada ya hotuba hii tunafanya nini? Kama wengi walivyosema hotuba hii ni changamoto kubwa kwetu sisi sote. Sote katika makundi makubwa mawili, kwanza kwa wananchi wenyewe, lakini pili kwa upande wa Serikali, kwa upande wa uongozi wa jumla kwa upande vile vile wa Chama Tawala.

Kwa upande wa wananchi, Mheshimiwa Rais ametuambia kwamba kwa kumkariri Mheshimiwa Rais Mstaafu Marehemu Mzee Julius Kambarage Nyerere, alituambia huko nyumba kwamba wakati wenzetu wanatembea, sisi tukimbie. Yeye ameonyesha katika kipindi hiki cha miaka minane mpaka sasa kwamba inawezekana. Tutaenda kwa kasi kuliko ambavyo tulivyokwenda huko nyuma. Lakini kasi hiyo haitoshi, uchumi wetu sasa hivi kwa asilimia 6.2.

Ukuaji huo hautoshi lazima tufike angalau kwenye asilimia nane na kwenda mbele zaidi. Sasa maadam tumeona kwamba kazi imefanyika changamoto kubwa kwa wananchi ni kwamba sasa kazi ni kwao na kazi yenyewe ina sura mbili. Kwanza lazima wananchi wote wenye uwezo wa kufanya kazi wachape kazi. (*Makofi*)

Tuondokane na fikra kwamba unaweza ukaishi kwa kumtegemea baba, mjomba, shangazi ama kwa kubabaisha. Hilo la kwanza. Lazima tuishi kwa kufanya kazi wote. Tuna watu wazima wenye uwezo wa kufanya kazi nchini zaidi ya milioni 15 kwa idadi yetu ya watu milioni 35. Wote tukifanya kazi nchi yetu itakimbia. (*Makofi*)

Lakini siyo tu tufanye kazi, lazima tufanye kazi kwa maarifa. Jambo la pili. Lazima tutumie maarifa katika kufanya kazi. Bado tuko nyuma katika kutumia maarifa. Kilio chetu bado kiko nyuma na sababu kubwa ni kwamba hatutumii maarifa ya kutosha. Hilo ni kwa wananchi. Lakini kwa upande wa Serikali sasa lazima Serikali la kwanza iunde mazingira. Itawawezesha wananchi walazimike kufanya kazi na wafanye kazi kwa maarifa. (*Makofi*)

Lazima Serikali iunde mazingira ili watu wafanye kazi. Pili, Serikali tufanye utaratibu wa kueneza elimu ya watu wazima yenye manufaa, *Functional Adult Education* maarifa ya kilimo, ya ufugaji, ya uvuvi, tuweke utaratibu wa elimu ya watu wazima, nchi nzima. Mafanikio ya mikoa ile inaitwa *Big Four*.

Mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati ule. Kazi kubwa tumefanya ni kuwafundisha wananchi kanuni za kilimo bora. Lazima turudi hapo. Pili, lazima vile vile Serikali iweke utaratibu mzuri na mtandao wa kufikisha pembejeo karibu na wananchi. (*Makofi*)

Tusitoe visingizio vya kwamba sasa hivi ni uchumi wa soko, ni shauri ya wafanyabiashara binafsi, hapana. Lazima tuunde mazingira, pembejeo ziwakaribie wananchi, halafu tuwaachie wao wafanye kazi. La tatu, kwa kweli lazima Serikali iweke malengo ya kueneza vitendea kazi vya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke malengo hivi tutaingia katika kilimo cha ng'ombe nchi nzima baada ya miaka mingapi? Hivi tutaeneza mikokoteni ili kuwakomboa hasa wanawake kubeba mizigo kichwani kueneza nchi nzima baada ya miaka mingapi? Hatuwezi tukasema sisi hivi tunangoja magari hatutengenezi magari hapa, lazima tufanye kile tunachokiweza. *(Makofi)*

Mwisho Chama Tawala. Chama Tawala kina wajibu mkubwa sana na ni vizuri kukumbushana kwamba chenyewe ndio chenye Sera, Ilani kwa hiyo, lazima kuhakikisha kwamba sisi wana CCM, viongozi na wanachama wenyewe ndio tunakuwa watekelezaji wa mfano. Kama ni suala la kufanya kazi kwa juhudi na maarifa sisi tujitokeze kuwa mstari wa mbele halafu wengine watuige sisi. Tunao udhaifu kidogo katika hili. Bado tuna watu ambao pamoja na kwamba ni viongozi wa Chama cha Mapainduzi, pamoja na kwamba ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi lakini hawako mstari wa mbele katika kutekeleza na kutetea Sera za Chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami nishiriki kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia mwaka huu wa 2004 katika Bunge letu Tukufu, naomba nianze kwa kutoa salaam za kheri ya mwaka mpya kwako Mheshimiwa Naibu Spika na kupitia kwako salaam kwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Waheshimiwa Watumishi wa Bunge, watumishi wa Serikali wanaotusaidia katika kutekeleza majukumu yetu hapa Bungeni na Waandishi wa Habari. Kheri ya mwaka mpya wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kumpa pole Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba na Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa maradhi yaliyomsibu kwa muda mrefu tukawa hatunaye ndani ya ukumbi huu wa Bunge lakini Mwenyezi Mungu amemjalilia amerejea Bungeni na tunamwomba Mwenyezi Mungu amponeshe haraka maradhi yanayomsibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Wabunge wa Afrika wanaotuwakilisha sisi kwa ushindi wao wa kishindo, sikushiriki katika kupiga kura lakini nawaunga mkono. Vile vile mwakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*, Mheshimiwa Sophia Simba. *(Makofi)*

Pia natoa pongezi za dhati kabisa kwa mjukuu wangu Mheshimiwa Charles Makongoro Kambarage Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Asha Ngede kwa kuchaguliwa kuwa mwakilishi wetu katika Tume ya Huduma za Bunge. Kura ilikuwa ya siri lakini inaonyesha dhahiri tulijali usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye mjadala wa hotuba. Nimeshampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini nataka kusema kwa kweli sifa zilizotolewa kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais kama Waheshimiwa Wabunge naweza kusema zaidi ya 99% wamekiri ilikuwa hotuba nzuri sana, yenye kutoa matumaini na ambayo imejengea heshima Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake wa Ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo ninaanza nalo ni kuomba vyombo vya habari visiishie katika maneno ambayo Mheshimiwa Rais aliweza kupata muda wa kuyasoma mbele ya Bunge hili. Kwa vile wanaweza kuandika maandike mpaka hata viambatisho. Viambatisho vina maneno mengi mazito sana ambayo yanasaidia kutafsiri mafanikio makubwa ambayo kwa ufynywa wa muda Mheshimiwa Rais hakuweza kusema kila jambo. Amezungumzia mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapiga kura wangu wa Jimbo la Muleba Kusini wamenipigia simu wanasema Wapinzani wanasema barabara ya kutoka Kagoma - Muleba - Rusahunga imefutwa. Kwenye kiambatisho ukurasa wa 94 imeelezwa zabuni za kutengeneza barabara hiyo katika kukamilisha barabara

kuu kutoka Dar es Salaam - Mutukula zinatangazwa Februari, 2004. Huo ni mfano tu wa kuonyesha jinsi ambavyo viambatisho vina maneno mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizingumzie njaa, Mheshimiwa Rais ametuambia tuna fedha za kutosha na tuna imani au tunasifika na wahisani wetu katika jitihada za kuhakikisha chakula kinafika pembe zote za nchi. Nawapa pole wote walioathirika na njaa ikiwa pamoja na wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini. Muleba mvua inanyesha lakini mihogo imeharibika kutokana na maradhi na huko kuna njaa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, tuwahimize Wakuu wa Mikoa na Wilaya washiriki kikamilifu kuleta takwimu sahihi. Rais ameonya kuhusu viongozi waoga. Wawe wajasiri kukiri kuna njaa na kusaidia kupeleka chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Rais kuwapongeza *TRA*. Fedha zinapatikana na tunazitamka hadharani. Serikali ya uwazi. Kwa kweli mimi nilikuwa nashangaa nilipokuwa nasikia Waheshimiwa Wabunge kadhaa humu ndani ya Bunge na viongozi wa kisiasa nje ya Bunge kwamba Mheshimiwa Rais kakwepa kuzungumzia rushwa. Kwa kweli hawamtendei haki Mheshimiwa Rais kutafsiri kwamba kwa kutotumia neno rushwa katika hotuba yake anasema rushwa imekwisha na Tanzania haina tatizo la rushwa. Ukifuatilia hotuba yake mambo ambayo ameeleza, sura tano za mwelekeo miezi 20 iliyobaki, ukurasa wa tatu, la tano ni kupambana au kuendelea kubaini kero za wananchi na kuondoa vikwazo kwa wananchi kujiendeleza. Kero za wananchi ni pamoja na rushwa. Mheshimiwa Rais hawezi kuorodhesha kero zote za wananchi kwenye hotuba. Kitabu hiki kitalingana na sanduku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa kwamba *PCB* sasa hivi ni watafiti tu hawapambani na rushwa hiyo si sahihi. Vijana hawa wa *PCB* wanapambana na rushwa kwa nguvu zote. Wanastahili pongezi na kutiwa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zote zinaonyesha dhahiri Mikoani na Wilayani. *PCB* inayozungumzwa sasa imejengwa na kuimarishwa kwa msaada wa Bunge hili na ndio maana Mheshimiwa Rais anatoa shukrani za dhiti kwa Bunge kama mdau ambaye anamsaidia sana kuimarisha Utawala Bora. Mheshimiwa Rais alichagua kutumia maneno Utawala Bora katika hotuba yake na sio rushwa kwa sababu ukizungumzia rushwa tu ni kueleza kwa ufyny masuala ambayo yanawasibu wananchi wake. Naamini wananchi wanamuelewa Rais wao anapambana na rushwa. Naye anajua bado rushwa ipo na anaikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *PCB* wanaelekea hadi Wilayani. Wakati tunaingia madarakani Awamu ya Tatu, *PCB* walikuwa kwenye Kanda wakihudumia wastani wa Mikoa minne. Sasa wako Mikoa yote. Wamefungua ofisi Wilaya 47. Mwisho wa mwaka huu Wilaya zote zitakuwa na vijana wa *PCB*. Hii naieleza kwa maana kwamba watasaidia sana *PCB* kukabiliana na matatizo ya rushwa hata rushwa za kisiasa iwapo watapewa ushirikiano na wanasiasa wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba *PCB* iondolewe Ofisi ya Rais imenishangaza kabisa baada ya Rais kupewa sifa nzito na kemkem kwamba ni muadilifu na mpambanaji wa rushwa. Kweli haaminiki kusimamia *PCB*? Lakini pendekezo ipelekwe wapi *PCB* hatujalisikia. Nchi nyingi vyombo kama hivi vinakuwa katika ofisi kuu yenye uwezo wa kusimamia ambayo ofisi kuu hiyo inawajibika kwa Bunge. Kwa hiyo, sifungi mjadala wa *PCB* ipelekwe wapi. Lakini hata *PCB* wanashangaa wapelekwe wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwita *General Kamazima* na timu yake waje wasikilize mjadala labda tutaondoka na kazi ya kufanya ya kuchunguza kesi madhubuti, mahsusi. Niliposikia ya Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, analalamika ndege ya Serikali ununuzi wake una udanganyifu, nikasema kazi imepatikana. Tulipofuatilia nikakuta ni tatizo la Kiingereza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaendelea kusikiliza. Sijatoka ndani ya ukumbi huu. Nasikiliza tuhuma mahsusi tufuatilie. Maana yake utafiti na uchunguzi ni jambo la msingi, ama sivyo tutamalizia watoto wa watu ndani ya jela eti watu watusikie tuko kazini. Mheshimiwa Isaac Cheyo, akasimama na hoja kwamba CCM imenunua Madiwani wake milioni tatu, tatu. Nikasema kazi imepatikana watu watahughulikiwa. Walipomwambia athibitisha akasema naomba kufuta usemi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni Bungeni ambapo tunapaswa kuzungumza bila woga. Kutaja hata Masilingi anakula rushwa nikashughulikiwa. Sasa hata watani zangu wanasema Rais wasaidizi wake hawamsaidii. Akina nani? Masilingi au nani? Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ni kuanzia Makamu wa Rais mpaka Mwenyekiti wa Serikali wa Kijiji na Afisa Mtendaji wa Kijiji. Nani hamsaidii kupambana na rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watakaolingia Ikulu tukitoka 2005. Nadhani nitaendelea nimalizie kipindi changu, nawashauri waheshimu uchunguzi na utafiti katika masuala mazito yanayohusu jinai. Ukifunga watoto wa watu miaka mitano na kuendelea ufurahishe mtu, ni dhambi. Halafu himizeni watoto wa watu wajenge nyumba na kulima. Mnaanza kuwatisha watoto ooh, ana mshahara mdogo amejenga, sasa tukae kwenye vibanda ndio tunaonekane ni waadilifu? Watumishi wa Serikali jengeni, jengeni Wabunge, posho hata kama ni ndogo utaeleza hela umezipata wapi lakini kwa Wabunge posho inatoshwa kujenga nyumba, huo ndio ukweli. Ukibana ukafanya *savings* utajenga na majengo yamejengwa Dodoma na vijijini.

Sasa watumishi walioko Serikalini tunasema ni waadilifu mpaka watakapothibitishwa vinginevyo. Wasitishike, chapeni kazi, Utawala Bora umedhihirisha. Serikali inakusanya hela inatamka. Barabara tunajenga. Je, tukikaa kwenye *cabinet* tukagawana fedha za *TRA* hizi tulizowatangazia tukawaambia wamekusanya kidogo wananchi watajuaje? Ndivyo Serikali isiyozingatia Utawala Bora zinavyoiba. Wanakaa wanagawana. Sisi tunasema hadharani. Tunaweka kwenye mitandao ya dunia nzima makusanyo yetu, matumizi yetu na kama kuna ubadhilifu na wizi tunaambizana tunashughulikiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kijana *DCI* amesema Morogoro akitafsiri *grand corruption* na *petty corruption* yaani rushwa kubwa na ndogo wakasema amesema yao ni ndogo ya wakubwa ndio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliitisha hotuba kwa sababu hatutaki viongozi hasa watendaji wa Serikali wanaogeza vita dhidi ya rushwa kama usanii, aiseme rushwa zaidi waseme yeye ni mwadilifu, huo ni unafiki. Ripoti yake ninayo yeye alieleza tangu mwaka 1995 Askari 1,138 wamefukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema maneno machache rushwa ndogo na kubwa bado zipo lakini hii haina maana kwamba zipo Tanzania tu ni dunia nzima. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kupongeza hotuba nzuri na yenye dira na mwelekeo mzuri wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuchangia hotuba hii katika upande wa ukame. Ningependa kutoa mapendekezo yangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, tuimarishwe kilimo cha umwagiliaji katika sehemu ambazo kinawezekana kama vile Wilaya ya Kilolo, Kata ya Mahenge. Ni kitu cha ajabu sana kuacha maji yanapotea bure.

Pili, baadhi ya sehemu mvua hazinyeshi kwa sababu sehemu hizo zimegeuzwa jangwa. Hivyo Serikali iweke kipaumbele katika upandaji wa miti na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Tatu, kwa kuwa sehemu nyingi katika Wilaya wanafunzi hupata mlo wa mchana shuleni. Napendekeza shule zote zinazotoa mlo wa mchana wapewe chakula cha msaada bure ili watoto waweze kuzingatia masomo.

Nne, ujenzi wa barabara uimarishwe zaidi katika sehemu ambazo zina mazao ya kutosha mfano, Kilolo. Endapo barabara za Wilaya ya Kilolo zitaimarishwa hakuna sababu ya kuomba chakula nje.

Tano, katika Mkoa wetu wa Iringa, katika Wilaya ya Kilolo kulikuwa na mkulima mmoja ambaye alikuwa na uwezo wa kulima na kulisha chakula zaidi ya Mkoa mmoja. Kwa kuwa mkulima

huyo yupo, ningeomba Serikali itume ujumbe ili aweze kusaidiwa na kupewa moyo anaweza kutusaidia kulisha chakula zaidi ya Mikoa mitano. Hivyo suala la kuomba chakula litakuwa halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la uvunaji wa maji lizingatiwe kwani hivi sasa maji yanaendelea kupungua duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba yote kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa kwa kuwapongeza wale wote waliochukua fomu kwa kugombea Ubunge wa Afrika kwa kuonyesha uwezo wao na pia kutumia demokrasia, lakini nawapongeza wale wote walioshinda Mungu awape nguvu na uwezo mkubwa wa kwenda kutuwakilisha vizuri. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kwenda kutuwakilisha kwenye *SADC Parliamentary Forum*, Mungu ampe uwezo mkubwa. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mradi wa *TASAF*, kwa kweli Jimbo langu limefaidika sana na mradi kwa kupata Vituo vya Afya na nyumba za Madaktari. Kwa kweli wametusaidia sana katika kuondoa tatizo hili kwa wananchi wetu, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais haina ulazima wa kuichangia sana ulazima ni utekelezaji. Isipokuwa namuomba Mheshimiwa Rais hali itakapokuwa nzuri zaidi basi afanye ziara yake ya makusudi ya kututembelea kwenye Majimbo yote ili apate kuona namna ya mageuzi kama alivyoyazungumzia kwamba ni mageuzi ya kimaendeleo na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi kwa kumpa pole Mheshimiwa Rais kwa maumivu makubwa aliyoyapata na namwombea dua Mwenyezi Mungu amwondolee maradhi hayo na ampe afya nzuri aweze kuendelea kutuongoza mpaka atakapomaliza muda wake na awe nasi bega kwa bega ili kulipeleka mbele gurudumu letu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa sababu ina ukweli na uwazi, kwa wale waliokuwa na masikio wameisikia kwa sababu inaweka wazi mambo yote ya Taifa letu zima, tukiacha wale waliozoea kumpinga kila kitu ikiwa kizuri au kibaya kwao ni kupinga. Kilichobakia sasa ni utekelezaji wa kuifanyia kazi na kufuata dira ya utekelezaji ya kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wale wote waliojitokeza kugombea nafasi za uwakilishi katika Bunge la Afrika kwa kuonyesha uwezo wao na pia kuamini demokrasia, lakini zaidi niwapongeze wale walioshinda na kuamini kwamba watatuwakilisha vyema na kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge, naanimi atalitumikia Bunge kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Rais kwa maumivu aliyoyapata na namwomba aamini kwamba maradhi aliyopata amepewa na Mwenyezi Mungu, hivyo ni yeye pia ndiye atakayeyaondoa haraka sana kwa uwezo wake. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais kimsingi tumepewa nafasi ya kuichambua kwa undani zaidi, sawa, lakini mimi binafsi nahisi hotuba hii imekamilika kinachotakiwa ni



kuifanya kuwa dira katika utekelezaji wa Iani ya Uchaguzi, na katika mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea kwa kasi katika dunia hii ya utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi hivyo ni Mwenyekiti miongoni mwa Wenyeviti wa Vyama vya Siasa. Ni dhahiri kama ni kipimo ameonyesha uwezo mkubwa wa kifalsafa miongoni mwao. Walikiri kwa kupiga makofi alipokuwa akihutubia kuonyesha kuisimka kwa ukweli wa mambo aliyokuwa akiyaeleza, lakini baadaye walianza kubeza kwa kutoa kasoro hii na ile, mimi ninavyofahamu Mheshimiwa Rais sio malaika kwamba atakapotoa hotuba basi imalize kila kitu. Lah!

Kwa mfano, walisema hakuzungumzia rushwa na kadhalika. Kama ni kasoro mbona na wao hawakuzungumzia zote pale alipozungumzia suala la ujambazi, ukimbizi, malezi ya yatima wa Ukimwi, barabara za juu kwa juu za magari, vifo vya watoto kupitia malaria na kadhalika. Mimi binafsi kama atakachokifanya binadamu, atafanya kadri ya uwezo wake aliyojaaliwa kwa wakati ule na kilichokamilika na ambacho hakina kasoro ni Biblia na *Quran* Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwombea afya njema Mheshimiwa Rais na Mungu amzidishie uwezo wa ziada ili atekeleze jukumu kubwa alionalo la kuongoza Watanzania na ulimwengu kwa jumla. Namalizia kwa kumnukuu Marehemu Baba wa Taifa kwa kusema: “Kazi ya Urais si ya kuomba ila ni ya majaaliwa kutokana na ulazima wa mmoja wetu awe Rais.” Naomba Mungu atujalie tumpate Rais wa kheri na mwenye uwezo mkubwa mwaka 2005. *Amin.*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya tarehe 12 Februari, 2004 ambayo Mheshimiwa Spika, aliita *authoritative, comprehensive and inspiring*. Mimi zaidi ya hayo ninaongeza neno *moving*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeze Serikali yote chini ya uongozi wa uhakika wa Mheshimiwa Rais kwa maendeleo makubwa ambayo nchi yetu inayapata hivi sasa. Ninamtakia kila la kheri kwa muda wa miezi 20 iliyobaki ili aweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo rahisi cha kupima maendeleo ya nchi ni kuangalia hali ya elimu, afya, barabara, na miundombinu na nishati hasa umeme. Hakika Serikali yetu yote hayo inayatia mkazo mkubwa na ndio ushahidi tosha kwamba Serikali imepania kutuletea maendeleo katika nyanja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba ni dhahiri kabisa kwamba maendeleo yanayoonekana zaidi katika maeneo fulani ya nchi kuliko maeneo mengine au Mkoa mingine. Mkoani Kigoma kwa mfano, hakuna umeme, hakuna barabara nzuri, huduma za afya ni duni na ni eneo ambalo hali ya ulinzi na usalama ni mbaya kutokana na wakimbizi toka Burundi na Kongo.

Mkoa huu umewekwa kwenye mpango wa *EPZ* ingawa hauna umeme. *EPZ* itafanikiwaje bila umeme? Kuna mpango gani wa kupeleka umeme Kigoma ili wananchi wa Mkoa huo nao waweze kushiriki katika kuongeza Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa zaidi. Ni lini barabara za Kigoma hadi Mwanza - Bukoba na Kigoma hadi Tabora zitawekwa lami ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao kwenye masoko ya uhakika na kufaidika kutokana na biashara na nchi za jirani za Kongo, Burundi, Rwanda na Zambia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma kwa miaka kadhaa sasa umepokea wimbi la wakimbizi toka Burundi na Kongo. Je, Mkoa huu unafidiwa vipi na Jumuiya ya Kimataifa na Taifa letu kwa kubeba mzigo huo mkubwa? Ni vyema, Seriakli ingechukua hatua za makusudi kuelekeza nguvu zake Mkoani Kigoma kwa lengo la kuuinua kiuchumi na kijamii. Ninamtakia afya njema na ahueni ya haraka Mheshimiwa Rais. Ahsante.

**MHE. FATMA SAID ALI MCHUMO:** Mheshimiwa Naibu Spika naunga mkono hoja hii. Kuhusu rushwa Waheshimiwa Wabunge wengi wanapiga kelele na rushwa Serikalini na kwa viongozi mbalimbali. Ushauri iundwe kamati ndogo ya Waheshimiwa Wabunge watoe mawazo yao namna ya kuondoa rushwa nchini kwetu.

Kuhusu Muungano naomba Serikali zetu mbili ziainishe maeneo mapya ya uchumi ambayo hayapo kwenye Wizara ya Muungano zifanyiwe miradi maalum kwa mfano MEM kwa Wizara ya Elimu Zanzibar. Kuhusu Nishati uwepo mradi wa pamoja ili tuondakane na tatizo la TANESCO. Ujenzi, barabara ziwepo zinazofadhiliwa na Muungano na Mawasiliano, usafiri majini na vijijini, uwepo mradi wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu huu utasaidia Zanzibar tuweze kupaa kwa pamoja na wananchi wa Tanzania Bara au tutabakia kutembea tu na kupunga mkono wetu hapo Zanzibar.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa hongera kwa hotuba nzuri Mheshimiwa Rais. Naahidi kuiunga mkono kwa uwezo wangu, sisi wote tunachotaka ni maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba ni mazingira sahihi ya kufanya kazi, msiwe na hofu na mimi, yote nafanya kwa ajili ya Watanzania wenzangu, kama mtanikubalia na kunipa nyenzo, naamini ninaweza kufanya vitu muhimu vitakavyomfanya Mtanzania kutembea kifua mbele, kwa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msinihofie.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni ya kueleza mfanikio na kutoa maelekezo bora ya hatua za kuchukua katika kipindi kilichobakia kabla ya uchaguzi. Nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais kwa kazi yake nzuri aliyofanya na anayoendelea kuifanya ya kuboresha uchumi wa nchi hii. Asiyeona ni yule aliyekaa kiti cha nyuma. Mheshimiwa Rais ameuona umuhimu wa wanawake katika ujenzi wa Taifa hili na ameahidi kutoa nafasi zaidi kwao. Naamini watendaji hao watauona umuhimu huo katika nafasi zao. Kama Naibu Waziri naahidi kusonga mbele katika shughuli za Wizara katika kuboresha Mawasiliano na Uchukuzi na tutaendelea kutekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi. Mawasiliano na Uchukuzi ni chachu ya ukuaji wa sekta zingine. Bila Mawasiliano na Uchukuzi hakuna Wizara inayoweza kupiga hatua. Hivyo wakati umefika wa kuona umuhimu wake ili nayo iwe katika *priority list*. Yapo ambayo wenzetu wa Wizara ya Fedha wangelisaidia Wizara hiyo:-

- Sasa wakati umefika wa kutoa *priority* kwa shughuli za Wizara hii ili ziweze kuchangia vyema katika uchumi wetu.
- Reli inahitaji isaidiwe kifedha itengenezwe, iboreshwe ili ibebe mizigo mizito na kuipunguzia barabara. Reli ikiboreshwa vyema barabara zitadumu.
- Magati yetu yote yana hali ngumu. Hili tukitaka kuliondoa na kuwaondolea umaskini wananchi wetu wanaoishi na wanaotegemea usafiri wa bahari na maziwa njia bora ni kuwaboresha magati yao na *excess roads* ziendazo katika gati, kwa njia hii tutaweza kufungua maeneo yetu na kuwasaidia wakulima wetu. Uchukuzi na usafirishaji wa mizigo yao hatimaye kuongeza kipato chao na kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari na viwanja vya ndege. Bandari yetu inafanya vyema katika eneo la *Container Terminal*. Kazi kubwa sasa ni kuiboresha *Dar Port* katika maeneo yake mengine, fedha zitengwe na zitolewe ili ziweze kukidhi shida hizo. Viwanja vya ndege ni lango lingine la kusaidia uchumi wa nchi yetu. Bado hatujatoa *priority* kwa viwanja vya ndege. Mapato yatokanayo na *Agency* ya *Airports* ni ndogo hayakidhi mahitaji ya *Agency* hiyo na kuboresha viwanja. Bado hatua za kufaa toka Wizara ya Fedha ya kuwapatia ufadhili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Sasa tuwe *serious* hasa Wizara ya Fedha ithubutu kutenda. La sivyo hatuwezi kukwea na kuvuka.

Kuhusu Vyuo vya Mawasiliano na Uchukuzi. Vipewe umuhimu wa pekee. *Subsidy* wanayopata ni chache sana haikidhi mahitaji ya vyuo hivyo. Ili tupate wataalamu bora Vyuo hivi sasa ni lazima visiadiwe na Serikali. Wizara itaendelea kujitahidi kuboresha shughuli zake ipasavyo.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake yeye upeo, mwelekeo na maudhui mahsusi katika kunyumbulisha na kueleza juu ya hali ya nchi, kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Aidha, kwa wananchi walio wengi naamini kuwa wametafsiri hotuba hii ina changamoto ya nini kifanyike katika kuboresha maisha na maendeleo ya Watanzania. Pamoja na pongezi hizi, naungana na Watanzania wengine wote kuzidi kumtakia kheri ya afya njema ili katika kipindi hiki azidi kulitumikia Taifa hili kwa moyo wa dhati. Pamoja na hotuba hii, nami napenda tu kujielekeza katika changamoto ya hotuba. Katika kipindi cha miaka nane ya utawala wa Mheshimiwa Mkapa mambo yafuatayo yamefanyika.

Moja, kuboreshwa kwa hali ya maisha ya Mtanzania katika nyanja za miradi ya jamii kama *TASAF*, *MMEM*, mara nyingi tumekuwa tukikopa kwa vyombo vya fedha lakini ulipaji wa madeni hayo haukwenda sambamba na matunda yake. Kwa miradi iliyopo na inayoendeshwa na wananchi imethibitisha kuwa Serikali hii imekuwa na mtazamo endelevu na hasa kwa kushirikisha wananchi ambao ndiyo wadau.

Pili, kuboreshwa kwa miundombinu ya kiuchumi na mawasiliano ya kijamii. Napenda kuwapongeza sana askari wote wa miavuli ambao kweli wamekuwa wakifanya kazi sambamba na mtazamo alionao Mheshimiwa Rais. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri walio chini ya Wizara yake wa nchi kwa kuwa makini katika masuala ya habari na jinsi ya kukubaliana na janga la njaa. Kwa nafasi ya pekee nampongeza sana Mheshimiwa William Lukuvi kwa mkakati mahsusi katika kushughulikia tatizo la njaa.

Mwisho, nashauri yafuatayo yapewe mkazo na msisitizo mkubwa kwa siku za usoni.

Moja, kuwawezesha kwa dhati watumishi wa umma waliotumikia taifa kwa ari kubwa na ubunifu.

Pili, kilimo, masoko na ushirika, vipewe uzito mkubwa ili tuwakomoe Watanzania na matatizo ya kilimo tegemezi na tuwe na masoko ya uhakika ya bidhaa zetu.

Tatu, rushwa izidi kupigwa vita kwa nguvu zote na suala la utawala bora lipewe msisitizo. Sote tupae kwenye ndege pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bila pingamizi katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, namwunga mkono mia kwa mia. Hakika ni hotuba nzuri, bora, makini na yenye mafunzo kwa wananchi Tanzania na hata nchi jirani. Pamoja na hayo nitachangia vipengele vichache kama ifuatavyo:-

Moja, kuhusu kuondoa umaskini, ni kweli yanawahusu wananchi na viongozi wao tukiwemo Waheshimiwa Wabunge. Lakini tuangalie taratibu za upanuzi wa barabara zetu ambazo zinawabomolea nyumba wananchi wetu na maskini bila kulipwa fidia. *TANROAD* inabomolea nyumba kwa upana wa mita 22.5, wakati enzi za *PWD* ilikuwa upana wa mita 15 je, kwa nini waliojenga kabla ya sheria hii ya *TANROAD* wasilipwe fidia kwa nyumba zao zinazobomolewa hivi sasa. *TANROAD* na Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam wanadanganya watu kuwa walikwishalipwa mwaka 1950, hili si kweli wapo wananchi ambao wapo hadi sasa wanadai hawakulipwa nyumba zao.

Kwa hiyo, Serikali bado tunaomba wananchi walipwe fidia za nyumba zao kwa kubomolewa kutokana na kupanua barabara. Wananchi pia wanashangaa kwa nini Serikali inabomolea vibanda na nyumba lakini barabara zenyewe hazijengwi kama ile ya Mbagala, Kongowe na iendayo Sinza na sasa wanatarajia kubomolea nyumba eneo la Gongolamboto -Pugu. Kama ujenzi wa barabara utachukua muda mrefu kwa nini wananchi wasipewe muda wa kutosha kujiandaa kuhama na kupata maeneo mapya ya

kuishi na famili zao? Bila maelezo ya kutosha, uchochezi wa kiupinzani unajenga chuki kwa wananchi na Serikali yao ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu. Hakika wazazi na watoto waliotangazwa ushindi wao wa kwanza tarehe 12 Februari, 2004 na Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge wamefurahi sana. Halikadhalika viongozi wa maeneo watokayo watoto hao tumefurahi pia. Hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwatangaza watoto hao na hivyo naomba utaratibu huo uendelee kufanyika kila mwaka ili kutoa changamoto kwa watoto wengine kufanya vizuri zaidi.

Kwa hayo machache, narudia tena kusema naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 12 Februari, 2004 mia kwa mia.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ilikuwa na hekima, ujasiri na imeonyesha mwelekeo wa Taifa letu. Sisi wasaidizi wake tumeipokea kwa furaha na tutaitumia kama dira ya kufanya kazi. Ninapenda kuchangia eneo linalonihusu moja kwa moja *EPZ/AGOA*. Mheshimiwa Rais ameonyesha kutoridhika na eneo hili na ametoa changamoto kuwa kasi ya kuendeleza *EPZ* maeneo huru ya biashara na pia fursa za kuuza bidhaa nje zifanyiwe uharaka kwa kipindi cha miezi 20. Nikiwa kama mtekelezaji mkuu naona nitoe matatizo yanayoikabili sekta hii na pia nitoe mawazo yangu ya ufumbuzi wa matatizo.

Moja, kuhusu mitaji ya kujenga miundombinu ya kuanzisha maeneo huru ya *EPZ*.

Pili, utaalamu na *Technical know how* ya kuanzisha viwanda au biashara za kuingia *EPZ/AGOA*.

Tatu, mitaji ya kuweza kuanzisha viwanda/biashara katika *EPZ* na za kupeleka *AGOA*. Benki zetu hazitoi fedha na kama zitatoa riba ni kubwa sana.

Nne, watu bado hawana mwelekeo wa kibiashara (*mindset*) kweli ni za kubadilishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufumbuzi. Moja, Serikali tayari tumeandaa mazingira mazuri ya kuwezesha watu kuanzisha hizi biashara kwa mfano, sheria ya *EPZ*. Tumehamasisha watu kujua kuhusu *EPZ* na *AGOA* na tumetafuta wataalamu wa kuanzisha viwanda hivi vya *AGOA* na kadhalika. Serikali imesaidia uanzishwaji wa kiwanda kimoja cha nguo kwa ajili ya *AGOA* ili ajira ipatikane na Watanzania waige mfano.

Pili, sasa pamoja na kufanya hayo bado kasi ya uanzishwaji ni ndogo na wawekezaji hawajitokezi. Tuna viwanda vitatu tu vinavyopeleka nje mali kwa *AGOA* na *EPZ*.

Napendekeza Serikali tufanye kama walivyofanya wenzetu wakati wa kuanzisha *EPZ* na *AGOA*. Mfano Sri-Lanka, Mauritius, Lesotho, Uganda and *South Africa*. Serikali tutenge fedha na kuzipitishia benki ya biashara yeyote ili tuwakopeshe watu na waanzishe viwanda ndani ya *EPZ* na kupeleka *AGOA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hii inaweza kuwa chini ya *Export Guarantee Scheme* inayosimamiwa na Benki Kuu (iliwahi kufahamika hapo awali). Mfuko huu uwe *deliberate* kwa *EPZ/AGOA* tu.

Tatu, Serikali tununue majengo ya *Millenium Park* ili yatumike kama eneo la *EPZ*. Tayari mazungumzo yamekwishaanza na *valuation* zimefanyika. Hii itatuwezesha kuanzisha viwanda hivi katika *EPZ Complex*.

Kwa kufanya hayo kwa haraka tunaweza kuanzisha viwanda vya *EPZ/AGOA* saba kwa kuanzia kabla ya Juni, 2004 na ajira itakuwa watu 10,000. Na baada ya *Budget* ya Juni, 2004 tungeanzisha viwanda 20 na kuleta ajira ya watu 30,000. Wawekezaji watatoka ndani ya nchi na nje ya nchi kama China, Sri-Lanka, Bangladesh na Mauritius.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nianze kwa kumtakia Mheshimiwa Rais afya njema ili aweze kupona mapema na kuungana nasi katika kazi za kuendeleza Taifa letu kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa nzuri sana, yenye kina, uwazi, matumaini na imetaja maeneo mengi muhimu. Hotuba hii kwa kweli ilikuwa *State of the Union Speech*. Kwa maoni yangu hotuba hii ilitoa tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa Uchaguzi Mkuu wa 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupendekeza kuwa hotuba hii wapewe ma-RC na ma-DC wote nchini, ili waweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuleta Bungeni Miswada ya kuanzisha Mashirika manne ya usimamizi ili kuwalinda wateja na kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki kwenye biashara yaani *EWURA, SUMATRA, TCRA* na *TCAA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Bunge lako Tukufu liliishakupitisha Miswada hii na Mheshimiwa Rais kuiridhia, mamlaka hizi bado hazijakamilika kiutendaji. Naomba, Serikali isichukue muda mrefu katika zoezi la kuanzisha Wakala hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa mpango mzuri wa MEM, ambao umewezesha shule zetu za msingi kupata madarasa na nyumba za walimu. Kwa upande wa shule za msingi za vijijini, napendekeza kuwa kipaumbele sasa kipewe katika kujenga nyumba za walimu. Kukiwa na nyumba za walimu za kutosha, basi tutakuwa tumepunguza kwa kiwango kikubwa tatizo la uhaba wa walimu katika shule hizo. Katika Jimbo langu la uchaguzi la Tabora Mjini, shule za msingi za vijijini zina tatizo sugu la walimu; kuna shule nyingi zina walimu wawili tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchangia kuhusu Mashirika ambayo yanasubiri kubinafsishwa na *PSRC* kama *TRC, Marine Services Company Limited, Tanzania Postal Corporation TTCL* na kadhalika. Zoezi la kubinafsisha linachukua muda mrefu! Wakati yanasubiri kubinafsishwa, Mashirika haya hayaruhusiwi kufanya kazi yoyote ya maendeleo! Kwa vile zoezi la kubinafsisha linachukua muda mrefu, hivi tunataka mashirika haya yaje kuuzwa kwa bei poa?

Vile vile wakati huu wa mpito mbona huduma zinazotolewa na mashirika haya zinaendelea kuwa mbaya? Kupanga ni kuchagua, kama tumeshindwa kubinafsisha mashirika haya, basi tukiri mapema ili tuendelee kuyaboresha mashirika husika kwa manufaa ya wananchi wetu.

Ningependa tena kuipongeza Serikali katika juhudi zake za kujenga barabara za uhakika nchini. Ninayo matumaini kwamba kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 fedha za kutosha zitatengwa kwa barabara zifuatazo:-

- Manyoni - Itigi-Tura - Tabora;
- Tabora -Urambo-Kaliua- Kigoma;
- Kigoma - Manyovu;
- Tabora- Sikonge -Mbeya;
- Tabora - Sikonge -Mpanda-Sumbawanga; na
- Tabora - Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi naomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kumpata Rais mwingine aliyejaliwa busara, imani, mkweli na mwenye kipaji maalum tena adimu duniani mwenye kulingana na Marais wawili waliomtangulia hapa Tanzania.

Baada ya kumshukuru Mungu Mtukufu mwenye uwezo na kila shaani, napenda niungane na wenzangu walionitangulia kuiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na ambayo inatoa dira ya utekelezaji na utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika kutokana na maudhui yake na namna ambavyo hotuba ilivyoandikwa na vile mwenyewe alivyokuwa anazungumza na sisi sote na hata kwa atakayeisoma tu kwa wakati wake basi iwapo atakuwa na akili timamu na kweli anataka kuona maendeleo basi hatakuwa na la kuongeza kwani imejaa kila kitu ambacho kimeagizwa na sera ya Ilani ya CCM wakati tulipokuwa tunaahidi kuwaondoshea dhiki na kero zao wananchi kwa kuwa karibu nao huko vijijini wanakoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe tungepata Rais wa aina gani mwenye sifa za aina hii zaidi ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa? Mimi nina hakika kuwa *wallah* Watanzania wengi na kama siyo wote wanaridhika na utendaji wake na ambao ametueleza kuwa muda wake wote tokea Taifa lilipomkabidhi ridhaa yetu ya kuiongaza nchi hii katika hotuba yake. Kwetu sote na mimi ninaipongeza sana. Mungu atampa afya kamili haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa hakika ninakuwa ninapata fadhaa kubwa kusikia kuwa bado Tanzania hii kuna watu wanaohubiri maneno na kutenda vitendo vinavyoashiria uvunjaji wa amani hapa Tanzania hususan kule kwetu Zanzibar. Hasa wanataka nini? Hivyo kweli bado tunao wasaa wa kuwasikiliza watu wajahili wa aina hii hapa Tanzania!

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wahenga huruma haileti mwana. Majeraha ya vurugu bado tunayo na kama dosari kwa umaarufu wa kutunza sifa ya amani Tanzania tumeipata kutoka huko huko na watu hao hao ambao hodari wa kukaanga mbuyu. Kuwaachia wenzao wazitafune, wanaeleweka na wengine wapya wanakuja, nasema hatutaki vurugu Tanzania hasa kule Zanzibar. Aidha, kwa kuwa sasa wakati wa kudhihirisha tabia ya uwazi na ukweli umewadia basi wale wanaoashiria umwagaji wa damu hapa nchini wasipewe nafasi hata kidogo. Kwa heshima zote na taadhima ninawaomba ninyi viongozi mliopewa dhamana ya kuidhinisha amani ya nchi muendeleze juhudi zenu za kuona amani Tanzania, basi tena kucheze kwani tuna baadhi ya watu wenye tabia za wale wagonjwa wa akili na hao wakisema basi hufanya ili mradi madhara hayawapati wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoshwa na kauli za vurugu ambazo zinatukosesha amani. Mabomu wamelipua kwenye mitambo yetu ya umeme, maghala yetu yenye akiba za karafuu yameuguzwa, mahoteli yetu mazuri yametiwa moto, nyumba zetu zimeuguzwa, shule na visima vya maji vimetiwa vinyesi, maaskari wetu wamejeruhiwa na kuuawa bado Serikali yetu inafuata utawala wa sheria, nadhani sasa Serikali zetu mbili zione umuhimu wa kuidumisha amani ambapo juhudi za makusudi zinafanywa kutiwa dosari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingetegemea kuwa hadi sasa tunapata vitendo hivyo na kauli hizo za kukosesha amani Watanzania wetu hususan kule Zanzibar kwa kuwapa bughudha ndugu zetu wa asili ya Tanzania Bara, kwani ni nani mkaazi na mzaliwa wa kule Visiwani ambaye ni Mtanzania asiye na asili ya Mtanzania Bara? Bado wanatokea wanajisifu kufanya fujo hata kudiriki kutaka kuteka Vituo vya Polisi na hata hili ndiyo Utawala Bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapinduzi ya mwaka 1964 Zanzibar yana uzuri na sababu zake na hili linaeleweka na lazima tudumisha mazingira yalioweka mapinduzi yale na tutambue kuwa mwanamume hadharau kauli.

Mheshimiwa Naibu Spika, narejea tena kutamka kuwa naunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

**MHE. DR. ASHA -ROSE M. MIGIRO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kujadili hotuba kuu (*Master piece*) ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Baada ya kusema hayo, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba ya kina na ya uwazi na yenye ukweli wa kisayansi. Vile vile naomba nimtakie afya njema na nafuu ya haraka aweze kupona kabisa na arejee katika kazi zake za Urais kama alivyokuwa kabla ya kupata maumivu.

Hata hivyo, hotuba yake bado imedhihirisha kwamba pamoja na maumivu hayo amepata muda wa kutayarisha hotuba nzuri kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiacha uzuri wa hotuba yenyewe na namna ilivyowasilishwa, hotuba hiyo imetoa changamoto kubwa kwetu kama wananchi, lakini pia tunaotokana na CCM tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyoelezwa na Mheshimiwa Rais kwani ndiyo lengo la Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2000.

Mafanikio hayo vile vile ni changamoto kwetu kuendeleza mafanikio haya kwa kuzingatia kwamba bado safari ya kuikwamua nchi yetu kiuchumi ni ndefu. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwa usahihi kabisa, nchi yetu sasa ipo katika njia ya kurukia ndege (*runway*) tuna changamoto ya kuifanya ndege sasa ipae. Hii ndiyo changamoto kwetu kama wananchi wazalendo na Watanzania na vile vile kama viongozi.

Tunapenda kuahidi kwamba tutafanya kila lililopo ndani ya uwezo wetu kusimamia na kuendeleza mafanikio tuliyoypata. Moja ya mambo ambayo ni ya msingi ni mabadiliko ya fikra na mtazamo. Wakati viongozi wa kisasa kama Waheshimiwa Wabunge, *RCS*, *DCs*, wanaonyesha utashi wa kisiasa kukamilisha programu mbalimbali za maendeleo, katika baadhi ya maeneo/Taasisi za umma watendaji hawajatambua umuhimu wao katika kufanikisha programu za maendeleo ambazo tumezianzisha.

Kwa hiyo katika kutekeleza changamoto alizozitoa Mheshimiwa Rais ni sharti sisi viongozi tuhakikishe tunakwenda sambamba na watendaji katika Majimbo yetu na katika maeneo yetu mengine ya kazi. Kwani utashi wa kisiasa ni sharti uende sambamba na utendaji makini, utendaji unaojituma na kuzingatia mipango ya maendeleo ambayo CCM na Serikali zake imejiwekea.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama msaidizi wa Rais na kiongozi wa shughuli za Serikali akishirikiana na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Makamu wa Rais, wamesimamia kikamilifu mipango yetu ya maendeleo, wametoa dira ya uongozi ambayo imewezesha nchi yetu kufikia kwenye *runway*. Tuwape ushirikiano, tujitume ili kwa pamoja sasa ndege yetu ipae.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DAMAS P. NAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza kwanza kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzito na iliyo dira ya maendeleo ya nchi yetu, na pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha Bungeni ili kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nipate ufafanuzi wa masuala kadhaa hapa chini:-

Kwanza, Elimu ya Sekondari. Tumepiga maendeleo ya haraka kwa Elimu ya Msingi kwa mpango wa MEM. Je, kuna mpango gani wa kiwango hicho kwa Elimu ya Sekondari ingawa tunayo habari juu ya MMES. Kulikuwa na msisitizo wa Elimu ya Msingi kwa wote wenye umri wa kwenda shule. Je, mpango wa Elimu ya Sekondari utakuwa na msisitizo na utekelezaji kama ule wa Elimu ya Msingi?

Leo hii hata ukitaka kujaza nafasi ya Mtendaji wa Kijiji sifa ya chini ni Sekondari, Kidato cha Nne. Hivyo ingefaa Elimu ya Sekondari iwe kwa wote, wakati umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, *vision* yetu ya mwaka 2025 inaimarisha maeneo muhimu ya kipaumbele kama vile afya, elimu, barabara vijijini ili katika kutokomeza umaskini. Ni kweli kumekuwa na mwamko katika maeneo hayo. Lakini tatizo langu ni barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini suala hili halipewi umuhimu unaostahili?

Kwa kuwa zaidi ya kilometa 50,000 za barabara vijijini ziko chini ya TAMISEMI, kwa nini isiundwe kurugenzi ya barabara katika Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi inamiliki kilometa 35,000 tu za barabara lakini ina kurugenzi za barabara kuu na Barabara za Mikoa. Lakini zaidi kuna *TANROADS*. Hii inaonyesha umuhimu unaowekwa juu ya barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini TAMISEMI ina tatizo gani kuweka uzito kama huo kwa barabara ambazo kwa hakika ndiyo inayomgusa Mtanzania hadi vijijini? Leo kuna Wahandisi wawili tu kuangalia barabara za nchi nzima. Haiwezekani!!! *They won't deliver.*

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda nipate ufafanuzi juu ya barabara Kuu ya Kaskazini, *The Great North Road*.

Je, Serikali haina mipango ya muda mrefu? Tunayo taarifa kuwa barabara hii inazungumzwa tangu miaka ya 1980 na 1990 lakini kwa uzito mdogo sana. Hata leo tunaizungumzia kama kipaumbele mojawapo katika *East African Community! This is not serious.*

Kama tunaamini mpango wa kujenga barabara nchini kwa fedha zetu ni endelevu kwa nini hauhusishi barabara hii? Angalau hata mpango huo wa *Special Projects* ungeonyesha mpangilio wake wa miaka kumi ili tuone na baadaye kufuatilia maendeleo yake.

Naomba tuambiwe *serious plan* juu ya barabara ya Minjingu - Babati - Dodoma hadi Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, bado shilingi bilioni 1.84 zinazotengwa kila mwezi kwa ajili ya barabara za *Special Projects* zinatosheliza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhusu reli, je, kuna mpango gani kuhusu kituo cha Reli hapa Dodoma ambapo kunakuwa na tatizo kubwa la *Access Road* kuwa kwenye sehemu moja na husababisha msongamano mkubwa wa magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kuna uwezekano wa *underground access road* kwenye *junction* au kufungua njia nyingine zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifafanuliwe hayo hapo juu. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo alilolizungumzia la mafanikio tuliyoypata katika kuboresha huduma za vituo vya Utafiti wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema Serikali imefanya ukarabati mkubwa wa Taasisi ya Vituo vya Utafiti uliohusisha Maabara, Ofisi, Nyumba na Miundombinu ya mashamba ya majaribio.

Katika hotuba yake amesema jumla ya wataalam 97 kati ya wataalamu 350 wamepatiwa mafunzo ya Shahada za juu (*MSc.* na *Ph.D.*) kwa shabaha ya kuwaimarisha kitaalamu.

Hatua hii ni mafanikio makubwa sana kwa Taifa letu na tuna kila sababu ya kujivunia kwa sababu kilimo katika nchi yetu bado kitaendelea kuwa ndiyo mhimili na nguzo kuu ya uchumi wa Taifa letu na



bado kitaendelea kutoa ajira kubwa kwa wananchi wapatao asilimia 80% ya Watanzania wote na kilimo kinatuingizia karibu asilimia hamsini ya mapato ya fedha zetu za kigeni.

Kwa kuwa katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema Serikali itaendelea kuimarisha Miundombinu ya mashamba ya majaribio ya Taasisi za Vituo vya Utafiti, nina maombi yafuatayo kuhusu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian.

Kwa kuwa kituo hiki cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo kina jumla ya eneo la ekari 769 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kuzalisha mbegu mama (*Breeder Seeds*) za mazao ya mahindi, maharagwe na ngano kwa mahitaji ya Taifa zima na kwa kuwa kwa sasa eneo hili la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo limepunguzwa ekari 150 ya mashamba ya majaribio kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja cha Ndege ili kifikie hadhi ya kuwa *International Airport* na kwa taarifa zilizopo Manispaa ya Mji wa Arusha katika *Master Plan* yake inataka kunyang'anya eneo lote la ekari 769 na sio tena ekari 150 kwa madhumuni hayo hayo ya kukitaka kiwanja hiki kiwe na hadhi ya *International Airport* katikati mwa eneo la Manispaa ya Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ifute hoja ya kutaka kuuu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian na isiruhusu kukubali hata ekari moja kutolewa katika Taasisi hii ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian.

Mheshimiwa Rais, ametamka katika hotuba yake jumla ya wataalamu 97 kati ya wataalamu 350 wamepatiwa mafunzo ya shahada za juu yaani (*MSc.* na *Ph.D.*). Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian ina jumla ya wafanyakazi wa kada mbalimbali 101 wakiwemo watafiti 40, wenye ujuzi wa viwango mbalimbali vya elimu kama Digrii ya Udaktari wa Falsafa (*Ph.D.*) 9, Digrii ya Uzamili (*MSc.*) 25, na Digrii ya kwanza (*BSc.*) 6 na Stashahada 34.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian ni uthibitisho wa ushahidi wa utekelezaji wa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake katika Bunge hili. Kutokana na maelezo haya naiomba Serikali hoja ya kutaka Taasisi ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo kuvunjwe na kuuawa ili kutoa nafasi ya kupanua Kiwanja cha Ndege ifutwe na kwa maana hii naomba eneo lote liachwe kuendelea kuwa eneo la miundombinu ya mashamba ya majaribio ya utafiti wa Kilimo na Mifugo kama ilivyoeleza hotuba ya Mheshimiwa Rais juu ya kuimarisha miundombinu ya mashamba ya majaribio.

Kwa maoni yangu hoja ya kuvunjwa na kuuu Taasisi ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian kwa ajili ya kupanua Kiwanja cha Ndege ili kiwe cha Kimataifa kiweze kuvutia Watalii kwa sababu kipo ndani ya Manispaa ya Arusha na hoja ya kutaka Kiwanja cha Ndege kuhitajika kuwa ndani ya Manispaa ya Arusha ili kuwa karibu na Mji Mkuu wa Afrika Mashariki hazina nguvu na wala hazina uzito hata chembe kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, Mradi wa *Tanzania Canada Wheat Programme* ulijenga nyumba za makazi kwa wafanyakazi wa kituo hiki cha utafiti Selian 58 na Serikali ya Canada ilijenga maabara za kisasa na ofisi.

Pili, Taasisi ya Kituo hiki cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian kimetoka kutoka mfumo wa ufadhili kupelekea mfumo wa kujiendesha chenyewe. Jambo ambalo Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ametueleza Watanzania tujenge tabia ya kujitegemea.

Tatu, Taasisi ya Kituo hiki cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian kimepungua mkazo kwenye utafiti wa mazao ya ngano na shayiri na kuanza utafiti wa mazao mbadala yanayolenga mahitaji ya wakulima wadogo zaidi. Jambo ambalo Mheshimiwa Rais ameagiza na amekuwa anaagiza mara kwa mara wakulima wadogo wadogo lazima waendelezwe.

Nne, majukumu hayo Taasisi ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian inatekeleza katika programu zifuatazo:-

- (i) Programu ya mazao ambayo yanahusisha mahindi, maharagwe, ngano na shayiri na mazao badili;
- (ii) Programu ya mifugo;
- (iii) Programu ya utafiti maalum (udongo, maji, miti na mazingira);
- (iv) Programu ya mifumo mbalimbali ya ukulima na uchumi wa kijamii; na
- (v) Idara ya mahusiano ya ugavi na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Ofisi ya Umoja wa Kimataifa iliyopo Kenya ipo umbali wa kilomita 15 kutoka *Nairobi City Centre* lakini wafanyakazi na watu wenye shida na ofisi hiyo wanasafiri umbali huo wa kilomita 15 kupata huduma wanazohitaji. Kwa hoja hii madai ya kutaka kuuu Taasisi ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian ili kupanua kiwanja ndani ya Manispaa ya Arusha haina msingi.

Sita, kiwanja hicho kinachotaka kupanuliwa ndege kubwa za *Boeing 707, Fokker Friendship* hata *ATC* zitashindwa kutua na kupaa kwa sababu *runaway* yake ipo karibu sana na milima hivyo ndege kubwa haziwezi kutua wala kuruka.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kwa sasa tayari tunacho Kiwanja cha Ndege cha *Kilimanjaro International Airport (KIA)* ambacho bado hakitumiki vizuri kikamilifu. Kwa ajili hii kuna sababu gani na kujenga kiwanja kingine kwa lengo la kutaka kuvunja na kuuu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian. Kama fedha zipo basi zijenge *International Airport*, Dodoma na vipanuliwe viwanja vya Lindi na Mikoa mingine.

Nane, karibu Miji yote Dunaiani (*International Airport*) zao zipo mbali na *City Centre* kwa mfano Kiwanja cha *Heathrow Airport* kilichopo London, Uingereza kipo mbali sana na *Central London*. Katika nchi ya *India Agricultural Research Institute* ipo New Delhi na *International Airport* ipo Bomba Mumbai na huo ni umbali mkubwa sana kutoka Mji Mkuu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, *Kilimanjaro International Airport (KIA)* ina umbali gani wa kutisha hata ionekane watalii na wageni wengine wakatae wanaposafiri kutua pale.

Kumi, kwa maoni yangu nadhani wanaotaka kiwanja hicho kijengwe ili kubomoa na kuuu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Mifugo Selian hoja zao haziko *balanced* na kumi na moja, wa sababu maelezo hayo niliyoyotoa na kwa maoni yangu yanazingatia maelezo ya hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naomba kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara zinazohusika zinipe maelezo kwa nini wanataka kuuu Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Selian na kutaka kujenga au kupanua Kiwanja cha Ndege na huku wakijua dhahiri tunacho Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ambacho kina hadhi ya Kimataifa na hivyo kinakidhi haja ya utuaji na urukaji wa ndege kubwa na ndege ndogo zinazotumiwa na watalii na wageni wengine wa Kimataifa.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya pili kuwa Bunge lako Tukufu limepata nafasi ya kujadili na kufafanua hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama kawaida hotuba hii ni nzuri na imejaa maelekezo na maagizo ya kufanyia kazi kwa Serikali wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Bunge lako Tukufu ni kutoa maelekezo kwa Serikali kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais. Ni ukweli usiopingika sasa inapelekea wakati wa kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais na wakati mwingine Miswada mbalimbali imekuwa ni kama kipindi cha kujipima ufasaha katika mambo ya aina nyingi. Serikali haitilii maanani na mwisho wake hakuna kinachotekelezwa.

Hotuba hii tunayojadili leo ni ya pili ambayo maagizo yake yanafanana na hotuba ya Mheshimiwa Rais iliyotolewa Bungeni hapa wakati wa kufungua rasmi Bunge hili mwezi wa Novemba 2001. Hotuba ile ilitoa malengo na maelekezo kwa mwenendo wa maendeleo kiuchumi na kijamii. Leo hii miaka minne na karibu Bunge linamaliza muda wake hakuna cha maana kilichotekelezwa kupelekea kutimiza malengo na maagizo ya Mheshimiwa Rais. Kama kumefanyika matekelezo ya malengo na maagizo mpaka sasa kwa maoni yangu hayatoshi ni kidogo sana na tena kwa kubahatisha tunaendelea kutembea pole pole badala ya kukimbia kujaribu kuwafikia wenzetu kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais kuna maeneo matatu ningependa kuchangia sekta za kilimo, umeme vijijini na barabara vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo sasa sio suala la “kuendeleza kilimo cha sasa ni suala la kuleta mageuzi kamili na kuachana na kilimo cha sasa cha kutegemea msimu wa mvua. Katika hotuba ya Novemba 2001 Mheshimiwa Rais aliagiza kuwa ifikapo mwaka 2025 Kilimo cha Taifa kitakuwa cha kisasa cha umwagiliaji maji, uvunaji maji ya mvua na kutumia nguvu za mashine na mitambo, pembejeo za kisasa na taaluma za kisasa.

Katika hotuba ya tarehe 12 Februari, 2004 Rais amesema kuwa atakapoachia madaraka mwaka 2005 uchumi wa Taifa utakuwa umepaa angani na sio kuendelea kuchochea injini zake kwenye njia ya kurukia (*economic runways*). Kwa miaka minne tangu Novemba, 2001 hakuna cha maana kilichoonyesha kuwa sasa kilimo kimeanza kutayarishwa kuingia kwenye mageuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha kumwagilia mashamba hakijapanuliwa kwa makusudi ya kuleta mageuzi. Hadithi zote za kilimo cha kumwagilia ni kujihami tu, leo mabwawa ya maji karibu 90% ni ya kunyweshea mifugo na matumizi ya binadamu. Mabwawa ya kilimo ni tofauti na mabwawa ya mifugo, mabwawa ya kilimo ina miundombinu ya ziada kama mifereji, mabomba, mapampu na kadhalika ili kufikisha maji mashambani kutoka mabwawani.

Kilimo cha kumwagilia mashamba kwa tasfiri ni kuwa kuweka uwezo kwa mwananchi aweze kulima (kupanda na kuvuna) wakati wowote hata wakati wa kiangazi. Kilimo cha umwagiliaji kinachopigwa kelele sasa ni kile cha kukinga maji ya mito wakati mvua na kupeleka mashambani mvua ikipotea hata kwa siku mbili umwagiliaji wa mashamba haupo kwani mito pia hupungua maji. Hiki ndicho kilimo cha umwagiliaji katika Taifa letu. Wakati wa kiangazi mito imekauka wananchi wakulima huweka majembe yao uvunguni kungojea msimu mwingine wa mvua!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa kilimo kama hiki kilichobatizwa kilimo cha umwagiliaji mwananchi kweli atajinusuru kutoka kwenye umaskini uliokithiri, hasa kama ataweza kwa bahati akavuna mara moja tu kwa mwaka? Hotuba hii ya Rais ilete mwamko mpya wa kuleta mageuzi kwenye kilimo kutoka kilimo cha kutegemea mvua na kuingia kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji na tuanze hatua kwa hatua mpaka tutakapozika kero za njaa katika Taifa letu. Hasa Halmashauri za Wilaya zingewezeshwa na zingeagizwa kuwa kila Kijiji kiwe na bwawa au mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ningependa kuchangia ni lile linalogusa umeme vijijini. Umuhimu wa kupeleka nishati hii vijijini ni kuharakisha maendeleo kwa sasa kasi ya kupeleka umeme vijijini ni ndogo sana na ni wakati Wizara sasa ikamilishe haraka iwezekanavyo kuunda Taasisi za Wakala (*REA*) na mfuko wa *REF* kusudi kutatua matatizo yaliyokwamisha umeme kupelekwa vijijini. Kimaendeleo kuwa maendeleo mengi vijijini yangeweza kunufaika na umeme vijijini kwa mfano kusindika mazao, uvuvi, elimu, teknolojia, viwanda vidogo vidogo (*fabrications*).

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo hotuba hii imemulika ni miundombinu ya barabara, madaraja na hata njia za miguu vijijini. Kusema kweli, Serikali hii ya Awamu ya tatu imejitahidi sana kufungua na kuunganisha nchi kimawasiliano hasa ujenzi wa barabara kuu (*National Highways*).

Kwa kipindi hiki sasa Serikali imulike zaidi katika Halmashauri za Wilaya kuziimarisha kiuwezo, kifedha, vifaa na kitaalamu kusudi ziweze kujenga mitandao ya kisasa ya barabara vijijini. Hali ya

barabara vijijini ni duni sana na hata tukakamilisha mitandao ya barabara za Kitaifa (*National Highways*) kimaendeleo tusipokwenda sambamba na uboreshaji wa mitandao ya barabara vijijini itakuwa kama kusafisha kikombe nje na kuacha uchafu ndani. Halmashauri zetu zipewe uwezo wa kutosha na sio tu ruzuku ndogo za fedha ambazo haziwezi kufanikisha ujenzi au ukarabati wa barabara vijijini. Suala la ruzuku na uwezeshwaji (*Capacity Building*) litazamwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, kwa hotuba ya utekelezaji na maelekezo ya utendaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwongozo wa maelekezo yaliyosaidia namna ya kuendeleza kazi nzuri iliyofanyika chini ya uongozi wa Rais wetu. Naunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Rais kwa hali yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais katika hotuba hii, yanatakiwa kufafanuliwa kwa lugha nyepesi. Idara kwa Idara, Shirika kwa Shirika, Taasisi kwa Taasisi. Lazima taarifa hii ifike mashuleni, vijijini na katika Kamati mbalimbali za wadau wote ili kwa pamoja lugha moja itumike katika kutoa tafsiri sahihi na isiyopotosha umma. Viongozi wa Chama Tawala na Watendaji wote waisimamie na kufafanua hatua hizi za awali za kujenga mazingira ya kukuza uchumi wa wananchi wetu. Hatuwezi kufanikiwa kuinua uchumi wa kila mmoja wetu, bila kuandaa mazingira na miundombinu ambayo itasaidia kuingia katika hatua ya kukuza uchumi. Utawala bora ndiyo msingi imara wa kufanikisha hayo. Tueleze kwa uhakika umuhimu wa hatua hizo za awali za kujenga uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ambao ningependa kuanza nao, ni kusaidia mafunzo ya kina kwa maafisa wetu Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti na Madiwani kwa kupewa pia posho za kuwasaidia wazunguke kuifanya kazi hii nzito. Semina za Kitaifa, zihamie vijijini. Vitendea kazi mfano baiskeli zisambazwe kwa viongozi wote wa vijiji, Kata kwa kusaidia jitihada za kuongeza motisha kwa kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni *agenda* ya kufa na kupona, usalama wa raia wetu unategemea sana upatikanaji wa maji salama na ya uhakika. Ninashauri Serikali itoe kipaumbele kwa kuanzisha Mfuko wa Maji (Kitaifa) ili usaidiane na mifuko ya maji midogo midogo iliyoanzishwa huko vijijini na katika kata nyingi nchini. Suala la madhara yatakayotokana na upungufu wa maji ni kubwa sawa kabisa na ukosefu wa chakula nchini. Uhusiano huu ni wa karibu sana. Sawa na jicho na mdomo na pua. Bila maji hakuna uhai, bila maji salama hakuna afya, bila afya hakuna uchumi kukua na huu ndiyo mtiririko wa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula kisiendeleo kutegemea Serikali peke yake. Lazima tuandae mazingira ya kuwaruhusu wafanyabiashara wajiingize kwenye hifadhi hii kwa masharti nafuu. Ombi pia ni kwa Serikali kuendelea kuimarisha kiwango cha akiba kisichopungua tani 150,000 kwa wakati wowote ule. Kila mara kiwepo chakula cha kuza na cha kazi. Cha bure kutolewa kwa maafu tu na kisitolewe kisiasa maana watu wetu wakijua wanaweza kila mara kupata chakula cha bure watabweteka. Tusisahau matatizo aliyoyapata Baba wa Taifa wakati wa njaa ya mwaka 1974 alipotakiwa na wakazi wa Dodoma atumie vijana wa JKT kufanya kazi za kuwalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa uhakika kwa vijiji na watu wetu ni wa upepo, *Biogas*, mkaa wa mawe na jua. Kila jitihada ifanywe ili kasi ya ongezeko la matumizi ya nishati hizi mbadala zifanikiwe. Mafanikio yatatokana na jitihada za kuanzisha Mfuko Maalum wa Nishati Vijijini, maana tunaielewa kuwa umeme wa *TANESCO* hautakuwa rahisi kulipiwa na watu wenye kipato kidogo. Hawa ndiyo tusipowapatia nishati mbadala, wataendelea kutumia kuni, mkaa wa kuni kwa kupikia na hivyo kuathiri sana mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha kilimo cha uchumi wa wananchi wetu, kazi ambayo imeanza na ningeiomba iendeleo ni kuendeleza kuimarisha Miundombinu muhimu. Barabara kwa kanda za Mikoa ya Kusini, Kanda ya Magharibi ya Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa hadi Mbeya zipewe kipaumbele. Uzalishaji wa kanda hizi, unaweza kuhakikishia nchi hii kuwa na chakula cha kutosha kwa

miaka mingi ijayo, bila hata kuingiza gharama nyingi za uzalishaji. Tuombe Serikali ikamilishe azma yake hii ili iungane na Mkoa iliyo kwenye *Mtwara Corridor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yamekwisha wasilishwa na Waheshimwa Wabunge wenzangu. Kinachotakiwa ni kila Mkoa uwe na *Action Programme* ya kutekeleza na kusimamia maelekezo ya hotuba hii ili ujasiri wa kila kiongozi uonekane, pia katika kupambana na rushwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kheri, fanaka, baraka na afya njema Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, ili akamilishe kazi nzuri aliyoianza.

Naunga mkono hotuba yote asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono mia kwa mia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake iliyojaa hekima, maelekezo na hasa hotuba hii ilionyesha utekelezaji wa Wizara mbalimbali katika kipindi cha miaka mitano. Mheshimiwa Rais anapaswa kupongezwa kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kusimamia kurekebisha uchumi ambao umetuwezesha kutekeleza miradi mingi katika Wizara ikiwemo elimu, maji, barabara, mawasiliano na kadhalika na kwa kweli Mheshimiwa Rais kazi alizozifanya ni nyingi sana likiwemo daraja la Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe angalau Serikali ilitupie macho suala la kilimo cha chakula. Wizara iandae miradi ya vijana ambao sasa hivi ni wengi hawana kazi na watafutiwe pembejeo kwa kukopeshwa ili waweze kulima na kuzalisha na kufungua viwanda vidogo vidogo na waweze katika maeneo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo la njaa ambalo limesababisha baadhi ya wanavijiji wengi kuhama vijiji vyao na baadhi ya wanaume wahame na kuacha wake zao na watoto wanahangaika kutafuta chakula kwa kisingizio cha kwenda kutafuta chakula.

Namuomba Waziri mwenye dhamana awakemee wanaume waliotoroka au kukimbia familia zao katika kipindi hiki kigumu cha njaa warudi wasaidiane na familia zao kutafuta chakula.

Kuhusu barabara, naiomba Serikali iweke barabara ya kutoka Minjingu - Babati - Kondo - Dodoma mpaka Iringa katika makisio yake ya fedha za ndani ijenge kwa kiwango cha lami kwani hakuna mfadhili anayeonekana kugharamia barabara hiyo ambayo ni ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Rais aiangalie barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika hotuba ya Mheshimwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ilikuwa nzuri sana na itafanya kazi katika muda wote wa uongozi hata kwa miaka mia ijayo kwani hotuba hii inafunza na inajenga kama kiongozi yoyote hupenda kujifunza au kukubali kukosolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia sehemu moja ambayo ni kiungo kikubwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijana na Halmashauri, Serikali ya Awamu ya Tatu ina mwamko mkubwa na kujali wananchi wake ndio maana ikatenga Wizara ya kuondoa umaskini hiyo yote ni jitihada ya Rais kujali wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana linakuwa tatizo kubwa na kupata usumbufu mkubwa katika kujajiri tunawaambia na kusesitiza vijana wasisubiri kuajiriwa na wao kuzingatia hayo. Sasa iweje vijana husumbuliwa kwenye Halmashauri nyingi kuwahamisha hamisha vijana hao na wengine kuwanyang'anya biashara zao. Serikali haioni hasa kuwa inawarudisha nyuma vijana hao kimaendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa za kulevya, vijana wengi huathirika na dawa za kulevya, je, Serikali yetu hasa vyombo vya dola haiyaoni haya na vijana wengi kupoteza maisha yao kwamba dawa hiyo kitengo cha kuzuia madawa hayo kuingia nchini? Kuna utaratibu upi ambao utatumika ili vijana kuepukana na tatizo la madawa hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na uongozi wa Awamu ya Tatu wa Rais Benjamin Mkapa alivyo makini naamini hili linamsumbua sana kwa ongezeko la dawa za kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni suala muhimu sana kulisimamia kama hatukuwa makini hapo baadaye kama miaka 10 ijayo tutakwama vijana wengi ambao wameathirika kiakili. Naomba suala hili lizingatiwe sana usemi ambao unasema vijana Taifa la kesho. Naamini usemi huo utakuwa hauna maana hata kidogo kwani vijana wengi watakuwa wameshaathirika na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuzingatia elimu kwa vijana na vijana kupata mwamko mkubwa wa kusoma kwa kiwango cha elimu ya juu ndani ya nchi na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo, vijana hao wanaomaliza masomo yao kuomba kazi maeneo tofauti lakini wanapooomba kazi hupewa masharti mpaka wawe na uzoefu. Je, uzoefu huo kaupata wapi na yeye akiwa katoka kusoma hauoni kuwa kigezo hicho ni kuwaburuza vijana ambao wana elimu kukosa kazi kwa kuwa hawana uzoefu wa kazi. Hiki ni kigezo kigumu sana hicho na kuacha vijana wenye elimu zao kuzurura au kuwa Wamachinga tu.

Kuhusu mikopo kwa vijana, Halmashauri zilisitisha na baadhi zilikuwa hazitoi kabisa na sasa muda unakwenda Serikali haioni kuwa vijana na akinamama wanazidi kupata taabu sana kwa nini Serikali isifuate utaratibu wa *PRIDE* ambayo inatoa mikopo kwa watu wote hao na haina matatizo hata kidogo inasaidia sana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwamba Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametaka kutushirikisha sisi Wabunge kama wabia wa Serikali katika kutekeleza masuala muhimu ya hatua ya Taifa letu.

Tunapoelekea mwisho wa utawala wa Serikali ya Awamu ya Tatu, kwangu mimi ninatafsiri jambo hili kama kitendawili changamoto nzito *a very challenging conundrum*. Hii ni kwa sababu kwa maneno mengine, Rais ametuachia wosia mzito kuendeleza utashi wa kisiasa na kuendeleza mageuzi ya kiuchumi ambayo ndio yamekuwa msingi wa mafanikio tuliyofikia mpaka sasa katika maendeleo yetu Watanzania kama alivyobainisha Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa kisiasa umewezesha kuendeleza mageuzi, ubinafsishaji, kukuza mitaji ya nje na ndani na kuongeza sehemu ya bajeti ya Serikali kwenye sekta za kuondoa umaskini. Mageuzi ya kiuchumi yamewezesha kuongeza mapato, kuvutia wawekezaji wa mitaji wa ndani na nje na kujenga mahusiano mazuri na wahisani kupelekea kuongezeka kwa misaada iendayo kwenye sekta za kupiga vita umaskini na kufutiwa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitendawili, changamoto nzito kwa sababu si siri kwamba baadhi yetu bado hatuyaamini mageuzi *lack of commitment to the reforms* na sio siri kwamba wengi wetu bado tunahoji ubinafsishaji na ukuzaji wa mitaji ya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitendawili changamoto nzito kwa sababu pasipo utashi wa kisiasa na pasipo kuchochea kasi ya mageuzi kiuchumi, maendeleo yetu, kwa ujumla yake, yatakuwa mashakani. Hayatakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Rais amebainisha baadhi ya misingi ya maendeleo endelevu ambayo alisisitiza katika kipindi kilichosalia cha utawala wake:-

- (a) Kuwasaidia na kuwawezesha wananchi kujiendeleza; kwa mfano kuwezesha Serikali za Mitaa, kuimarisha ushirika, kuwashirikisha wananchi kidemokrasia katika kupanga kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.
- (b) Kuimarisha usimamizi wa uchumi.
- (c) Kuwezesha sekta isiyo rasmi, kwa mfano kutumia Bajeti ya Serikali kuchochea upatikanaji wa mitaji na ajira.
- (d) Kukuza mauzo nje kama msingi wa kujenga uchumi imara wa ndani na kuondosha vikwazo vilivyo katika njia ya Watanzania walio tayari kujiendeleza kwa mfano mipango ya kuboresha elimu (MMEM, MMES, Mifuko ya Kuendeleza Elimu), kuongeza upatikanaji wa mitaji na kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi hiyo itasaidia sana kuimarisha uchumi. Mpaka sasa uchumi wetu haujaimarika *skill fragile* kuweza kuhimili misukomsuko inayotokana na mazingira yanayotuzunguka. Tunashuhudia uchumi wetu ukitikisika na kuyumba sio tu wakati wa matatizo, lakini pia hata nyakati za mema. Kwa mfano, nyakati za ukame kunakuwepo njaa, upungufu wa umeme na kadhhalika. Hali kadhalika, wakati wa maridhawa, uwezo kwa mfano kununua, kuhifadhi na kusafirisha chakula unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hayo, ningependa kupendekeza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha barabara za vijijini. Ili kufanikisha hili nashauri tupitie upya mgawanyo wa asilimia 70:30 wa fedha za matengenezo ya barabara za Kitaifa na za vijijini angalau uwe asilimia 50:50 ili kuongeza Bajeti ya Serikali iendayo kwa matengenezo ya barabara vijijini zenye asilimia 60 ya mkudao wa barabara zote nchini; na zinahusu zaidi ya asilimia 85 ya Watanzania wote ambao ndio wazalishaji wakuu wa Pato la Taifa na uuzaji bidhaa nchi za nje. Na vile vile ndio walengwa wa sera na mikakati ya kuondoa umaskini.

(b) Kuibua na kuendeleza Kanda kuu za Maendeleo ya Uchumi wa Taifa ambazo kwa ujumla, ni tatu, *Mtwara Southern Highlands - Lake Tanganyika Development Corridor*, (ii) *Lake Victoria - Kilimanjaro - Tanga Development Corridor* na (c) *The Central Economic Development Corridor* kukijumuisha Dar es Salaam -Morogoro- Dodoma- Singida- Tabora- Kigoma na Tawi la Isaka Kanda ya Maziwa Makuu.

Kama alivyobaini Rais katika hotuba yake, nyakati zimebadilika, tunahitaji mbinu mpya kukabiliana na changamoto za leo, zijazo (ukurasa wa 12). Hivyo tuwe wajasiri kutekeleza mikakati mahsusi wa kuibua na kuendeleza wakati mmoja, Kanda Kuu za Maendeleo ya Taifa, Kanda zinazotokana na bahati ya kijiografia ya nchi yetu

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulilaani mpangilio wa miundombinu tuliyoachiwa na Wakoloni ya barabara na reli kuwa zililenga kunyonya malighafi zetu ili kuneemesha uchumi wa nchi zao, lakini nyakati zimebadilika na kama ambavyo kwa ujasiri kabisa Rais ameongeza tija kama jambo la tano katika mambo manne ya maendeleo yetu yaani watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora na si kujielekeza kwa makusudi kuibua na kuendeleza hizo Kanda kuu tatu ya maendeleo ya uchumi wetu ya utandawazi yanatusukuma. Tusilazie damu fursa zinazojitokeza kuimarisha biashara ya kupitisha baina yetu na nchi 6 tunazopakana nazo, na papo hapo kuimarisha uwezo wa ndani wa kukuza mitaji, kuzalisha huduma na kufanya biashara ya uhakika zaidi.

Hivyo, kama ambayo Serikali imebaini pasipo shaka Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, lakini kwa ujumla wake zipo Kanda kuu tatu za maendeleo:-

(i) Ukanda wenyewe wa Mtwara lakini uendelee mpaka Ziwa Tanganyika kupitia Nyanda za Juu Kusini ili kuibua pia raslimali za makaa ya mawe na chuma ya Liganga na Mchuchuma na kuchochea biashara kubwa ya madini iliyoko Mikoa ya Kusini mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo;

(ii) Kanda ya Ziwa Victoria - Kilimanjaro Tanga ili kuibua na kuendeleza uchumi wa migodi madini ya Kanda ya Ziwa Victoria, Utalii wa kanda ya Kaskazini, uzalishaji wa mazao Makuu ya kahawa, pamba, katani, mazao yasiyo asilia. Kwa mfano, bidhaa za kusindika viwandani na kukuza biashara na Uganda; na

(iii) Ukanda wa Kati wa Maendeleo ukilenga kuibua na kuendeleza uwezo wa kiuchumi na kijamii uliopo katika mabonde ya Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Kigoma na papo hapo, kukuza biashara ya kupitisha kati yetu na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Rwanda na Burundi.

(c) Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya kilimo yanayosindikwa katika viwanda hapa nchini ili kuongeza thamani yake, kukuza vipato vya wananchi, kupata ajira ya kujenga uwezo wa soko la ndani. Mazao mengi ya kilimo yanatuwezesha kutimiza azma hiyo kwa mfano pamba, mbegu za mafuta ya kula na kadhalika.

(d) Kuendeleza nishati yenye uhakika zaidi kuhimili mahitaji ya Kitaifa na sio nchi jirani kutokana na fursa za utandawazi, hususan kuendeleza umeme wa makaa ya mawe ya Mchuchuma wenye bei nafuu.

(e) Kuboresha elimu kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano. Maendeleo ya elimu katika mazingira ya utandawazi lazima yaambatane na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano (*Information Technology*) tangu shule za chekechea kuendelea mpaka juu, kama ilivyo katika nchi zingine. Hivyo na sisi kama Taifa, lazima tuwe na mkakati wa kusambaza nishati itakayowezesha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano wakati wa kutoa elimu katika shule zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena, Rais ametupa kitendawili, changamoto nzito na nzito zaidi kwa sababu kwa namna moja au nyingine, kwa kiasi kikubwa, lazima tukubali pia kwamba maendeleo ya sasa ya nchi yetu yanatokana na dira na *goodwill* ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine mimi ninapata wasi wasi mkubwa kweli kweli kama kweli maendeleo yetu yatakuwa endelevu. Tuchukue sura moja tu ya maendeleo yetu; tunapanua na kuboresha miundombinu ya kiuchumi na kijamii - barabara, shule, hospitali/zahanati, visima vya maji na kadhalika na kuajiri walimu na watendaji wengi zaidi.

Mambo yote haya yanapelekea kupanua sana msingi wa matumizi japokuwa tumejiwekea malengo mahsusi ya kuongeza mapato ya nchi. Wasiwasi wangu ni kama wahisani wataendelea kutuunga mkono na mapato yetu yataendelea kupanuka sambamba na upanuzi wa msingi wa matumizi. Kama kweli uwezo wetu utaendelea kupanuka kwa kasi ile ile ya mahitaji yanayotokana na kupanuka kwa msingi wa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonitia moyo ni kwamba waasisi wa Taifa letu walitujengea misingi ya kutuwezesha kuwa na maendeleo. Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julisu Kambarage Nyerere, alituachia misingi ambayo imetufanya tuendelee kama Taifa lenye heshima, mshikamano, amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *this was the ceasar, would there come such another!* Nakushukuru sana.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo thabiti katika kuendeleza Tanzania kwa mujibu wa sera za CCM na mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa kasi kubwa zaidi na maendeleo endelevu. Ama nchi yetu imepiga hatua kubwa mbele takriban katika nyanja zote za huduma za jamii na uchumi



mpana kwa muda mchache tokea jitihada mpya zilipopamba moto chini ya Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, akisaidiwa na askari wake makini wa mwamvuli. Ni dhahiri kwamba asiyeona maendeleo hayo makubwa ama ana kasoro yeye mwenyewe au ana lake tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya uzuri wake, hakika hotuba hiyo imeweka mkazo mzito katika maeneo yote muhimu ya maendeleo. Kutokana na ufinyu wa fursa ya uchangiaji, ningependa kuchangia baadhi tu ya masuala haya, hasa ikizingatiwa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamekwisha kuchangia karibu maeneo yote muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza kasi ya kubadili mtazamo wa watumishi wa umma kuna umuhimu wa pekee. Bila kuwa na watumishi wenye elimu stahiki, wenye kutambua ipasavyo wajibu wao mkubwa kuwa ni kuhudumia umma wa Tanzania na kuendeleza katika maendeleo ya kweli na endelevu kwa nidhamu ya hali ya juu, uadilifu mkubwa bila mizengwe, ubabaishaji au ubaguzi wa aina yeyote, nchi yetu haiwezi kusonga mbele kwa namna na kasi inayotarajiwa. Hivyo, hapana budi msisitizo mkubwa na hatua thabiti zichukuliwe kuhakikisha maboresho yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,ufanisi katika kuleta maendeleo ya kweli kwa kasi kubwa utaweza kuimarishwa kutokana na kuchapa kazi kwa bidii, nidhamu ya hali ya juu, mshikamano katika ngazi zote za uongozi na utekelezaji pamoja na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna umuhimu mkubwa wa kuwahamisha watumishi wa umma kutoka mahali pamoja hadi pengine mara kwa mara ili kuwapa uzoefu mpana na kuepusha hatari ya watumishi kuota mizizi mahali pamoja na kutumbukia katika lindi la rushwa na kuuwa misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika sana kwamba Jimbo langu la Uchaguzi la Mkinga na Wilaya ya Muheza kwa jumla tumefaidika sana na programu mbalimbali za maendeleo chini ya sera za CCM na ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. Hata hivyo, bado jimbo la Mkinga lina kiu kubwa za maendeleo hasa katika nyanja za elimu, afya, maji, uchumi na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo mkazo uliowekwa na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake inatupa matumizi mapya na hamasa kubwa zaidi ya kuongeza jitihada za kuibua na kuchukua hatua zipasazo kuondoa kero mbalimbali kwa matumizi kwamba Serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza pamoja na wahisani wataunga mkono jitihada za wananchi kwa kiasi na kasi kubwa zaidi, bila umangimeza usio wa lazima au kusahau kwamba jimbo la Mkinga liko nyuma kimaendeleo kama zilivyo sehemu nyingi zilizomo pembezoni mwa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada na mafanikio makubwa katika ujenzi na uboreshaji wa barabara na madaraja. Hata hivyo, nimeshangazwa sana kwamba ujenzi wa barabara ya Tanga - Horohoro kwa kiwango cha lami si miongoni mwa barabara zilizoordheshwa katika hotuba yenyewe au kiambatanisho Na. 3 cha hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuamini kwamba barabara hiyo muhimu haikuachwa kwa makusudi bali huenda kosa la uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa ahadi mbalimbali ambazo wananchi wa jimbo la Mkinga wamekuwa wakifuatilia kwa shauku kubwa ni pamoja na kupatiwa nishati ya umeme, mawasiliano ya simu na Wilaya au angalau Halmashauri kwa awamu ya kwanza ili kupunguza usumbufu wa kiutawala na kulisimua maendeleo kwa karibu na urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa ni ya chini sana Wilayani Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tena kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake na hotuba nzuri sana na kumwomba Mwenyezi Mungu ampe afueni ili Watanzania tuzidi kufaidika na uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

tufanye utaratibu wa kueneza elimu ya watu wazima yenye manufaa, *Functional Adult Education* maarifa ya kilimo, ya ufugaji, ya uvuvi, tuweke utaratibu wa elimu ya watu wazima, nchi nzima. Mafanikio ya mikoa ile inaitwa *Big Four*.

Mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati ule. Kazi kubwa tumefanya ni kuwafundisha wananchi kanuni za kilimo bora. Lazima turudi hapo. Pili, lazima vile vile Serikali iweke utaratibu mzuri na mtandao wa kufikisha pembejeo karibu na wananchi. *(Makofi)*

Tusitoe visingizio vya kwamba sasa hivi ni uchumi wa soko, ni shauri ya wafanyabiashara binafsi, hapana. Lazima tuunde mazingira, pembejeo ziwakaribie wananchi, halafu tuwaachie wao wafanye kazi. La tatu, kwa kweli lazima Serikali iweke malengo ya kueneza vitendea kazi vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke malengo hivi tutaingia katika kilimo cha ng'ombe nchi nzima baada ya miaka mingapi? Hivi tutaeneza mikokoteni ili kuwakomboa hasa wanawake kubeba mizigo kichwani kueneza nchi nzima baada ya miaka mingapi? Hatuwezi tukasema sisi hivi tunangoja magari hatutengenezi magari hapa, lazima tufanye kile tunachokiweza. *(Makofi)*

Mwisho Chama Tawala. Chama Tawala kina wajibu mkubwa sana na ni vizuri kukumbushana kwamba cheneyewe ndio chenye Sera, Ilani kwa hiyo, lazima kuhakikisha kwamba sisi wana CCM, viongozi na wanachama wenyewe ndio tunakuwa watekelezaji wa mfano. Kama ni suala la kufanya kazi kwa juhudi na maarifa sisi tujitokeze kuwa mstari wa mbele halafu wengine watuige sisi. Tunao udhaifu kidogo katika hili. Bado tuna watu ambao pamoja na kwamba ni viongozi wa Chama cha Mapainduzi, pamoja na kwamba ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi lakini hawako mstari wa mbele katika kutekeleza na kutetea Sera za Chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami nishiriki kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia mwaka huu wa 2004 katika Bunge letu Tukufu, naomba nianze kwa kutoa salaam za kheri ya mwaka mpya kwako Mheshimiwa Naibu Spika na kupitia kwako salaam kwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Waheshimiwa Watumishi wa Bunge, watumishi wa Serikali wanaotusaidia katika kutekeleza majukumu yetu hapa Bungeni na Waandishi wa Habari. Kheri ya mwaka mpya wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kumpa pole Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba na Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa maradhi yaliyomsibu kwa muda mrefu tukawa hatunaye ndani ya ukumbi huu wa Bunge lakini Mwenyezi Mungu amemjalila amerejea Bungeni na tunamwomba Mwenyezi Mungu amponeshe haraka maradhi yanayomsibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ntoa pongezi kwa Wabunge wa Afrika wanaotuwakilisha sisi kwa ushindi wao wa kishindo, sikushiriki katika kupiga kura lakini nawaunga mkono. Vile vile mwakilishi wetu katika *SADC Parliamentary Forum*, Mheshimiwa Sophia Simba. *(Makofi)*

Pia ntoa pongezi za dhati kabisa kwa mjukuu wangu Mheshimiwa Charles Makongoro Kambarage Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Asha Ngede kwa kuchaguliwa kuwa mwakilishi wetu katika Tume ya Huduma za Bunge. Kura ilikuwa ya siri lakini inaonyesha dhahiri tulijali usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia kwenye mjadala wa hotuba. Nimeshampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini nataka kusema kwa kweli sifa zilizotolewa kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais kama Waheshimiwa Wabunge naweza kusema zaidi ya 99% wamekiri ilikuwa hotuba nzuri sana,

yenye kutoa matumaini na ambayo imejengea heshima Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi katika utekelezaji wake wa Ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo ninaanza nalo ni kuomba vyombo vya habari visiishie katika maneno ambayo Mheshimiwa Rais aliweza kupata muda wa kuyasoma mbele ya Bunge hili. Kwa vile wanaweza kuandika waandike mpaka hata viambatisho. Viambatisho vina maneno mengi mazito sana ambayo yanasaidia kutafsiri mafanikio makubwa ambayo kwa ufinyu wa muda Mheshimiwa Rais hakuweza kusema kila jambo. Amezungumzia mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapiga kura wangu wa Jimbo la Muleba Kusini wamenipigia simu wanasema Wapinzani wanasema barabara ya kutoka Kagoma - Muleba - Rusahunga imefutwa. Kwenye kiambatisho ukurasa wa 94 imeelezwa zabuni za kutengeneza barabara hiyo katika kukamilisha barabara kuu kutoka Dar es Salaam - Mutukula zinatangazwa Februari, 2004. Huo ni mfano tu wa kuonyesha jinsi ambavyo viambatisho vina maneno mazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizungumzie njaa, Mheshimiwa Rais ametuambia tuna fedha za kutosha na tuna imani au tunasifika na wahisani wetu katika jitihada za kuhakikisha chakula kinafika pembe zote za nchi. Nawapa pole wote walioathirika na njaa ikiwa pamoja na wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini. Muleba mvua inanyesha lakini mihogo imeharibika kutokana na maradhi na huko kuna njaa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, tuwahimize Wakuu wa Mikoa na Wilaya washiriki kikamilifu kuleta takwimu sahihi. Rais ameonya kuhusu viongozi waoga. Wawe wajasiri kukiri kuna njaa na kusaidia kupeleka chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Rais kuwapongeza *TRA*. Fedha zinapatikana na tunazitamka hadharani. Serikali ya uwazi. Kwa kweli mimi nilikuwa nashangaa nilipokuwa nasikia Waheshimiwa Wabunge kadhaa humu ndani ya Bunge na viongozi wa kisiasa nje ya Bunge kwamba Mheshimiwa Rais kakwepa kuzungumzia rushwa. Kwa kweli hawamtendei haki Mheshimiwa Rais kutafsiri kwamba kwa kutotumia neno rushwa katika hotuba yake anasema rushwa imekwisha na Tanzania haina tatizo la rushwa. Ukifuatilia hotuba yake mambo ambayo ameeleza, sura tano za mwelekeo miezi 20 iliyobaki, ukurasa wa tatu, la tano ni kupambana au kuendelea kubaini kero za wananchi na kuondoa vikwazo kwa wananchi kujiendeleza. Kero za wananchi ni pamoja na rushwa. Mheshimiwa Rais hawezi kuorodhesha kero zote za wananchi kwenye hotuba. Kitabu hiki kitalingana na sanduku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa kwamba *PCB* sasa hivi ni watafiti tu hawapambani na rushwa hiyo si sahihi. Vijana hawa wa *PCB* wanapambana na rushwa kwa nguvu zote. Wanastahili pongezi na kutiwa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zote zinaonyesha dhahiri Mikoani na Wilayani. *PCB* inayozungumzwa sasa imejengwa na kuimarishwa kwa msaada wa Bunge hili na ndio maana Mheshimiwa Rais anatoa shukrani za dhati kwa Bunge kama mdau ambaye anamsaidia sana kuimarisha Utawala Bora. Mheshimiwa Rais alichagua kutumia maneno Utawala Bora katika hotuba yake na sio rushwa kwa sababu ukizungumzia rushwa tu ni kueleza kwa ufinyu masuala ambayo yanawasibu wananchi wake. Naamini wananchi wanamuelewa Rais wao anapambana na rushwa. Naye anajua bado rushwa ipo na anaikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *PCB* wanaelekea hadi Wilayani. Wakati tunaingia madarakani Awamu ya Tatu, *PCB* walikuwa kwenye Kanda wakihudumia wastani wa Mikoa minne. Sasa wako Mikoa yote. Wamefungua ofisi Wilaya 47. Mwisho wa mwaka huu Wilaya zote zitakuwa na vijana wa *PCB*. Hii nalieza kwa maana kwamba watasaidia sana *PCB* kukabiliana na matatizo ya rushwa hata rushwa za kisiasa iwapo watapewa ushirikiano na wanasiasa wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba *PCB* iondolewe Ofisi ya Rais imenishangaza kabisa baada ya Rais kupewa sifa nzito na kemkem kwamba ni muadilifu na mpambanaji wa rushwa. Kweli haaminiki kusimamia *PCB*? Lakini pendekezo ipelekwe wapi *PCB* hatujalisikia. Nchi nyingi vyombo kama hivi vinakuwa katika ofisi kuu yenye uwezo wa kusimamia ambayo ofisi kuu hiyo inawajibika kwa Bunge. Kwa hiyo, sifungi mjadala wa *PCB* ipelekwe wapi. Lakini hata *PCB* wanashangaa wapelekwe wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwita *General Kamazima* na timu yake waje wasikilize mjadala labda tutaondoka na kazi ya kufanya ya kuchunguza kesi madhubuti, mahsus. Niliposikia ya Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, analalamika ndege ya Serikali ununuzi wake una udanganyifu, nikasema kazi imepatikana. Tulipofuatilia nikakuta ni tatizo la Kiingereza. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaendelea kusikiliza. Sijatoka ndani ya ukumbi huu. Nasikiliza tuhuma mahsus tufuatilie. Maana yake utafiti na uchunguzi ni jambo la msingi, ama sivyo tutamalizia watoto wa watu ndani ya jela eti watu watusikie tuko kazini. Mheshimiwa Isaac Cheyo, akasimama na hoja kwamba CCM imenunua Madiwani wake milioni tatu, tatu. Nikasema kazi imepatikana watu watahughulikiwa. Walipomwambia athibitisha akasema naomba kufuta usemi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni Bungeni ambapo tunapaswa kuzungumza bila woga. Kutaja hata Masilingi anakula rushwa nikashughulikiwa. Sasa hata watani zangu wanasema Rais wasaidizi wake hawamsaidii. Akina nani? Masilingi au nani? Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ni kuanzia Makamu wa Rais mpaka Mwenyekiti wa Serikali wa Kijiji na Afisa Mtendaji wa Kijiji. Nani hamsaidii kupambana na rushwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wale watakaolingia Ikulu tukitoka 2005. Nadhani nitaendelea nimalizie kipindi changu, nawashauri waheshimu uchunguzi na utafiti katika masuala mazito yanayohusu jinai. Ukifunga watoto wa watu miaka mitano na kuendelea ufurahishe mtu, ni dhambi. Halafu himizeni watoto wa watu wajenge nyumba na kulima. Mnaanza kuwatisha watoto ooh, ana mshahara mdogo amejenga, sasa tukae kwenye vibanda ndio tunaonekane ni waadilifu? Watumishi wa Serikali jengeni, jengeni Wabunge, posho hata kama ni ndogo utaeleza hela umezipata wapi lakini kwa Wabunge posho inatosha kujenga nyumba, huo ndio ukweli. Ukibana ukafanya *savings* utajenga na majengo yamejengwa Dodoma na vijijini.

Sasa watumishi walioko Serikalini tunasema ni waadilifu mpaka watakapothibitishwa vinginevyo. Wasitishike, chapeni kazi, Utawala Bora umedhihirisha. Serikali inakusanya hela inatamka. Barabara tunajenga. Je, tukikaa kwenye *cabinet* tukagawana fedha za *TRA* hizi tulizowatangazia tukawaambia wamekusanya kidogo wananchi watajuaje? Ndivyo Serikali isiyozingatia Utawala Bora zinavyoiba. Wanakaa wanagawana. Sisi tunasema hadharani. Tunaweka kwenye mitandao ya dunia nzima makusanyo yetu, matumizi yetu na kama kuna ubadhilifu na wizi tunaambizana tunashughulikiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kijana *DCI* amesema Morogoro akitafsiri *grand corruption* na *petty corruption* yaani rushwa kubwa na ndogo wakasema amesema yao ni ndogo ya wakubwa ndio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliitisha hotuba kwa sababu hatutaki viongozi hasa watendaji wa Serikali wanaogeza vita dhidi ya rushwa kama usanii, aiseme rushwa zaidi waseme yeye ni mwadilifu, huo ni unafiki. Ripoti yake ninayo yeye alieleza tangu mwaka 1995 Askari 1,138 wamefukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema maneno machache rushwa ndogo na kubwa bado zipo lakini hii haina maana kwamba zipo Tanzania tu ni dunia nzima. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo niliitoa kuhusu Bunge kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyotoa hapa Bungeni tarehe 12 Februari, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limejadili hotuba hii kwa ufasaha sana. Idadi ya Wabunge ambao wamechangia katika hotuba hii ni wengi jumla yao ni 81. Waliochangia kwa kusema ni 60 na waliochangia kwa maandishi ni 21. Napenda niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia hotuba hiyo kwa ufasaha mkubwa. (*Makofi*)

Waliochangia kwa kusema hapa Bungeni ni hawa wafuatao Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa

Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya.

Wengine ni Mheshimiwa Abdulkarim Hassan Shah, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Khadija Kusaga, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Raynald Mrope.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru na Mheshimiwa Wilson Masilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Mariam Faki, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Zuhara Shamis Abdallah, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa Dr. Masunga Chegeni na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoshuhudia wote mjadala umekwenda vizuri sana wote wamempongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri yenye upeo mkubwa na mpana kabisa. Hotuba ambayo imesemea sekta mbalimbali, mafanikio yetu na wapi ambapo tumepata matatizo. Maeneo yaliyotajwa katika hotuba na Waheshimiwa Wabunge wamekiri kwamba yamepata mafanikio makubwa ni mengi, huduma za jamii kwa upande wa elimu, afya, maji, barabara, huduma za miundombinu, uchumi kwa upande wa uwekezaji, ubinafsishaji na utawala bora. Lakini pamoja na maeneo yote hayo ambayo yamejadiliwa yenye mafanikio makubwa bado Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana maeneo ambayo bado yana matatizo. Kuna maeneo mengine huduma za jamii bado zinahitajika, huduma za umeme bado zinahitajika, miundombinu bado lakini tatizo kubwa ambalo pia Waheshimiwa Wabunge wote wamelizungumzia ni la upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote, Serikali imeyapokea na tutazikabidhi Wizara zote kwa sababu kwa kweli katika mjadala huu nilikuwa nafikiria kama ingekuwa mwezi wa nne labda kazi yako ya kuendesha Bunge la Bajeti ingekuwa ndogo sana kwa sababu kwa kweli kazi yote imekamilika kwenye kikao hiki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge walioongea wameongea kwa kujielekeza katika hotuba, lakini pia kwa kujielekeza katika matatizo mbalimbali katika Majimbo yao ya uchaguzi ambayo kwa kawaida ndio kazi tunazofanya katika Bunge la Bajeti. Kwa hiyo, nina hakika kabisa tungekuwa karibu na Bunge la Bajeti basi kazi kubwa ingekuwa imekamilika na kazi ya Bunge la Bajeti ingekuwa rahisi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mawaziri wote watapeleleza yote yaliyozungumzwa pamoja na kwamba na wao pia wana wataalam katika Wizara zao ambao walikuwa wanaandika maeneo yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo yanawahusu.

Ningependa nizungumzie maeneo machache sana kwa sababu kwanza mengi kwa kweli yalikuwa ni michango ya kuboresha lakini pili nawashukuru pia wengi ambao wametoa michango ambayo imeweza kujibu baadhi ya maeneo na hii sio Mawaziri tu hata Waheshimiwa Wabunge wapo waliotoa ufafanuzi mzuri sana katika maeneo fulani fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa kifupi sana juu ya suala la chakula, tumelizungumza sana hapa tuligawa hata vitabu lakini tunaendelea kulifanyia kazi. Tunashukuru kwamba katika *Supplementary Budget* ambayo Bunge imeidhinisha tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 20 ili kuweza kununulia chakula. Kwa hiyo, tunaamini kabisa tutaweza kupambana na tatizo hilo lakini pia tatizo lenyewe sio jepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nigusie maeneo mengine machache tu ili kuhitimisha hoja yangu. Eneo la kwanza ambalo ningependa kuligusia ni eneo la rushwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Wilson Masilingi ambaye amelielezea kwa ufasaha sana tatizo hili la rushwa. Nadhani ubishi si kama Tanzania kuna rushwa au hakuna rushwa la msingi ni kama tunapambana na rushwa. Katika dunia yote kuna rushwa ukienda nchi za jirani kuna rushwa ukienda nchi zilizoendelea kuna rushwa la muhimu ni kama tuna mapambano ya dhati dhidi ya rushwa. Katika Tanzania inaonekana kama tuna mwelekeo wa kama unataka kusema usikike, basi dawa ni kusema juu ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Waziri Mkuu sasa miaka zaidi ya nane mfululizo. Katika nchi hii hakuna Wilaya ambayo sijakanyaga, nimetembea nchi hii yote. Ninaelewa sana sura ya rushwa nilipoingizwa madarakani mpaka leo. Kule mwanzoni wakati nikienda kwenye mikutano ya hadhara na kwa wale ambao mnanifahamu huwa ninapenda sana kwenye mikutano ya hadhara kupata maswali ya wananchi. Huko mwanzoni katika maswali 10, maswali 6 yatakuwa juu ya rushwa. Leo ukipata swali moja juu ya rushwa ni sana bahati na watu wanaridhika sana kwamba kwa kweli kuna mapambano ya dhati dhidi ya rushwa. Hatusemi imekwisha, lakini yapo mapambano ya dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limetusaidia pia katika mapambano haya dhidi ya rushwa. Tumetunga sheria mbalimbali, tunajua yale maeneo ambayo yalikuwa yanasumbua sana wananchi, Mahakama za Mwanzo, Polisi na kadhalika. Tumeweka ule utaratibu wa Mabaraza yanayosimamia Mahakama za Mwanzo ambayo yako chini ya DC ambayo yamesaidia sana. Tumetunga sheria za ununuzi wa bidhaa za Serikali, yote haya ni katika kupunguza mianya ya rushwa. Kwa hiyo, kazi kubwa sana kwa upande wa kupambana na rushwa imefanyika. Namshukuru Mheshimiwa Wilson Masilingi, amelielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wachache waliozungumza juu ya rushwa wanasema kwamba tunaamini kabisa Rais wetu ana dhamira ya dhati ya kupambana na rushwa na mimi nashukuru sana angalau mmefikia hapo lakini wanakuja wanasema lakini Wasaidizi wake hatuna uhakika.

Sasa kama unasema tunakusanya kodi vizuri tumetoka shilingi bilioni 25 tuko zaidi ya shilingi bilioni 100 bado hujaamini tu kwamba hapo kuna dhamira ya kupambana na rushwa kwa sababu ili ukusanye kodi ni lazima ukubali wale wanaokusanya kodi wanakataa rushwa. Hatusemi imekwisha lakini angalau juhudi ni kubwa. Miradi yote ya Serikali ambayo inaonyesha mafanikio ni kwa sababu tunapambana sana na suala la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningewashauri sana wale ambao mpaka sasa wana wasiwasi mkubwa wazungumze na wawekezaji. Huko mwanzoni wakati tunaanza uwekezaji kulikuwa na tatizo hilo sana na wanakuambia kwamba tunakwama mahali fulani kwa sababu watu wanataka hiki na kile lakini leo wawekezaji wengi sana wanasema tunashangaa hizi kelele za rushwa kwa Tanzania kwa sababu ni tofauti kabisa na nchi nyingine za Kiafrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wenyewe wanasema na ndio maana leo nchi yetu ni mojawapo ya nchi inayovutia sana wawekezaji. Mapambano ya rushwa ni kigezo kimojawapo cha mafanikio ya uwekezaji. Kuna mambo mengi sana ambayo unaweza kutolea mfano kuonyesha kwamba kwa kweli kuna dhamira ya dhati ya kupambana na rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja ambaye alikuwa na vijana wake watoto wazuri tu majirani wote wanawafahamu ni watoto wazuri, wakitumwa ni watiifu ni watoto wa mfano kabisa lakini yeye mzee akirudi nyumbani kwa nia njema lazima anawafokea sana nyie mtakuwa majambazi, ninyi watu wa aina gani, mtakuja kuwa majambazi ninyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wakipita njiani huyu mtu kila siku anagombeza watoto mtakuwa majambazi. Siku ya siku ilivunjwa nyumba ya mtu, wale watoto wa yule bwana ndio wakawa wa kwanza kuja kukamatwa lakini si majambazi ila yeye kila siku anapiga kelele ya ujambazi nyumbani kwake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Tanzania tusifike hapo. Kama alivyosema Rais kama kuna mambo mazuri tumeyafanya tujivunie, tujipe moyo wa kwenda mbele zaidi kuliko kila siku unadhani nchi hii ina matatizo makubwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, PCB tumeimarisha sana. General Kamazima ameajiri vijana wasomi na amewapeleka mafunzo na tumeongeza sana uwezo wao wa kufanya kazi leo wako mpaka Wilayani na wanafanya kazi nzuri. Sasa tukisema kwamba rushwa ndio inapamba moto nadhani kwa kweli tutakuwa hatujitendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wako waliosema hata tofauti za maisha zinazojitokeza, namshukuru sana Mheshimiwa Aggrey Mwanri, alifafanua hilo. Katika uchumi wowote unaotoka katika mazingira tuliyokuwemo na tunakwenda kwenye uchumi huria, wachumi wako wengi sana hapa lazima zijitokeze hizo tofauti sasa ni kazi ya Serikali kuzidhibiti lakini huwezi kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwana Mwanri kama ni wajamaa hapa nadhani yeye yuko karibu sana na Mzee Kingunge Ngomale-Mwiru, lakini ndiye aliyetupa falsafa hiyo ambayo ni ya kweli. Unapotoa fursa kuna ambao wataziwahi zile fursa lakini kuna ambao watakuwa waoga kwa sababu ya mfumo wa zamani waliouzoa. Wale watakaowahi watafika mbali na lazima uwape nafasi wachache wafike mbali ili uwatumie sasa kufufua uchumi ili kuweza kusaidia wale wengine walioko chini na hiki ndicho tunachokifanya katika nchi yetu.

Tunakuza uchumi bila ya kuwakwaza wale ambao wanatumia fursa hizo, lakini wakati huo huo tuwatumie hao ili kufufua uchumi mzima na kuweza kupata uwezo wa Serikali kuweza kusaidia wale wengine ambao wao ni waoga au hawawezi kutumia fursa hizo kwa sababu mbalimbali. Kwa hiyo, hiyo siyo rushwa. Ukiona wafanyabiashara wanajichomoza si lazima kwamba wamekula au wametoa rushwa, ni kwamba katika hali hii ya sasa ni *opportunities* au fursa zinajitokeza, sasa ni namna gani mtu mwingine ana ule uthubutu wa kuwahi fursa zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa za kisiasa nadhani zimezungumzwa sana hapa. Kuna Mheshimiwa mmoja alisema kwamba sasa tunaweza kupata Marais wanaotengenezwa kwa fedha haramu. Mimi nadhani sisi ndiyo wanasiasa wenyewe, sisi ndiyo Wabunge tulikuja huku kwa kugombea nafasi hizo na nina hakika mwakani tutakwenda tena kugombea nafasi hizo hizo.

Basi sisi tuwe mfano na mstari wa mbele wa kutokufanya hayo. Pale ambapo hayo yanafanyika basi sisi tuwe na ujasiri wa kusema. Ujasiri usiishie tu kuja kufoka kwenye Bunge, tuwe na ujasiri kabisa wa kupambana na rushwa huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naamini kabisa kuna kazi kubwa sana inafanyika. Mimi pia nataka kuwahakikishieni kwamba tutaendelea kufanya kazi hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba kwa miezi ishirini iliyobaki ataendelea kuimarisha hayo na kuongeza kasi kwenye yale ambayo alikuwa anafanya na mimi nina imani kabisa kama yeye alivyokuwa na imani kwamba Serikali itakayokuja itakuwa bado ni ya Chama cha Mapinduzi na itaendelea na kasi hiyo hiyo katika kupambana na rushwa. Rushwa ni vita vya kudumu, rushwa siyo mbio za maili moja kwamba ukifika mwisho basi umemaliza, haiwezekani, rushwa ni vita vya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu mengine machache. Moja, wenzetu wa Upinzani wengine wanakubali kwamba Vyama vyao ni dhaifu, lakini udhaifu kwa kusingizia CCM na wengine wanakataa kwamba si dhaifu. Yupo rafiki yangu mmoja Mheshimiwa Mutungirehi alisema CCM aliyokuwepo yeye siyo hii ya sasa, imebadilika. Sasa CCM haijabadilika, ila yeye alibadilika na mimi nina hakika ataendelea kubadilika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli alichokizungumza Rais mimi nilidhani watu wa Upinzani pamoja na viongozi wenu mngempongeza sana Rais kwa sababu alielezea udhaifu ambao yeye anauona, ambao ni dhahiri. Lakini akasema mimi yaani yeye, mimi ningependa Upinzani ambao una nguvu, lakini *constructive* ambao utasaidia Chama cha Mapinduzi na Serikali visiweze kusinzia. Hivi ulitaka mtu mwema zaidi ya hapo umpate wapi? Anakueleza udhaifu wako na anakwambia jirekebishe ili unipe mimi tabu. Sasa wewe ulitaka umpate wapi zaidi ambaye angekupa mambo mazuri kuliko hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kweli Rais amewasaidieni sana na mimi ningefurahi kama Vyama vyetu vya Upinzani vitakuwa imara. Mimi nina matumaini labda kuna siku vinaweza kuwa. Rais katika hotuba yake ame-*address* Bunge hili lakini kwa Watanzania wote kwa yale yote aliyozungumza. Sasa nyie mkiona tu jambo mnadhani amewasema ninyi, hapana alikuwa anawaambia Watanzania. Sasa inawezekana katika yale aliyokuwa anawaambia Watanzania ninyi yanawagusa zaidi. Lakini sasa dawa siyo kukataa ni kuyakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape tena mfano mwingine, kulikuwa na watu wanacheza bao, kundi tu, unajua bao lina ushabiki. Sasa wengine wanakuja na wengine wanaondoka. Basi mtu mmoja katika wale waliokuwa wanatazama alikuwa na kisu, hapo pembeni kulikuwa na jiwe akaanza kunoa kisu, halafu anazungumza maneno hayasikiki, anaguna guna hivi, lakini kwa kujifanya. Sasa mmoja wa rafiki zake akamwuliza vipi bwana mbona unanoa kisu? Akasema ahaa, leo acha iwe mwisho bwana nimechoka, mimi mtu hawezi kunitafunia mali yangu mimi nakaa tu, hii leo basi itakuwa mwisho tu. Basi katika wale waliokuwa wanacheza bao jamaa mmoja alitimka mbio, hakuambiwa yeye lakini alitimka mbio, akapotea moja kwa moja na yule aliyekuwa ananoa kisu akabaki kucheka. Akawa anasema wala sikuwa najua kama hata kuna mtu hapa ambaye alikuwa ananifanyia ubaya. Sasa kumbe kweli yupo ambaye ananifanyia ubaya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndiyo nasema hii habari ya kujihisi hisi unaweza ukatimka tu mbio kumbe wala jambo halikulengwa kwako. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge muwe na nguvu ya kuhimili haya mambo, mara nyingine wala hayakuelekezwa kwako yameelekezwa tu kwa Taifa. Sasa ninyi kwa sababu mnahisi kuna jambo mlifanya, mnatimka mbio, si vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema Rais ametusaidia sana, amesaidia Watanzania wote, amewasaidia hata wa Upinzani. Kuna suala la Katiba liliguswa hapa kwamba katika mojawapo ya mambo ambapo wanasema hatuna utashi wa kutaka kuimarisha Upinzani ni suala la Katiba kwamba tumesema kuwe na mabadiliko ya Katiba, CCM hamtaki. Mimi nataka Mheshimiwa yeyote awe wa Upinzani au wa wapi, ni lini sisi tumekataa mabadiliko ya Katiba. Hivi kikao kijacho tunaleta Muswada wenye mabadiliko ya Katiba na ni lini Mheshimiwa Mutungirehi ni lini umeleta hoja ya kuleta mabadiliko ndani ya Katiba tukakukatalia. Lete tu, kama una hoja ya kutaka kuleta mabadiliko katika Katiba Waheshimiwa Wabunge hawa watakusikiliza. Kama hoja yako ina mantiki wataipitisha na kama haina mantiki wataipinga, ndiyo kazi tuliyo nayo ndani ya nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali italeta hoja ya kubadilisha vipengele fulani fulani vya Katiba. Waheshimiwa Wabunge watajadili wakiona haina mantiki watakataa, wakiona ina mantiki wataikubali. Sasa ninyi hamwezi kupiga tu kelele mabadiliko ya Katiba, lakini hamleti. Kwa hiyo, jitahidini tu ndiyo maana watu wamewachagua mje hapa kama kuna jambo lolote mnataka kulibadilisha lileteni tutalisikiliza. Kama linafaa sawa, kama halifai sawa. Lakini kama hoja unayozungumza kwa mabadiliko ya Katiba ni Katiba mpya, hiyo tunasema haipo, hiyo hoja hatuikubali kwa sababu Katiba halali tunayo. Kama kuna vipengele katika Katiba ambavyo havikufurahishi vilete, kama tunakubaliana tutavibadilisha, hatukubaliani ndiyo demokrasia na lazima tukubali demokrasia.



Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwamba kumekuwa na tuhuma nyingi sana dhidi ya Polisi hapa. Tuhuma ambazo mimi nasema hazikubaliki, kwamba Polisi inapendelea CCM, Polisi inatumiwa na Chama cha Mapinduzi na kadhalika. Hilo halipo, Polisi wetu ni watu wanaoelewa kazi yao na Majeshi yetu hayana mwelekeo wowote wa kisiasa, lakini Polisi wana kazi ya kulinda usalama wa raia. Kwa kweli kama unafanya mambo ya vituko, Polisi watakushughulikia, hawatajali kama wewe ni wa Upinzani ama ni wa Chama cha Mapinduzi ama huna Chama chochote ama ni raia ama siyo raia. Mradi unafanya vituko ndani ya mipaka ya nchi hii Polisi watakushughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nawaomba sana hasa nyakati za uchaguzi tuache vituko. Ukiona CCM kwa wingi hawakamatwi na Polisi ni kwa sababu wanatii sheria na sisi Chama chetu ndivyo kinavyotuelekeza. Ndiyo maana mara nyingine vijana wa CCM wanakuwa wengi lakini wanapigwa hata na vijana wachache wa Upinzani, hawataki kurudisha kwa sababu ya malezi ya Chama. Tunaomba na ninyi mwingize malezi hayo katika Vyama na mtaona Polisi hatawagusa. Polisi haina mwelekeo wa kusema huyu ni wa CCM ama huyu ni wa Upinzani, Polisi inaangalia usalama wa raia. Kwa hiyo, naomba sana tuwashukuru Polisi wetu, kwa kweli wanafanya kazi nzuri, wanajitahidi sana. Kama siyo hao Polisi kwa kazi wanayofanya mazingira yetu yangukuwa ya ovyo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lililoelezwa hapa la yaliyotokea kule Kata ya Nkoma Bariadi. Tulikuwa na Uchaguzi mdogo wa Diwani wa Kata ya Nkoma. Waliendelea na shughuli zao za uchaguzi. Ndugu Cheyo bahati mbaya hayuko hapa, alieleza mambo mengi sana ukiyasikiliza unaweza ukafikiri pale Polisi na CCM basi kazi yao ilikuwa ni kumaliza watu wa *UDP*, lakini sivyo. Alikuwa anaeleza upande mmoja tu wa shilingi. Kwa taarifa, kilichotokea, kulikuwa na tetesi kwamba mama huyo Christina Mboje, watu walihisi alikuwa na karatasi za kupigia kura. Kulikuwa na mwelekeo wa kutengeneza karatasi za kura, kwa hiyo alikuwa na hizo karatasi za kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi walikwenda nyumbani kwake, wakajitambulisha akasema sina hizo karatasi. Wakasema basi kama utaratibu unavyotaka tunaomba tumpate balozi au mashahidi wawili ili tukague nyumba yako. Yule mama aliposikia hayo alikataa, akatoka nje, akapiga yowe. Watu wakaja, *of course* inahisiwa wengi wao ni wa *UDP*, walianza kufanya vurugu pale, wakamkamata Mtendaji wa Kijiji walitaka kumchoma moto, wakapiga mawe gari na wakataka kumnyang'anya na askari bunduki. Ili kuepusha shari wale wakaingia kwenye gari wakaondoka. Lakini gari ile ikapigwa mawe.

Baadaye ndiyo huyo mama akaja akapelekwa hospitali usiku na Cheyo mwenyewe kwamba eti amepigwa na Polisi kwenye mkutano wa siasa. Hayo ndiyo mambo yaliyotokea. Zipo taarifa za hospitali, alikuwa na maumivu gani au alikuwa na nini, jambo hili inashughulikiwa na Polisi. Lakini Mheshimiwa Cheyo hakueleza mengine yaliyotokea. Pia tarehe 10 yupo bwana mmoja anaitwa Minda Lugesha alikamatwa na Katibu Tarafa baada ya kumchoma kisu mwanachama wa CCM katika mkono. Ndiyo na kisu kipo Polisi kwa ushahidi. Lakini pia bwana Mtei Paul alikamatwa na galoni ya petroli akiwa na wenzie wakitaka kuchoma jengo la *World Vision* ambalo ndilo lilikuwa limewahifadhi watu wa CCM. Haya yote hakusema. Lakini pia nyumba ya bwana Mgembe Nyesi ilipigwa mawe, huyo bwana walimtumumu kwamba ndiye aliwaelekeza wale Polisi nyumbani kwa Christina kwamba nyumba ya Christina ni ile pale. Basi usiku wakaja, wakapiga nyumba yake mawe. Lakini bwana Joseph Paul ambaye ni Katibu Mwenezi wa Kata ya CCM alipigwa pia kisu kwenye shavu, tarehe kumi na kesi imefunguliwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Bwana Lyabuyenza, Katibu Mwenezi wa CCM wa Wilaya naye pia alipigwa na wafuasi wa *UDP*. Sasa ndiyo nasema tusije tuka-*dramatize* tu jambo fulani mengine yote tunayaacha, kwa sababu kama tunataka kutoa picha halisi kwa wananchi basi tuwape picha kamili. Sasa vituko vya namna hii Polisi wakichukua hatua mnasema kwamba Polisi wapo na CCM, hapana, Polisi wanapambana na raia wabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wa CCM wakifanya vituko wanakamatwa tu. Polisi haikuulizi wewe ni wa Chama gani. Kwa hiyo, nawaombeni sana tuvumiliane, ndiyo kazi ya siasa, bado mpo wachanga lakini matumaini yetu mtakua tu. Kwa hiyo, wanasema CCM haina utashi wa kisiasa, mara inanunua Madiwani shilingi milioni tatu, Madiwani 14 wa Bariadi waliotoka CCM. Hivi kweli, iwanunue milioni tatu kila mmoja kwa sababu gani? Sisi tuna asilimia 98 ya Madiwani katika nchi hii.

Kwa nini tukawanunue hawa wachache waliobaki asilimia mbili, wa kazi gani? Tatizo ndiyo hilo hilo, mnafanya vituko mpaka watu wenu wanawakimbia, halafu mnasema CCM wamewanunua. Hivi Danhi Makanga kuna mtu hata alimwambia aje CCM, si walimtimua wenyewe, wamemfukuza wenyewe, walimtoa wenyewe, kwa sababu alikuwa na wafuasi wengi na Madiwani nao wakasema kama wewe umefanyiwa hivi je, sisi? Basi afadhali twende wote, wakamfuata. Ninyi mnaituhumu CCM. Jamani, Waswahili wanasema mbaazi ikikosa maua husingizia jua, ndiyo kawaida hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuwahakikishia, Chama cha Mapinduzi wala Serikali yake haina dhamira hata kidogo ya kupuuza Upinzani wala kuunyanyasa lakini ikafanya shughuli zote ili shughuli za siasa ziende sawa. Chama cha Mapinduzi ni Chama cha Siasa kama ilivyo *TLP* ya kwako, CHADEMA, *CUF*. Kwa hiyo, CCM inapofanya kazi yake ya siasa, mimi nilifikiri kama CCM inafanya kwa mafanikio basi hivyo Vyama vingine ambavyo bado ni vichanga vinatakiwa viige kutoka kwa CCM siyo ukiona CCM inafanya vizuri basi unaituhumu, hapana. Kuna mengi sana ambayo mtajifunza na kama alivyosema Rais na sisi tunataka upinzani wenye nguvu. Upinzani ambao tutakuwa na matumaini nao, siyo wa kulalamika tu kila siku hata pale ambapo hakuna sababu ya kulalamika. Kwa hiyo, Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kitaendelea kuimarisha mfumo wetu wa demokrasia ya siasa katika nchi yetu. Wala hatuna dhamira yoyote ya kuuu Upinzani, hatuna sababu. Tunataka kuuimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri baada ya mambo haya machache niliyoyasema, nimalizie tu kwa kusema hotuba ya Rais imetuzindua sana lakini kuna mambo makubwa ametusisitiza ambayo ni lazima kwa kweli tuyazingatie. *Reforms* zetu za uchumi ndizo zilizoleta mafanikio haya yote. Naomba sana wote tusimamie jambo hili tuhakikishe *reforms* zetu zinakwenda kama tulivyopanga, urekebishaji wetu wa uchumi unakwenda kama tulivyopanga bila ya kubeza. Lakini pale ambapo matatizo yanajitokeza tuyashughulikia jinsi yanavyojitokeza kwa sababu katika mfumo wowote hata ulioendelea sana, hasa mambo haya ya uchumi hakuna ambalo linakwenda bila *corrugation*, bila matuta. Lakini ukikutana na matuta, dawa siyo kugeuza gari bali ni kuyavuka taratibu ili uweze kuendelea na safari.

Mimi nina hakika chini ya uongozi wa Rais Mkapa kama alivyosema, nina hakika ndege yetu hii ya uchumi na hali ya maisha ya Watanzania ataiacha ikiwa angani na nina hakika rubani atakayeipokea kwa sababu atakuwa huko huko angani, hataweza kuiteramsha, ataendelea kuipeleka ili iweze kufikia kwenye *hit* inayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Hoja ya Kuijadili Hotuba ya Rais Bungeni ilipitishwa na Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kufikia hapo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 06.52 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**ND. KIPENKA M. MUSSA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Nne, sasa zimemalizika.

#### **HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumehitimisha shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu. Pamoja na kuwa leo ndiyo siku ya mwisho ya shughuli zetu, naomba nitumie fursa hii kuwatakia Waheshimiwa Wabunge wote heri ya mwaka mpya, 2004. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na nguvu. Huu ni mwaka wenye changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na upungufu wa chakula unaotokana na hali mbaya ya hewa ambayo bado haitupi

matumaini mazuri. Lakini kama ilivyokuwa kwa mwaka 2003, tutumie akili, vipaji tulivyopewa pamoja na raslimali zetu kukabiliana na changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nami nimpongeze Mheshimiwa Asha Ngede kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Huduma za Bunge anayewakilisha Kambi ya Upinzani. Sote tuna imani kuwa ataungana na Makamishna wengine katika kuendelea kuimarisha Taasisi hii ya Bunge ili iwe chombo madhubuti cha uwakilishi na chenye kuonesha taswira halisi ya demokrasia nchini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nirudie pongezi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kutuwakilisha katika vyombo muhimu vya Bunge la Afrika na katika *forum* ya Wabunge wa Nchi za *SADC*. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kujiunga nasi katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huu jumla ya maswali 187 ya Waheshimiwa Wabunge yamejibiwa na mengine mengi ya nyongeza. Aidha, Miswada 5 imepitishwa pamoja na Maazimio 6. Waheshimiwa Wabunge wamekubali na kuridhia Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza, kwa Mwaka 2003/2004 kama yalivyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huu wa Bunge pia umepata bahati ya kuhutubiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 12 Februari, 2004. Napenda tena kwa niaba yenu wote Waheshimiwa Wabunge nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa hotuba yake nzuri sana na yenye upeo mpana. Nina hakika Watanzania wote wamefaidika na hotuba hiyo ambayo imeweka bayana hali ya nchi yetu ya sasa na kuwapa matumaini makubwa ya huko tunakoelekea na kutaka kufika. *(Makofi)*

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wameipokea na kuijadili hotuba hiyo kwa makini sana. Naomba kwa mara nyingine tena niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mizuri na ushauri mlioutoa kwa Serikali wakati wa kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge hili Tukufu. Kama nilivyoahidi wakati nahitimisha mjadala huo, Serikali itaendelea kusimamia sera, mipango na mikakati iliyojiwekea yenye lengo la kuendeleza kwa kasi kubwa zaidi mafanikio tuliyonayo hivi sasa. Bunge hili ni sehemu ya mafanikio tunayoyashuhudia katika nchi yetu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kushirikiana na Bunge lako Tukufu ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi zilizofanywa na mkutano huu ni kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Nyongeza kwa mwaka wa 2003/2004. Kama alivyoeleza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Makadirio haya yameletwa na Serikali kwa lengo la kuiwezesha kukidhi mahitaji ya lazima ambayo yana udharura na hayakwepeki katika muda mfupi ujao. Kama taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilivyoonyesha mahitaji haya hayatokani na udhaifu wa Serikali katika kukusanya kodi na kufikia malengo yake. Kwa hakika ukusanyaji wa mapato ya Serikali umevuka lengo la miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2003/2004 na kwa mwenendo tulionao, hatutegemei kuwa tutashindwa kufikia malengo ya mwaka 2003/2004 tuliyojiwekea katika Makadirio ya Bajeti yetu. Ndiyo maana Serikali haikufikiria kuleta mapendekezo ya mabadiliko ya kodi mpya kama njia ya kupata nyongeza hiyo ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipohutubia mkutano huu wa Bunge, Mheshimiwa Rais alieleza uchumi wetu hivi sasa ni nyumbulifu na endelevu na kwamba unao uwezo wa kuhimili mikikimikiki kama tuliyonayo hivi sasa inayosababishwa na hali ya ukame. Moja ya eneo muhimu sana ambalo tutalishughulikia kutokana na nyongeza ya fedha ambazo Bunge lako Tukufu limeidhinisha ni tatizo la upungufu wa chakula. Hivi sasa hali ya hewa katika maeneo mengi nchini bado haijawa nzuri ya kuridhisha. Yapo maeneo ambapo mazao yameanza kunyauka na yapo maeneo mengine ambayo bado wakulima wamesita hata kuanza kupanda kwa vile dalili za mvua kunyesha hazileti matumaini makubwa. Fedha hizi zilizoidhinishwa na Bunge zitatumika katika kuongeza akiba ya chakula katika Akiba ya Taifa ambayo hivi sasa imepungua sana kutokana na mahitaji makubwa ya chakula kutoka sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza hali ya upungufu mkubwa wa chakula katika maeneo yao kwa uchungu mkubwa. Lakini wapo pia baadhi ambao wameeleza kutoridhika kwao na juhudi zilizochukuliwa na Serikali. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali katika suala la upungufu wa chakula haijasinzia wala kupumzika. Kama siyo juhudi kubwa iliyoifanywa na Serikali, leo hali ingelikuwa tofauti sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha tukumbuke kuwa sura ya hali hii inabadilika siku hadi siku na hasa baada ya mvua za vuli nazo kutokunyeshwa katika maeneo mengi mwaka huu. Katika makisio ya awali, ilitegemewa Wananchi wasiojiweza wangehitaji tani kama 77,000 za chakula, ambapo tani 32,000 zingetoka Serikalini na tani 45,000 zingetoka kwa wahisani mbalimbali hasa kupitia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*). Upungufu mwingine ungejazwa na chakula cha biashara kutoka Akiba ya Chakula cha Taifa (*SGR*) na wafanyabiashara binafsi ambao hadi sasa wameondolewa kodi zote katika uagizaji wa mahindi na mchele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika taarifa tulizosambaza, mpaka sasa zaidi ya tani 17,000 za mahindi kutoka Serikalini kwa wale wasio na uwezo zimegawanywa katika Wilaya 66 nchini. Ili kusambaza chakula hicho Serikali imetoa jumla ya Shilingi milioni 870 kwa Halmashauri husika kama gharama za kuchukulia chakula hicho kutoka vituo vya *SGR* hadi wilayani. Hivi sasa mgao mwingine wa zaidi ya tani 14,000 kwa hao hao wasio na uwezo umekwishaandaliwa. Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*) nalo limegawa zaidi ya tani 10,000 katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Tabora na Iringa. Aidha, juhudi pia zimefanywa za kusambaza chakula cha biashara katika maeneo mbalimbali yenye shida. Akiba ya Chakula cha Taifa (*SGR*) mpaka sasa imeza zaidi ya tani 29,000 na wafanyabiashara binafsi nao wameingiza zaidi ya tani 330,000 za nafaka za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizi za kusambaza chakula, Serikali kwa kushirikiana na nchi wahisani hasa kwa kupitia Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) imesambaza mbegu za mahindi tani 391, mbegu za maharage tani 122.5, mtama tani 287 na mpunga tani 65 ambazo zimegawanywa katika maeneo yenye shida. Sambamba na hilo, Serikali pia imegawa Shilingi milioni 120 kwa Mikoa 13 iliyotoa maombi kwa ajili ya mbegu za mazao ya ukame hasa mihogo na mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo hali ya hewa itaendelea kuwa ya wasiwasi ni wazi kuwa hali ya upatikanaji wa chakula kwenye masoko ya mijini na kwa Wananchi vijijini itaendelea kuwa ya matatizo. Bado Serikali inaendelea kuwahimiza wafanyabiashara kuagiza chakula na kukifikisha kwenye masoko karibu na walaji na vilevile kutumia akiba yake kila inapobidi kama njia ya kupunguza makali ya bei, lakini vilevile kuwasaidia wale walioathirika zaidi. Uzoefu tulioupata katika miezi michache iliyoipita ni kuwa, bado wapo baadhi ya Watendaji wa Serikali ambao ni wazito katika kutoa maamuzi au hata kuchukua hatua zinazopasa katika kushughulikia mahitaji ya chakula katika maeneo yao. Napenda nitumie fursa hii kuwataka watendaji wachache wa aina hiyo kuwa uwezo wa Serikali wa kusambaza chakula cha njaa unategemea sana watendaji wake katika ngazi zote za Serikali. Hivyo kila mmoja wao atimize wajibu wake katika suala hili la chakula. Atakayezembea katika usimamizi wa chakula atachukuliwa hatua kali sana bila ya huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuongezewa uwezo wa kukabiliana na tatizo hili, lipo pia suala la Wananchi wenyewe kutumia mvua zinazoendelea kunyeshwa katika baadhi ya maeneo nchini kwa kulima mazao yanayostahimili ukame. Bado baadhi ya wakulima katika maeneo yanayopata mvua chache wanapanda mazao yasiyostahimili hali hiyo kama vile mahindi, badala ya mazao yao ya asili na yanayostahimili mvua chache kama vile mihogo, viazi, mtama, uwele na kadhalika. Pamoja na Viongozi wa Kitaifa kuisisitiza suala hili, bado usimamizi wake ni dhaifu sana katika maeneo mengi. Wataalamu wa Kilimo na wale wa Maendeleo ya Jamii wanahitajika kuwafikia wakulima vijijini kwenye mashamba yao na kuhakikisha kuwa suala la kupanda mazao yanayostahimili mvua chache linazingatiwa. Hili siyo suala la hiari tena ni suala la kufa na kupona. Aidha, maeneo ya mabonde na yale yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji yatumiwe kikamilifu. Ni lazima angalau maeneo yale ambayo bado yana matumaini ya kupata mvua, Viongozi na Wataalam waimarishe usimamizi na uhamasishaji wa Wananchi ili tuweze kuziba pengo la mahitaji makubwa ya chakula msimu unaoendelea na ule ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za kitaalam zinaonesha kuwa hali ya mvua na maji itaendelea kuwa mbaya hasa katika nchi za Afrika kadri miaka inavyosonga mbele na uharibifu wa mazingira unavyoendelea. Kinachotakiwa sasa ni wakulima kujizatiti katika kilimo cha kisasa chenye tija na kisichoharibu mazingira. Ni vema tukarudi kwenye utaratibu wa kulima mazao yanayostahimili hali ya hewa na tukajiwekea akiba katika ngazi ya kila kaya. Nataka nitahadharishe kabisa kuwa, mawazo yanayojengeka kuwa ukame ukitokea tunadhani Serikali italisha watu wote kwa kugawa chakula, si endelevu. Itafikia wakati Serikali itashindwa na watu wataathirika sana au hata kupoteza maisha. Kilimo kisimamiwe kwa misingi hiyo na hifadhi ya chakula kwa njia za asili ifanywe katika kila kaya. *(Makofi)*

Leo ukisafiri mkoani Dodoma, Singida, Shinyanga na maeneo mengine ya ukame utoana watu wamelima sana, lakini wote wamepanda mahindi ambayo kwa asilimia kubwa sote pamoja na wakulima wenyewe tunajua hawatavuna na tayari yameanza kunyauka. Waliopanda mtama, uwele, ulezi hata mwaka jana walivuna na mwaka huu wataavuna. Nataka nikumbushe tena kuwa, ni aibu kwa Taifa kutokuweza kujilisha na vivyo hivyo ni aibu kwa mtu kushindwa kulisha familia yake. Wajibu wa kwanza wa kulisha familia ni wa mkuu wa familia husika. Serikali itajitahidi kutimiza wajibu wake, lakini Wananchi nao lazima watimize wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huu, Bunge lako Tukufu limekubali na kuidhinisha matumizi ya ziada kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi waliofaulu kujiunga na masomo ya sekondari. Kama ambavyo idadi ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi imekuwa ikiongezeka, idadi ya wanaofaulu darasa la saba pia imekuwa ikiongezeka, yote haya yakiwa ni matokeo ya mafanikio mazuri ya mpango wetu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatupa changamoto ya kujenga zaidi shule za sekondari ili vijana wanaofaulu wapate nafasi za kuendelea na masomo. Kazi hii itahitaji ushirikiano wa karibu baina ya wadau wote yaani Serikali, Madhehebu ya dini, asasi mbalimbali, watu binafsi na Wananchi wenyewe. Ni vyema basi Viongozi na Watendaji katika kila ngazi ya utawala na uongozi nchini watambue matokeo hayo na kuanza sasa kuwahamasisha Wananchi washiriki katika ujenzi wa shule za sekondari kwa nguvu zaidi.

Kwa upande wake, Serikali ipo katika hatua za kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MEM) ambao kama ulivyokuwa ule wa elimu ya msingi utahitaji rasimali kutoka kwenye Bajeti ya Serikali na mchango mkubwa wa Wananchi na wadau wengine wa maendeleo yetu. Ningependa kuwataarifu Wananchi kuwa, kama ilivyokuwa kwa mradi wa MEM, watakaofaidika zaidi ni wale ambao watakuwa wamejizatiti katika ujenzi wa shule zao za sekondari. *(Makofi)*

Napenda nirudie sehemu hiyo. Ningependa kuwataarifu Wananchi kuwa, kama ilivyokuwa kwa mradi wa MEM, watakaofaidika zaidi ni wale ambao watakuwa wamejizatiti katika ujenzi wa shule zao za sekondari. Hao watapata mchango wa MEM ili kukamilisha majengo yao, lakini ambao hawakufanya lolote, hawatafaidika na mpango huo. Ni vema sote na hasa sisi Waheshimiwa Wabunge tukawahamasisha wapiga kura wetu ili watoto wetu wanufaike na mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu pia limetupa uwezo mkubwa zaidi kifedha wa kuanza maandalizi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kasi ya utekelezaji wa jukumu hilo sasa iweze kuwa kubwa zaidi. Matayarisho ya daftari hili hayapo kwenye upatikanaji wa vitendea kazi tu, bali ni pamoja na wadau wote kushiriki kikamilifu katika hatua zote.

Lipo pia suala la kuwaelimisha na kuwahamasisha Wananchi wakubali kushiriki katika zoezi hili. Nchi yetu inao uzoefu wa Wananchi kushiriki katika mazoezi yanayofanana na zoezi hili. Tumeendesha zoezi la sensa kwa mafanikio ya hali ya juu ambayo yamewashangaza hata baadhi ya wadau wetu wa maendeleo.

Kwa msingi huo, naomba nitoe wito maalum kwa Watanzania wote kuwa, zoezi la kuandaa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni zoezi muhimu sana katika kuimarisha demokrasia na utawala bora nchini. Kuandikishwa kupiga kura ni wajibu na ni haki ya kila Mtanzania mwenye sifa zinazohitajika kufanya hivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda kuwataka Wananchi wote wenye sifa hizo wajitokeze kujiorodhesha kwenye daftari hilo mara zoezi litakapoanza. Ni vyema Wananchi waelewe tofauti iliyopo kati ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na utaratibu ule tuliozoea wa kuandikishwa kupiga kura. Daftari hili zaidi ya kurahisisha kazi ya uchaguzi, litaondoa usumbufu hata kwa Wananchi na litaondoa uwezekano wa watu kujiandikisha zaidi ya mara moja na vivyo hivyo kupiga kura zaidi ya mara moja. Hili ni jambo muhimu sana kwa kukuza demokrasia yetu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuwasaidie Wananchi kuelewa umuhimu wa zoezi hili na kuwahamasisha washiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria ya Kukabiliana na Bidhaa kutoka kwa Wawekezaji wenye nia ya Kuuu Ushindani wa Ndani wa mwaka 2003. Muswada huu utakapokuwa Sheria utatusaidia kujenga mazingira bora ya ushindani wa bidhaa katika soko letu la ndani. Kama nilivyoieleza wakati wa semina iliyoandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kutuelimisha juu ya jambo hili, sheria haitalinda bidhaa ambazo ni duni na zisizokidhi matakwa ya walaji kwa ubora.

Aidha, katika mazingira ya utandawazi na kwa kuzingatia Mikataba ya Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia, hatuwezi kufunga soko letu kwa bidhaa zinazotoka nje ambazo zinaingia kihalali na zinakidhi ubora unaohitajika.

Kwa msingi huo, kupitishwa kwa Muswada huu kunatoa changamoto kwa wenye viwanda nchini kuwa ni lazima wajizatiti kikamilifu kuzalisha bidhaa bora, kupunguza gharama za uzalishaji, lakini vile vile, kutangaza bidhaa zao na kuweka mtandao wa soko hadi kwa Wananchi walio wengi vijijini. Changamoto nyingine ipo kwa Wananchi ambao ndio watumiaji wa soko la bidhaa za ndani na nje. Tupende bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwani kupanuka kwa soko la bidhaa hizo kutaongeza ajira ya Watanzania wengi zaidi; kutasaidia vile vile kuingizwa kwa teknolojia mpya kwenye viwanda hivyo na kuongeza mapato mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasimili kuu ya Wananchi wengi wa nchi yetu. Kwa zaidi ya asilimia 85 ya Wananchi, ardhi ndiyo inayowapa matumaini ya kuweza kupambana na umaskini. Muswada wa Sheria ya Kufanya Mabadiliko katika Sheria ya Ardhi wa Mwaka 2003 una madhumuni ya kuwawezesha Wananchi kutumia ardhi yao kama kitega uchumi kitakachowawezesha kupata mikopo ili wawekeze na hivyo kupambana na umaskini. Sote tunaielewa kuwa mikopo ikitumiwa vizuri huwa ni chanzo kimojawapo cha kuwezesha uwekezaji iwe kwa mwananchi wa kawaida, taasisi au nchi. Mabadiliko haya yaliyopitishwa na Bunge hili Tukufu kwenye Muswada huo, yanatambua ardhi kama ni mali isiyoundosheka na ambayo inaweza kutumiwa na mwananchi yeyote kuweka rehani kama dhamana ili aweze kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mabadiliko haya yanaletwa Bungeni, wapo baadhi ya Wananchi na makundi mbalimbali yaliyoonesha kuwa mabadiliko haya yanaweka mazingira ya kuwezesha ardhi ya Wananchi kuchukuliwa kwa urahisi na vyombo vinavyotoa mikopo. Ukweli ni kuwa, ardhi inayohusika siyo ya Kijiji au ardhi ya Jumuiya, bali ni ardhi au hata nyumba yenye hati ya mtu au familia ambao kwa hiari yao wanataka mkopo ili waendeleze maisha yao.

Hata hivyo, ili mali hiyo hasa kama ni nyumba ya kuishi au ardhi ya kilimo ya familia iwekwe rehani, ni lazima kwanza ridhaa ya mume na mke ipatikane. Aidha, kama watahinda kulipa mkopo, mali kama hiyo ina utaratibu mgumu wa kuiiza ambapo ni lazima wafike mahakamani na mahakama itoe idhini ya mauzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lililo dhahiri ni kuwa benki zilikuwa hazikopeshi Wananchi kwa dhamana ya nyumba za kuishi au ardhi kwa sababu kwa sheria zilizopo, ilikuwa vigumu sana wakopaji hao kuuza nyumba za kuishi au ardhi zilizowekwa dhamana. Dhamana hizo zilipokataliwa, ilijenga hisia kuwa benki za kigeni zilikuwa zinabagua katika utoaji wa mikopo kwa kuwakopesha tu watu wenye biashara kubwa wengi wao wakiwa wageni wa kutoka nje na kuwanyima Wananchi wa kawaida. Hivyo, lengo la mabadiliko haya ni kuwasaidia Wananchi wetu wakopesheke kwa kutumia rasimili waliyonayo ambayo ndiyo ardhi yao.

Jambo la msingi ambalo Viongozi na Watendaji hatuna budi kulifanya sasa kwa nguvu sana ni la kutoa elimu kwa Wananchi ili waelewe maana na madhumuni ya mabadiliko hayo. Sio hilo tu, ni lazima elimu hiyo iwasaidie kutambua kuwa mkopo siyo msaada bali ni fedha zinazotakiwa kurejeshwa na kwamba asiporejesha ardhi yake au mali yake nyingine aliyoiweka rehani itachukuliwa na hivyo kumletea matatizo zaidi katika maisha yake.

Kama alivyoahidi Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Gideon Cheyo, wakati anahitimisha hoja yake, Serikali kupitia Wizara yake na kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali itaongoza jukumu hili la kuelimisha jamii kuhusu sheria hiyo. Wanaotaka kutumia ardhi yao kwa kupatiwa mikopo sasa fursa wanayo, lakini pia wafahamu kuwa fedha za namna hiyo zitumike tu kwa mradi uliokusudiwa na lazima fedha za mkopo zilipwe kwa kadri ya makubaliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ardhi ina thamani ni vyema vile vile tuitunze. Bado uharibifu wa mazingira ni mkubwa nchini. Bado Watanzania wengi hatujawa na mwamko wa kutunza mazingira kwa kupanda miti, kuzuia uchomaji ovyo wa mioto na kadhalika.

Kwenye baadhi ya maeneo, wapo baadhi ya Wananchi wanalima kwenye milima bila hata kuweka makingamaji na hivyo kusababisha mmomonyoko mkubwa wa ardhi. Tuendeleo kuwahimiza Wananchi kuitunza ardhi na kupiga vita kwa nguvu zote shughuli zozote zenye kuchafua au kuharibu mazingira. Tukumbuke pia thamani ya ardhi zetu zitapishana sana kutegemeana na jinsi ardhi ilivyotunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uharibifu wa mazingira limechangia pia kwa sehemu kubwa kukauka kwa vijito na hata mito inayoingiza maji kwenye mabwawa muhimu kama bwawa la Mtera ambalo hutumika kuzalisha umeme wa gridi ya Taifa.

Kupungua kwa maji kwenye bwawa hili la Mtera sasa kumeanza kuwa jambo linalojirudia kila baada ya muda mfupi kuliko ilivyotarajiwa. Tusipochukua hatua za kulilinda na kulinda vyanzo vya mito na vijito vinavyoingiza maji kwenye bwawa hilo wakati wote wa mwaka itafika wakati litakauka kabisa. Kupungua kwa maji kwenye bwawa hilo na mengine yanayotumika kuzalisha umeme kumesababisha uzalishaji umeme kwa maji kupungua sana nchini.

Kwa kuelewa athari za upungufu wa umeme kwa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, Serikali imechukua hatua za kuliwezesha Shirika la Umeme (*TANESCO*) kununua umeme wote unaozalishwa na Kampuni binafsi ya *IPTL* ya Jijini Dar es Salaam na vile vile kununua mafuta ya kuendesha mitambo ya gesi iliyoko Ubungo, Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzigo huu wa kutoa ruzuku kwa *TANESCO* ni mkubwa sana kwa Bajeti ya Serikali. Lakini kama Serikali isingechukua uamuzi huo ni wazi mgao wa umeme ungeanza na hivyo kuathiri uzalishaji viwandani, uchumi wetu, ajira na huduma nyingine. Tumesikia taarifa ya Waziri wa Fedha kuwa makusanyo ya mapato ya ndani katika kipindi cha miezi sita ya Julai-Desemba 2003 yalifikia shilingi 713,511 milioni ambazo ni asilimia 2 zaidi ya lengo la kukusanya shilingi 699,354 milioni katika kipindi hicho. Makusanyo haya yamewezekana kwa sababu shughuli za uzalishaji na utoaji huduma hazikusimama kutokana na ukosefu wa umeme. Kwa msingi huo, ni busara kuendelea na uamuzi huu na napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kukubali kupitisha maombi hayo ya fedha za ziada kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa *TANESCO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na itayafanyia kazi. Hata hivyo, naomba tu nigusie jambo moja ambalo limezungumziwa kwa nguvu sana nalo ni mradi wa Mchuchuma. Serikali inakubaliana sana na ukweli kuwa ni hatari kutegemea tu umeme unaotokana na maji na ndiyo maana Serikali iliwekeana mkataba wa awali na wanaotaka kuwekeza katika mradi wa Mchuchuma na Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara kwa ujumla.

Hivyo ni wazi kuwa Serikali haina nia yoyote ya kuukwamisha mradi huo. Tunachotaka kujiridhisha nacho ni gharama mbalimbali zinazohitajika ili umeme huo usiwe mzigo kwa uchumi, Bajeti ya Serikali au mtumiaji. Hata hivyo, nakubali uchambuzi huo umechukua muda mrefu. Hivyo,

ninawaagiza Waziri wa Nishati na Madini kwa kushirikiana na Waziri wa Ujenzi, wahakikishe Bunge hili linapata taarifa kamili ya mradi huo wakati wa Mkutano wake wa Kumi na Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku chache zijazo Marais wa nchi tatu za Jumuiya ya Afrika Mashariki watatia saina Mkataba wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Utiaji saina mkataba huo unazidi kuimarisha umoja wetu wa Afrika Mashariki kwa kuwa na soko la bidhaa lililoainishwa kwa uwiano uliokubalika baina ya nchi zetu tatu, yaani Kenya, Tanzania na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia ya sasa ya utandawazi, ushindani mkubwa na matumizi ya teknolojia ya kisasa, nchi ndogo ndogo na maskini kama zetu zinaweza tu kushindana kwa kuungana pamoja. Kwa kuungana pamoja nchi zetu za Afrika Mashariki zitakuwa na sauti kubwa zaidi katika masoko ya dunia na pia kuwa na soko pana zaidi la kwetu wenyewe. Kwa kuungana huko tutakuza uchumi wa eneo letu na hivyo manufaa kwa kila mmoja wetu. Hata hivyo, wapo watu wenye wasiwasi mkubwa na hatua hii. Wanachohofu ni kuwa viwanda vyetu vitauawa na bidhaa kutoka nchi za Afrika Mashariki zenye viwanda kuliko sisi. Ningependa kulikumbusha Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa suala hili limewekewa utaratibu hasa katika miaka ya mwanzo ambapo bidhaa za kutoka Kenya bado zitalipa ushuru zikiingia katika soko la Tanzania au Uganda. Katika muda huo wa miaka mitano inatarajiwa zile nchi zilizo nyuma zitakuwa zimejizatiti kufikia viwango vizuri vya uzalishaji viwandani. *(Makofi)*

Aidha, tukumbuke kuwa hata hizo nchi zilizo nyuma kiuzalishaji viwandani, zina maeneo ambapo nao wana unafuu kuliko zile zilizo mbele zaidi. Kinachotakiwa sasa ni kila nchi kutumia unafuu, fursa au umaarufu ilionao na kwa kuhimiza wananchi wake kufanya kazi kwa bidii na kuzalisha bidhaa bora kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kwa Waheshimiwa Wabunge ya tarehe 12 Februari 2004 aliwaambia Watanzania kuwa kazi ya Serikali ni kujenga fursa za kila mtu kupambana na umasikini. Kusaini mkataba wa umoja wa forodha ni fursa nyingine ya aina hiyo. Maana yake ni kuwa, Mtanzania sasa ataweza kuuza bidhaa zake Kenya na Uganda bila kutozwa ushuru ili mradi bidhaa hiyo imetengenezwa Tanzania. Cha kushangaza ni kuwa Watanzania tunalalamika kuwa nchi yetu itakuwa soko badala ya kuona kuna fursa sasa ya soko kubwa zaidi la kuuzia bidhaa zetu. Kwa nini sisi ndiyo tu tujione wanyonge badala ya kutumia fursa hizi kwa manufaa yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya soko la pamoja la bidhaa za Afrika Mashariki baadaye itayakumba maeneo mengine ikiwa ni pamoja na ajira. Wafanyakazi wetu wanatakiwa waanze kuchukua tahadhari kuanzia sasa. Kama tija ya wafanyakazi wetu ni ya chini kuliko wafanyakazi wa nchi zingine au nidhamu zao ni za ubishi na migomo, wenye ajira hata wangukuwa Watanzania wataajiri wafanyakazi kutoka Kenya au Uganda ili mradi wanapata tija kubwa zaidi kwa usumbufu mdogo. Ni vema Watanzania tukayaelewa mazingira haya ya biashara ya kisasa. Ni lazima twende na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake alizungumzia sana juu ya kujenga uchumi endelevu kwa bidii, lakini pia kukubali mazingira ya uchumi wa kisasa. Alisisitiza sana suala la umuhimu wa mitaji. Sera yetu ya urekebishaji wa uchumi *(Economic Reform Policy)* inajikita sana katika kuingiza mitaji, teknolojia na menejimenti ya kisasa ikiwa ni pamoja na ujuzi wa masoko katika uchumi. Kwa hiyo, ni lazima tuendeleo kuwavutia wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na viwanda, kilimo, madini, utalii na kadhalika. Uwekezaji wowote uwe wa nje au wa ndani lazima una mahitaji yake maalum hasa kama wawekezaji hao wanagombaniwa na nchi nyingi na hivyo ndivyo ilivyo. Kama tunataka uwekezaji katika kilimo, ni lazima tukubali kutoa ardhi tena kwa masharti nafuu. Kama tunataka wachimbe madini au wajenge viwanda au mahoteli, ni lazima tukubali kuwavutia kwa kuwapa unafuu fulani ambayo yatawafanya waje kwetu badala ya kwenda kwingine. Haya yakifanyika siyo kuuza nchi bali ni kujenga uchumi. Hivyo, Watanzania tunatakiwa tuelewe kuwa raslimali ni chache duniani, zinatafutwa sana na walio nazo wanagombaniwa na wengi. Tusione haya kuwavuta wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanaosema kuwa mpaka Watanzania wapate uwezo, mali zitakuwa zimekwisha na kuchukuliwa na wageni. Hili nalo kiuchumi si kweli. Kama uwekezaji utakuwepo wa kutosha, uchumi utajengeka na kipato cha Watanzania kitapanda. *(Makofi)*



Hii maana yake ni kuwa Watanzania watakuwa na hali nzuri zaidi ya maisha na umaskini utaondoka. Yule mgeni aliyefungua shamba kubwa na kuwekeza vizuri hatabeba hilo shamba au kiwanda na hatimaye hao hao Watanzania wataingia katika umiliki wa biashara hiyo ama wataanzisha biashara zao kwa sababu sasa wamepata uwezo wa mitaji, ujuzi teknolojia na elimu ya masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunawavutia wawekezaji wakubwa, juhudi pia lazima ziendelezwe kuwajenga wawekezaji wadogo na wa kati *small medium enterprises*. Hivi sasa kuna mwamko mzuri sana hasa kwa wakina mama wanaosindika matunda, vyakula na wenye viwanda vidogo vya kushona nguo na kutengeneza mapambo. Hili nalo ni kundi muhimu sana kwa sababu linajenga ajira nyingi sana kwa ajili ya uwingi wao. Aidha, kundi hili pia hushughulika na bidhaa za kawaida ambazo hutokana na shughuli za watu wa kawaida na hivyo kutawanya mapato kwa watu wengi. Ili kuyawezesha makundi kama haya, Serikali imekuwa ikitenga fedha kupitia mifuko mbalimbali kama Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana na wakati mwingine wafanyabiashara ndogondogo. Vikundi vya wanawake na vijana wanaokopa fedha hizo ambazo hupitishwa katika Halmashauri zao za Wilaya, Miji, Manispaa au Jiji wana wajibu wa kuhakikisha fedha hizo zinatumiwa kwa makusudio yaliyooombewa na pia zinarejeshwa kwa wakati ili makundi mengine nayo yakopeshwe. Kama taarifa iliyotolewa hapa Bungeni iliyotawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inavyoonyesha, Halmashauri nyingi sana hazijasimamia fedha hizo za wakina mama na zikarudishwa. Hii ni kinyume na kujenga uchumi na kuwawezesha Watanzania. Naagiza Halmashauri zote ambazo hazijafanya hivyo zifanye hivyo mara moja, fedha hizo zirudishwe ili makundi mengine yakopeshwe na iwe hivyo kwa makundi yote yanayopata fedha za kukopeshwa kupitia Halmashauri. Kila anayekopa awe mtu binafsi ama kikundi kione wajibu wa kwanza wa deni ni kulipa deni lenyewe. Serikali itatoa tu fedha kwa Halmashauri zile ambazo vikundi vyake vinarudisha fedha zilizokopeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa dhati na wewe mwenyewe Naibu Spika na Wenyeviti wetu Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Mheshimiwa Anne Makinda kwa kutuwezesha kukamilisha shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya mkutano huu. Aidha, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Kipenka M. Mussa na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma zao mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge. Naomba vilevile niwashukuru Watumishi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kuiwezesha Serikali kutimiza wajibu wake kikamilifu na hivyo kuliwezesha Bunge, kuhitimisha shughuli zilizokuwa zimepangwa kwenye mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo vilevile watu binafsi mmoja mmoja au taasisi na Asasi zisizo za Kiserikali ambazo zimeshiriki kutoa mawazo yao kwenye mikutano ya baadhi ya Kamati za Kudumu za Bunge. Napenda niwashukuru kwa dhati kwa kutumia muda na raslimali zao kufikisha hoja na michango yao ya mawazo ambayo bila shaka imezisaidia sana Kamati kufikia maamuzi yaliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Naomba pia niwatambue na kuwashukuru wale wote walioandaa semina mbalimbali zilizotuelimisha kuhusu masuala mbalimbali yenye uhusiano na Miswada iliyowasilishwa ndani ya Bunge au masuala ya kawaida ya harakati za maendeleo yetu. Navishukuru sana vyombo vyote vya habari kwa kazi yao nzuri ya kueleza yaliyokuwa yanatendeka ndani ya Buunge lako Tukufu, kwa kipindi chote cha mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 13 Aprili, 2004 siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 11.44 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 13 Aprili, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*